M A P

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

Nguvu ya Ukarimu

I N D

GARY KEESEE

U Z I

M A P

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

Nguvu ya Ukarimu

I N D

GARY KEESEE

U Z I

**Your Financial Revolution**
***Power of Generosity,*** Kiswahili By Gary Keesee

© Gary Keesee, 2023

Originally published in English
ISBN: 978-1-945930-52-2

Faith Life Now
P.O. Box 779
New Albany, OH 43054, USA

You can reach Faith Life Now Ministries on the Internet at
FaithLifeNow.com

**Mapinduzi yako ya Kifedha**
***Nguvu ya Ukarimu,*** Kiswahili na Gary Keesee

© Gary Keesee, 2023

Awali kilichapishwa katika lugha ya Kiingereza
ISBN: 978-1-945930-52-2

Faith Life Now
P.O. Box 779
New Albany, OH 43054, USA

Unaweza kufikia Faith Life Now Ministries kwenye Mtandao katika
www.faithlifenow.com

Isipokuwa imebainishwa vingine, Maandiko yote yametolewa kutoka kwa Tafsiri ya Biblia ya 'UNION' ya Biblia Takatifu. Hakimiliki ©1952, United Bible Societies, Tanzania. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

Manukuu ya Maandiko yaliyowekwa alama (EHV) yametolewa kutoka kwa Tafsiri ya 'Evangelical Heritage Version® (EHV®)' ya Biblia Takatifu. Hakimiliki © 2019 Wartburg Project, Inc. Haki zote zimehifadhiwa. Imetumika kwa ruhusa.

Kimechapishwa nchini Kenya. Haki zote zimehifadhiwa chini ya Sheria ya Hakimiliki ya Kimataifa. Yaliyomo na/au jalada haviruhusiwi kunakiliwa kwa ujumla au kwa sehemu kwa njia yoyote bila idhini ya kutoka kwa Mchapishaji.

# WAKFU

Kitabu hiki kimewekwa wakfu kwa mke wangu mrembo wa miaka 40, Drenda. Yeye ndiye mtu mkarimu zaidi kati ya wote ambao nimewahi kukutana nao. Yeye huwafikiria wengine kila wakati na amenifundisha mengi kuhusu kupenda watu, jambo ambalo ninamshukuru milele!

— Gary Keesee

# YALIYOMO

**UTANGULIZI** ........ ix

**SURA YA 1:** Nguvu ya Ukarimu ........ 1

**SURA YA 2:** Jibu: Neema ........ 15

**SURA YA 3:** Je Unastahili? ........ 37

**SURA YA 4:** Pesa Ni Za Nani Je? ........ 51

**SURA YA 5:** Unahitaji Mshirika! ........ 63

**SURA YA 6:** Siri Ya Zaka ........ 75

**SURA YA 7:** Unahitaji Mkoba Wa Fedha: Sehemu Ya Kwanza ........ 91

**SURA YA 8:** Unahitaji Mkoba Wa Fedha: Sehemu Ya Pili ........ 115

**SURA YA 9:** Sheria Ya Kipimo! ........ 125

**SURA YA 10:** Mfalme Mkarimu ........ 137

**SURA YA 11:** Ahadi Kwa Walio Wakarimu ........ 153

# UTANGULIZI

Mungu aliponiita mimi na Drenda kufanya huduma ya TV, lazima nikiri kwamba kawaida nisingekuwa na wazo kama hilo hata kidogo. Nilikuwa nimerudi kutoka Albania, ambako nilifundisha katika vikao vitano kuhusu Ufalme wa Mungu na kuwaambia jinsi mimi na Drenda tulivyotoka kwa madeni kwa kufuata sheria za Ufalme.

Ikiwa umesoma vitabu vyangu vilivyotangulia, unaweza kukumbuka jinsi ukungu wa utukufu wa Mungu wa rangi ya samawati ulivyojaza sebule ya mmisionari usiku baada ya kumaliza kikao cha mwisho. Hapo ndipo Bwana aliniambia, *"Ninakuita kwa mataifa ili uwafundishe watu agano Langu la baraka za kifedha. Na popote nitakapokutuma, nitalipia matumizi."*

Usiku huo ulibadili maisha yangu. Hata hivyo, sikujua hasa Bwana alimaanisha nini aliposema, *"Ninakuita kwa mataifa."*

Nilivyokuja kutambua, televisheni ilikuwa njia moja ambayo Bwana angetumia. Tena, hilo si jambo ambalo ningefikiria kufanya au hata kutamani kufanya. Jambo moja ambalo nilijua kwa hakika ni kwamba nilikuwa na shauku ya kuwasaidia watu kugundua kile ambacho mimi na Drenda tulikuwa tumegundua—Ufalme wa Mungu.

Tulikuwa na madeni mengi, tulidaiwa na wakopeshaji wa kila aina, na nilikuwa nikipambana na mashambulizi ya hofu yanayodhoofisha kwa miaka tisa. Dawa za kuzuia huzuni nilizopewa na madaktari hazikusaidia. Nilianza kujitenga na wengine, na giza la hofu lilivamia mawazo yangu yote. Niliingiwa na woga hata nikafika mahali niliogopa kuondoka nyumbani kwangu, jambo ambalo bila shaka lilidhuru mauzo kwenye biashara yangu. Haraka tulikuwa tukiingia katika hali ya kufilisika, wala sikuwa na uwezo wa kuzuia hilo. Sasa aibu ilikuwa kawaida kwangu, na nilihisi kama mtu aliyeshindwa. Pakubwa nilihisi kama mtu aliyeshindwa machoni mwa mke wangu mrembo na watoto wangu. Zaidi ya kutokuwa na fedha zilizohitajika

na familia yangu, sikuwa baba au mume bora katika miaka hiyo.

Tuliishi katika nyumba nzee mashambani ya miaka ya 1850 ambapo kila kitu kilikuwa kimechakaa. Madirisha yalikuwa yameunganishwa na mkanda wa bomba. Tulikuwa tumeokota zulia ya sakafu kando ya barabara kwenye rundo la takataka. Magodoro ambayo vijana wangu walikuwa wakilalia tulitoa kwenye rundo la yale yalikuwa yametupwa kutoka kwa nyumba ya wazee. Magari tuliyoendesha yalikuwa ya aibu. Tulipigiwa simu mara kwa mara na mawakili na kampuni za kadi za mkopo na kampuni za mikopo tulizodaiwa nazo.

Sikuwa na tumaini! Ndio, nilikuwa Mkristo aliyempenda Mungu. Nilikuwa mshirika kanisani na nilikuwa nimejazwa na Roho Mtakatifu. Nilikuwa na Shahada ya Kwanza katika mafundisho ya Agano la Kale na nilikuwa nimesoma mwaka mmoja katika shule ya Biblia, lakini kulikuwa na kasoro mahali!

Siku moja katika hali ya kukata tamaa, nilimlilia Mungu, na alijibu mara moja. Si kwamba sikuwa nimeomba katika miaka hiyo tisa yenye shinikizo. Lakini wakati huu, nilihitaji kusikia kutoka kwa Mungu.

Nafikiri hadi wakati huo, nilidhani kwamba wakati wowote ningejiondoa kwenye shimo la kifedha ambalo nilikuwa nimechimba kwa kufanya mambo kwa nguvu zangu mwenyewe. Lakini asubuhi hiyo nilikuwa nimetosheka. Nilikuwa nimekopa kutoka kwa marafiki wangu wote, na makumi ya maelfu ya dola kutoka kwa wanafamilia, na kila njia ambayo ningetumia kukopa zaidi ilikuwa imefungwa.

Nilipoomba asubuhi hiyo, nilikuwa nimekwisha kukata tamaa, na hivyo nilishangaa Mungu alipojibu haraka sana. Kutoka ndani ya roho yangu nilimsikia akininukuu Wafilipi 4:19:

> *Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.*

Nilimjibu Bwana, “Bwana, najua andiko hilo, lakini sioni hilo likitendeka maishani mwangu.” Alinena nami tena na kusema kwamba nilikuwa katika shinikizo hilo kwa sababu sikuwa nimewahi kujifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi. Sikujua alimaanisha nini aliposema hivyo, lakini mimi na Drenda tuliazimia kujua.

Moja ya Maandiko ya kwanza ambayo Mungu alituonyesha ni Luka 6:20:

*Akainua macho Yake akawatazama wanafunzi Wake, akasema, "Heri ninyi mlio maskini, kwa sababu ufalme wa Mungu ni wenu."*

Ufalme wa Mungu ulikuwa jibu letu?! Tena, kwa kweli hatukuwa na fununu alichomaanisha, lakini tulitaka kujua.

Tutazungumza zaidi kuhusu Ufalme baada ya dakika moja, lakini hebu nikwambie matokeo yalikuwa nini.

Roho Mtakatifu alianza kutuonyesha mambo katika Biblia ambayo hatukuwa tumeona hapo awali. Kwa kutumia yale ambayo Bwana alikuwa akitufundisha kuhusu Ufalme, tuliweza kutoka kwa madeni kabisa katika muda wa miaka miwili na nusu. Tulianza kununua magari yetu kwa pesa taslimu, tulinunua shamba la ekari 55 kwa pesa taslimu, ardhi yenye miti mizuri mirefu na mabwawa ambapo ningeweza kuwinda na kuwalea watoto wangu kwenye eneo lililo na nafasi.

Na mojawapo ya furaha yangu kuu maishani ilikuwa kumtazama Drenda akibuni na kujenga nyumba ya ndoto yake, ambayo tunamiliki sasa bila deni pia.

Baada ya yale niliyoyapitia na baada ya kuona Ufalme wa Mungu ukifanya kazi maishani mwetu, tuliishi katika hali ya sherehe *kila siku*. Kwa kweli, sherehe haijakwisha. Bado tunasherehekea Ufalme kila siku. Bila shaka tunasherehekea kwa sababu tumeacha kutafuta pesa ndani ya matakia ya viti ili kupata kiasi kidogo cha senti za kununulia watoto wetu chakula cha kuwafurahisha na sasa tunaishi bila madeni na tunatoa mamia ya maelfu ili kusaidia kueneza Injili duniani kote.

Mimi na Drenda tuna shauku kuu ya kuwaambia watu kuhusu Ufalme wa ajabu wa Mungu. Hii ndiyo sababu nilikuwa nimeenda Albania.

Kama nilivyotaja awali, Mungu aliponena nami huko Albania kuhusu kwenda kwa mataifa, nilichanganyikiwa sana. Hiyo ilimaanisha nini? Wakati huo, nilikuwa mchungaji wa kanisa ambalo mimi na Drenda tulianzisha miaka kumi awali. Nilipaswa kujiuzulu kutoka kanisani na kuanza kusafiri?

Kupitia msururu wa kutambulishwa kwa watu uliowekwa na Mungu, mimi na Drenda tulikutana na watu ambao walifanya kazi katika makampuni ya runinga. Sio kwamba nilikuwa nikiwatafuta; Mungu ndiye aliyewaleta kwetu. Tena, sikuwa na nia ya kufanya huduma ya televisheni hata kidogo, lakini nilikumbuka maono niliyoyapata miaka kadhaa awali. Nilikuwa nikiomba katika mojawapo ya ibada za kanisa letu wakati, ghafla, Bwana aliniambia kwamba ningeanza kuwa na vipindi vya televisheni na redio. Sikufikiria hilo sana maana sikuwa na hamu nalo wakati huo, ingawa

lilivutia umakini wangu, na nilimwambia Drenda kulihusu.

Ili kufupisha hadithi ndefu, Mungu alifungua milango ya kushangaza na kutuletea watu wa ajabu ambao walituhimiza kufanya huduma ya televisheni, lakini hatukujua chochote kuihusu. *Na ninaposema hatukujua chochote, ninamaanisha hivyo kabisa*. Lakini tulihisi tulihitaji kuendelea kufuata kile Mungu alichokuwa akituonyesha.

Hatukuwa na vifaa wala kujua ni vifaa gani vilivyohitajika katika huduma ya televisheni, lakini watu ambao Mungu alituletea walikuwa na juzi. Hatimaye, tulifika mahali ambapo tulipaswa kufanya uamuzi. Kampuni ya televisheni ilitupa kandarasi ya kuandaa vipindi vyetu kwa bei iliyopunguzwa. Tulipohesabu muda wa kuwa hewani na gharama zote zilizohusika, tuliona kwamba ingegharimu takriban $300,000, wala hatukuwa pesa hizo wakati huo. Lakini baada ya kusali kuhusu jambo hilo na kuwa katika hali ya mapambano na Mungu, hatimaye nilikubali. (Bila shaka huwezi kamwe kuwa mshindi unapopambana na Mungu).

Kwa hivyo kampuni ya kuandaa vipindi vya televisheni ilikuja mjini (kutoka Texas), kisha tukaanza kurekodi kipindi chetu cha kwanza. Maana hatukuwa na studio, tulirekodi mwaka wetu wote wa kwanza kwenye sebule yetu mbele ya mahali pa moto. Kusema nilikuwa na woga nilipofanya kipindi cha kwanza ni kupuuza. Sikujua cha kutarajia. Na haikuwa kurekodi kipindi hicho ambako kulinifanya kuwa na wasiwasi. Ilinibidi niandae programu nzima, bila shaka yakiwemo maoni ya Drenda. Timu ya kurekodi vipindi hivyo ilitupatia ushauri mzuri na kutufundisha, lakini bado sikuwa na raha.

Tafadhali elewa kwamba mimi kawaida si mtu wa watu, kwa hivyo kurekodi vipindi vya televisheni kulikuwa nje ya faraja yangu. Kando na hayo, timu ya wanatelevisheni waliokuwa wakirekodi walikuwa wamechanganyikiwa sana. Asubuhi hiyo kabla ya kuanza kurekodi, waliniambia kwamba mkuu wa timu yao alikuwa ameondoka usiku wa manane kwa sababu mwanaye mchanga alikuwa amegongwa na gari la jirani kwenye barabara kuu, na kufariki. Niliamua kutomwambia Drenda hadi baada ya kumaliza kurekodi. Hilo lilikuwa jambo gumu.

Kisha, moja kwa moja baada ya kurekodi, mmoja wa wafanyakazi wetu alikuwa akiendesha baiskeli ya mwanangu Tim na kuigonganisha. Tim alikuja mbio ndani ya nyumba huku akipiga kelele kwamba David amekufa. Hakuwa amekufa, aligongwa tu, lakini huo ulikuwa mwanzo mgumu.

Tuliweza kufaulu katika wiki hiyo ya kurekodi, na kipindi kiliwekwa

hewani kwenye kituo cha televisheni cha mtaani. Tuliendelea kurekodi wiki moja kila mwezi, lakini mwishoni mwa mwezi wa pili, haikuwa rahisi maana nilikuwa nikipambana na hisia za kutostahili na hofu, zote wakati mmoja. Hatimaye nilimwambia mmiliki wa kampuni ya kurekodi kwamba singeweza kuendelea. Alinitazama kwa muda mfupi na kusema, "LA! Lazima uendelee!

Kisha akaniambia niketi kitini kwa sababu alitaka kunionyesha jambo. Aliwasha runinga na kufungua sehemu ya Kikristo ya mitandao. Kusema kweli, sikuwa nimewahi kutazama vipindi vingi vya Kikristo, lakini nilichokiona siku hiyo kilinipa hisia mbaya na kunifanya nifikirie upya ikiwa kweli nilitaka kujihusisha na huduma ya televisheni hata kidogo.

Katika programu moja, walikuwa wakiuza "mafuta matakatifu ya zeituni" ambayo walidai yangeleta upako mkubwa zaidi wa kufanikiwa. Kwa kipindi kingine, mhubiri alikuwa akiuza "mikate iliyotiwa mafuta," akisema kwamba utapata ufunuo mpya kila uilapo. Katika kipindi kingine, nilisikia kwamba ukitoa kabla ya dakika tatu kuisha, utapata upako mara tatu wa kufanikiwa. Katika kingine, chakula kilichokaushwa kilitolewa. Kila kipindi kilitoa aina fulani ya motisha ya ajabu ili kuwafanya watu watoe.

Lakini sehemu ambayo sikuona ni kwamba hakuna hata mhubiri mmoja aliyewaambia watu jinsi ya kupokea kile walichohitaji—jinsi Ufalme unavyofanya kazi kihalisi. Walikuwa wakiwaambia watu wapande mbegu, lakini mtu alihitaji kuwaambia jinsi ya *kuvuna* mbegu hiyo!

Kulikuwa na vipande vingi vya fumbo ambavyo watu walihitaji kujifunza ili kuona mafanikio. Kuwafundisha watu jinsi ya kutoa tu na si jinsi ya kuvuna, nilijua kwamba watu wangekatishwa tamaa na kufikiri kwamba Mungu alikuwa amekosa kuwafanikisha wakati mambo hayatokei jinsi walivyotarajia.

Watu walihitaji kujua sheria za Ufalme na kwa nini kutoa ni sehemu muhimu sana katika kuona utele wa Ufalme hapa duniani. Na tena, muhimu zaidi, walihitaji kujua cha kufanya *baada ya* kutoa. Walihitaji kujua jinsi ya kuvuna kile walichohitaji kutoka kwa Mungu.

Niligundua kwamba nina sehemu ya kutimiza katika mavuno yangu—ambayo ya kwanza ni kujifunza imani ni nini na kwa nini inahitajika. Nilihitaji kujifunza jinsi Roho Mtakatifu anavyoongoza mtu kwenye mavuno na jinsi wakati mwafaka na maelezo kuhusu mavuno yalivyo mambo muhimu. Niligundua kwamba kuna sheria za kiroho nilizohitaji kujifunza ambazo huathiri mavuno zinapotumiwa pamoja na sheria za ulimwengu wa asili.

Vipindi hivyo vyote vilifanya ionekane kana kwamba pesa zingejitokeza tu kwenye kisanduku cha barua.

Nitakubali kwamba wakati mwingine pesa *hujitokeza* kwenye kisanduku cha barua, lakini ukichunguza matukio hayo kwa ukaribu, utapata vidokezo vya kiroho kuhusu sababu na jinsi yalivyotukia.

Baada ya kutazama vipindi vichache, niliaibishwa na kile nilichokiona. Haishangazi watu hawavitazami. Lakini pia nilikuwa na hasira. Niligundua wakati huo kwamba nilihitajika, kwamba nilikuwa na kitu cha kusema.

Niliamua kuendelea na huduma ya televisheni kwa sababu nilikuwa na hadithi ya kusimulia. Na nimeendelea kwa miaka 14 iliyopita na nimeona makumi ya maelfu ya watu wakigundua Ufalme ni nini—si dini bali Ufalme—na wamekuwa na matokeo kama yangu na Drenda.

Najua utakuwa na matokeo sawa pia.

Kitabu hiki, *Your Financial Revolution: The Power of Generosity*, ni kitabu cha tano na cha mwisho katika mfululizo wangu uitwao Mapinduzi ya Kifedha. Nimefurahia kukamilisha mfululizo huu, na nina msisimko kuhusu kitabu hiki cha mwisho.

— Gary Keese

SURA YA 1

# NGUVU YA UKARIMU

Jioni moja tulikuwa tukila chakula cha jioni pamoja kama familia katika mkahawa fulani tunaopenda mtaani mwetu. Mhudumu alikuwa mwanadada ambaye alikuwa mjamzito sana. Nilipokuwa karibu kulipa bili yetu, ghafla nilihisi kumpa bakshishi kubwa kuliko ile ambayo mimi hutoa kwa kawaida, kwa hivyo niliongeza $100. Alichukua risiti niliyokuwa nimetia saini bila kuitazama na kurudi kuelekea jikoni.

Ndani ya dakika moja, alirudi huku machozi yakimtoka. Alirudi kutushukuru. Alituambia jinsi alivyokuwa katika hali ngumu ya kifedha na alikuwa akishangaa angeishije. Tulipata fursa ya kushiriki Kristo pamoja naye na kumwombea kabla ya kuondoka.

Hatukufanya lolote ila kuwa wakarimu na hilo lilifungua mlango wa huduma kwa moyo wake.

> *Au waudharau wingi wa wema Wake na ustahimili Wake na uvumilivu Wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate **kutubu**?*
>
> — Warumi 2:4

Tafsiri ya Kimombo ya King James inasema kwamba wema wa Mungu hutufanya tutubu.

**Kuwa mkarimu ni kutenda kama Mungu anavyotenda.**

Mathayo 5:45 inasema:

> *Ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana Yeye huwaangazia jua Lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.*

Mungu ni mwema, na ni mkarimu! Sisi ni watoto Wake, na asili yetu mpya katika Kristo ni kuwa wakarimu pia. Kama katika hadithi niliyosimulia hapo juu, kuwa mkarimu ni kushiriki moyo wa Mungu kuhusu watu. Kama vile kunywa maji baridi wakati wa joto jingi kunavyoleta kitulizo na tumaini, ndivyo kuwa mkarimu kunavyofanya ulimwenguni palipo na majangwa ya umaskini.

Athari ya ukarimu inaonekana wazi katika maagizo ya Paulo aliyoyaandikia kanisa la Korintho katika 2 Wakorintho 9:10-15:

> *Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*
>
> *Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu; kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.*

Ukarimu huwafanya watu wamsifu na kumshukuru Mungu!!! Tazama kwamba Paulo alisema kuwa mkarimu ni *utumishi* wako kwa Mungu.

Ufafanuzi wa neno huduma ni: *Kutenda kazi au jukumu kwa mkuu au kama mtumishi*.

Ni sehemu ya wajibu wako kwa niaba ya Mungu, hapa duniani, kushiriki moyo Wake na kuwajali watu. Matokeo ni wazi—hilo hugusa mioyo ya watu na kuwafungua ili wampokea Kristo.

Nafikiri sote tunaweza kukumbuka wakati mtu fulani alikuja kutusaidia na jinsi tulivyohisi.

Nakumbuka nilikuwa na deni la dola 4,000 za kodi mwanzoni katika ndoa yetu na sikujua nipate pesa wapi. Nililala macho usiku mwingi nikihofia hali yangu. Tulikuwa tunaishi Tulsa wakati huo na tulikuwa kwenda likizo huko Ohio.

Babangu aliponiuliza juu ya hali yetu, nilimwambia kuhusu deni la ushuru, naye akasema, "Vema, hiyo ni rahisi kurekebisha," hundi na kuniandikia kiasi chote cha pesa nilizodaiwa. Ukarimu wake wa papo hapo kwangu wakati huo ulinifanya kumpenda babangu hata zaidi kuliko nilivyompenda awali. Maana papo hapo niliona moyo wake kunihusu.

Babangu mara nyingi alificha moyo wake. Hakuwahi kuonyesha hisia zake waziwazi kwa watu, hata kwa mamangu. Hakuwa amewahi kuniambia ananipenda maisha yangu yote hadi wakati huo, kwa kadiri nilivyoweza kukumbuka. Ni wakati mmoja tu ambapo mamangu alimwambia aniambie kisha mwishowe akakubali, baada ya mabishano mengi. Naweza kukumbuka siku hiyo kana kwamba ni jana. Mama alimsihi, akisema, "Huwezi kumwambia mwanao kwamba unampenda?" Lakini alikaa kimya.

Hatimaye, huku mamangu akitiririkwa na machozi, Baba aliniambia ananipenda. Lakini sikuhesabu wakati huo mmoja aliponiambia ananipenda kwa sababu alilazimishwa kufanya hivyo.

Badala ya kutuambia kwa maneno kwamba anatupenda, kuna nyakati ambapo babangu alitununulia vitu spesheli, na nafikiri sisi watoto wanne tulifahamu kwamba baba alitupenda. Tuliuona moyo wa baba kwa yale aliyoyafanya tu, wala si kwa yale aliyoyasema. Nilithamini sana nyakati hizo maana kwangu ziling'aa kama taa gizani.

Siku baba aliponiandikia hundi ya deni la ushuru, moyo wangu ulijawa na shukrani. Kwa machozi nilimkumbatia na kumshukuru. Nilipigwa butwaa na jibu lake. Alisema, "Mradi ninazo, nataka kuwa msaada."

Nina hakika kama mimi una kumbukumbu za ukarimu wa mtu fulani, wakati uliovutia umakini wako. Kwa hivyo, tia hili akilini mwako:

**Ukarimu huonyesha watu moyo wako na moyo wa Mungu juu yao.**

Ukarimu una nguvu sana. Unapita maneno na kwenda moja kwa moja hadi moyoni. Inashangaza jinsi tulivyo na uwezo wa kukumbuka pongezi au zawadi ambayo mtu fulani alitupa.

Moja ya nyakati za kwanza nilipouona moyo wa babangu nilikuwa katika darasa la sita. Wakati huo mimi na binamu yangu tulikuwa tunapenda mifano ya roketi, na nilikuwa nimenunua moja ambayo ungeweza kuweka vitu ndani na kuvirusha angani.

Siku hii mahususi, mimi na binamu yangu tulifikiri kuweka chura kwenye ncha ya roketi na kuifunga ili roketi ianguke badala ya kufungua parachuti yake. Kusudi lilikuwa kuona ni nini kitamfanyikia chura, jambo ambalo nafikiri tayari unajua.

Kweli, tulirusha roketi na, kwa mshangao wetu, babangu alikuwa ametoka nje kututazama. Tulijua hangefurahishwa kwamba tumemuua chura.

Roketi ilipaa juu kama ilivyotakiwa kisha ikajikunja na kuanguka ncha kwanza ardhini. Nilipoenda kuichukua, niliona ncha ilikuwa imevunjika na chura alikuwa amekufa kama nilivyotarajia.

Nilipookota roketi, niliitupa kando yule chura aliyekufa haraka ili kuficha nia yetu ya kweli kutoka kwa babangu. Alinikaribia na kuniomba ile roketi. Bado nakumbuka jinsi alivyoijali sana roketi yetu. Alipoishikilia ile mikononi mwake, alianza kuniambia jinsi ningeweza kuikarabati na jinsi alivyosikitika kwamba ilianguka. Kisha akaelezea kwa undani jinsi ningeweza kujenga upya vipande vilivyovunjika. Jinsi sauti yake ilivyosikika kuwa ya kujali sana na kujawa wema, nilitiwa hatiani kwa kosa langu. Hakujua kuhusu chura, lakini sikusahau kamwe upole wake kwangu na roketi yangu. Ilidhihirika kwangu wakati huo kwamba alinijali sana.

Kisha kuna nyakati ambazo Mungu hutumia watu tusiowajua kututia moyo na kutufikia.

Wakati mmoja kama huo ninaokumbuka vyema ni wakati ambao mimi na Drenda tulikuwa tumeenda kuwinda ndege na marafiki wengine. Mimi na Drenda tulikuwa wanandoa wapya na tulikuwa tunaishi Tulsa. Mmoja wa wanafunzi wenzangu ambaye alikuwa anaishi kule Kansas alitualika tujiunge naye katika siku ya kwanza ya msimu wa kuwinda ndege wa mwaka huo. Kusema kweli nilifurahi sana.

Tuliendesha gari kwa masaa matano hadi Kansas, tukawa na siku nzuri sana ya kuwinda, na kupata ndege waliotutosha. Lakini tulipokuwa tukirudi Tulsa, injini ya gari ya rafiki yetu iliharibika. Tulikuwa katikati ya mahali pasipokuwa na watu kwenye barabara ya ardhi na masaa mengi kutoka nyumbani. Ikiwa umewahi kwenda Kansas, basi unajua jinsi eneo hilo lililo na ukame.

Sasa giza lilikuwa limeingia, na tuliona taa moja tu kwa mbali.

Tulitembea hadi nyumbani kwa mkulima huyo na kumweleza hali yetu. Nilishtuka sana aliposema, "Vema, nitawapeleka nyumbani usiku wa leo. Nitaweka gari lenu juu ya trela yangu, kisha nitawarudisha nyumbani kwenu ili mweze kwenda kazini Jumatatu." (Drenda alikuwa aanze kufanya kazi mpya ya muda asubuhi ya Jumatatu katika mkahawa fulani, na alikatishwa tamaa sana kwamba angehitaji kuwapigia simu kusema kwamba hangeweza kuwa hapo.)

Cha kushangaza ni kwamba, mtu huyo, ambaye hatukumjua hapo awali, alitupeleka nyumbani Tulsa kwa masaa tano kisha akageuka na kuendesha gari hadi Kansas kabla ya asubuhi kufika. Aliendesha gari usiku kucha!

Sitasahau kamwe tendo hilo la fadhili lisilo na ubinafsi. Hakutaka hata senti moja ya petroli. Nitamshukuru mtu huyo milele. Kila ninapomkumbuka, huwa nafikiria ukarimu wake kwa shukrani.

Watu wanapokukumbuka, watamshukuru Mungu kwa ukarimu wako.

**WATU HUMSHUKURU MUNGU KWA NEEMA KUU ALIYOWAPA WALE WALIO WAKARIMU!**

Nina hakika kwamba unaweza kufikiria hali kama hizi katika maisha yako mwenyewe. Utakumbuka jinsi ulivyokuwa na shukrani mtu alipokujali na kukutunza. Vema, hiki ndicho Paulo alichokuwa akiliambia kanisa hili la Korintho—ukarimu wao ulikuwa ukiwaonyesha watu moyo wa Mungu kuwahusu na kuwafanya watoe sifa na shukrani Kwake kwa ajili ya huduma yao Kwake.

Nilipookoka, niliona kwamba moyo wangu ulifanyika mwororo, na nikaona kwamba kweli nilijali watu. Nilipoona uhitaji, kila wakati nilitaka kusaidia, lakini ilifadhaisha sana kwa sababu kwa kawaida sikuweza kwa sababu sikuwa na pesa.

Nimegundua kwamba hivi ndivyo watu wengi wanavyohisi pia. Uliza katikati ya umati njia ya kwenda mahali, na utakuwa na watu kadhaa wanaotaka kukusaidia.

Lakini kama nimeshagundua katika Biblia, kuwa mkarimu kuna nguvu zaidi kuliko nilivyofikiri. Kusoma kifungu hiki katika 2 Wakorintho 9 kulifunua sheria ya Ufalme ambayo ilibadili kila kitu nilichofikiria kuhusu kutoa:

> *Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani*

*nyingi apewazo Mungu.*

*Kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote.*

*Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya <u>neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu</u>. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!*

— 2 Wakorintho 9:12-15

Watu humshukuru Mungu kwa neema kuu aliyowapa wale walio wakarimu!

Ili kuelewa kihalisi ukweli anaosema Paulo hapa, tunahitaji kufafanua maneno haya.

Kuzidi sana: ya kiasi kikubwa au shahada ya juu; kuzidi, bora, au isiyo ya kawaida: *<u>miundo ya utukufu kupita kiasi</u>*.

Ni nini kitakuwa chako kwa kiasi kikubwa? Nini kitakuwa cha ajabu na kuzidi ukuu katika maisha yako? Neema ya Mungu!!!!!

Sawa, sasa tunahitaji ufafanuzi wa neema.

Neno **neema** linamaanisha kibali cha Mungu kisichostahiliwa.

Hii ndiyo fasili ya kawaida ya neema, lakini inapungukiwa sana na maana kamilifu. Hebu nikupe ufafanuzi bora zaidi.

Ifuatayo ni nukuu kutoka kwa Wikipedia kuhusu neema ya Mungu:

*Mafundisho ya kawaida ya kurasa za mtandao wa Kikristo ni kwamba neema ni rehema isiyostahiliwa (neema) ambayo Mungu alitoa kwa wanadamu kwa kutuma mwanawe kufa msalabani, na hivyo kutoa wokovu wa milele. Hata hivyo, ufafanuzi huu pekee haushughulikii matumizi yote ya neno hili katika maandiko. Kwa kielelezo, Luka 2:40 (Tasfiri ya Biblia ya 'UNION'), "Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu Yake." Katika mfano huu unapotumia ufafanuzi wa neema kumaanisha kibali kisichostahiliwa haileti maana kwamba Kristo asiye na dhambi angehitaji hili.*

*James Ryle anapendekeza "Neema ni Uwepo wa Mungu utiao nguvu za kukuwezesha kuwa yule uliyeumbwa kuwa, na kufanya yale aliyokuita kufanya." Kwingine, Bill Gothard anapendekeza "Neema hutupatia hamu na nguvu ya Mungu inayohitajika katika kutimiza mapenzi Yake." Fasili hizi zote mbili zinaleta maana nzuri ya neno neema katika Biblia nzima.*

Kwa hiyo, tunaona kwamba kile Paulo alichozungumzia katika kifungu hiki ni neema, au kutiwa nguvu, ili kufanikiwa. Karama hii ya neema, ilisifiwa kwa sababu iliwawezesha watu kufanikiwa. Na kwa vile walikuwa wakarimu kwa kutimiza mahitaji ya wengine, hilo liliwafanya watu wamwabudu Mungu.

Paulo anamalizia mazungumzo yake kwa kusema, "**Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!**"

Sawa, ufafanuzi mmoja mwingine. Kutoweza kukisifu kama ipasavyo maana yake ni wazi kwamba, hakuna maneno yanayoweza kukielezea vya kutosha. Hiki ndicho Paulo alichomaanisha, kwamba karama ya neema ilikuwa nzuri *zaidi kupita maneno*, na hasa kwa wale waliosaidika na fedha ambazo ilileta.

Hii ni nguvu inayoweza kukuweka huru kutoka kwa utumwa wa kifedha. Nguvu hii ya neema ya Mungu, inapatikana kwa kila mwamini.

Lakini hapa kuna suala. Tunaweza kutumia muda mwingi kuzungumza kuhusu kile ambacho Paulo alisema tufanye—yaani kutoa. Lakini ikiwa hatuelewi neema, ambayo ni uwezeshaji wa kufanikiwa kwa uwezo wa Mungu, tunakosa mavuno aliyoyakusudia Mungu kwa ajili yetu. Ni kama kupanda bustani yako msituni chini ya kivuli cha mti mkubwa—hakuna mwanga wa jua, hakuna nguvu za kuleta matokeo unayotamani.

Mimi na Drenda tulisoma hadithi katika Biblia ambapo nguvu za Mungu zilidhihirika na kubadili kabisa hali kuwa nzuri. Itabidi nikiri kwamba tulisikia hadithi chache sana kama hizo zikitokea katika kanisa letu tulipokuwa tukikua. Nje ya wokovu, hakuna mtu aliyewahi kuzungumza kuhusu jinsi ya kuleta neema ya Mungu katika hali fulani.

Ninaelewa kwamba wokovu wetu ndilo jambo muhimu zaidi. Lakini kama nilivyotaja, nilihitaji neema hiyo hiyo kufanya kazi katika kila eneo la maisha yangu, lakini sikujua jinsi ya kusababisha hilo. Na kwa sababu ya ujinga wangu, tulikosa pesa, tulikuwa wagonjwa, na wenye huzuni. Tulijua kuhusu wokovu—suala la wokovu wetu wa milele lilikuwa limeshughulikiwa kikamilifu—lakini hatukujua au kuelewa jinsi ya kuleta mbingu maishani mwetu na kudhihirisha nguvu za Mungu. Kama nilivyokuambia, tulikuwa katika janga la kifedha!

Lakini siku ile Bwana aliponena nami kuhusu Ufalme alisema, "*Uko katika hali hii mbaya kwa sababu hujawahi kujifunza jinsi Ufalme Wangu unavyofanya kazi!*"

Kwa maneno mengine, alikuwa akisema kwamba sikujua jinsi ya kuachilia mamlaka ya Mfalme hapa duniani. Sikuwa nimewahi kujifunza

jinsi ya kufanya hivyo wala kufahamu kwamba hilo lingewezekana. Sikujua hata kidogo jinsi ya kupata neema, yaani nguvu ya Mungu.

Kulikuwa na mengi zaidi aliyoyanena Mungu katika yale mazungumzo kuhusu Ufalme. Alisema, "*Kanisa Langu linaishi kama wana wa Israeli walivyoishi utumwani, walipokuwa wakimtengenezea Farao matofali. Ni watumwa! Watu Wangu wana madeni, na ninawataka wawe huru!*"

Hebu nitoe hoja hapa: Hutawahi kuwa huru hadi utakapokuwa huru kifedha. Na kama vile mimi na Drenda tumesema kwa miaka 30, hutawahi kugundua wewe ni nani na kutimiza kusudi la kiroho la maisha yako hadi utakaposuluhisha suala la pesa.

Na hebu niseme kwa uwazi pia: **UNAWEZA KUWA HURU!**

Nilithibitisha, na maelfu ya wengine wamethibitisha pia. Neema ya Mungu ipo ili kukusaidia. Kuna mambo umeitwa kufanya ambayo hutaweza kuyatimiza kama mtumwa. Ni lazima upate uhuru wa kifedha si kwa ajili yako mwenyewe na familia yako tu bali pia ili watu waweze kuona Ufalme wa Mungu ukitenda kazi maishani mwako, na, kama mti wa matunda uliosheheni matunda yaliyoiva, utavutia watu kwenye Ufalme.

Watu wanatafuta majibu. Wanatafuta mpango halisi. Wanahitaji sana kuona Ufalme wala si dini.

**WATU WANATAFUTA MAJIBU. WANATAFUTA MPANGO HALISI. WANAHITAJI SANA KUONA UFALME WALA SI DINI.**

Acha nikusimulie mazungumzo niliyokuwa nayo na wauguzi wawili majuzi.

Mamangu ana umri wa miaka 88 na anaendelea vyema, lakini anahitaji usaidizi wa kwenda hapa na pale, kama unavyoweza kufikiria. Kwa hivyo, siku hii maalum, nilipaswa kumpeleka kwenye miadi kadhaa ya daktari.

Nilipokuwa nikizungumza na muuguzi katika muadi wa kwanza, alianza kuniuliza ninafanya kazi gani. Nilimweleza kuhusu kanisa letu na pia kuhusu kampuni yangu ya kifedha na jinsi tunavyosaidia watu kutoka kwa madeni. Naam, hilo lilimvutia. Aliendelea kuniambia kwamba alikuwa na shida, alikuwa na deni kubwa, na hakujua jinsi angeendelea kuishi.

Tulipoenda kwa daktari wa pili siku hiyo, nilikuwa na mazungumzo karibu sawa na muuguzi yule wa kwanza. Kwa kweli alitokwa na machozi alipokuwa akinieleza kuhusu hali yake ya kifedha.

Rafiki, si wao tu. Hivi ndivyo Amerika ilivyo leo.

Moyo wangu na shauku yangu ni kuwasaidia watu kuelewa kwamba kuna njia bora ya kuishi—njia ya Ufalme.

Mimi na Drenda tulipoanza kujifunza kuhusu Ufalme wa Mungu na kuanza kutumia yale ambayo Mungu alikuwa anatufundisha kuhusu Ufalme, maisha yetu yalibadilika sana. Tulianza kuona ile neema Paulo aliyozungumzia ikidhihirika maishani mwetu.

Usiku mmoja, niliota ndoto kuhusu kuanzisha biashara yetu wenyewe ya kusaidia watu kutoka kwenye madeni. Lilikuwa jambo la kichaa, sivyo? Mtu maskini kuendesha kampuni ya kuonyesha watu jinsi ya kutoka kwa madeni, ni Mungu tu, sivyo?

Huenda ukauliza, "Hilo lilifanyikaje? Ulijuaje jinsi ya kutoka kwa madeni ili kuweza kusaidia watu wengine?" Hilo ni swali nzuri!

Ili kufipisha hadithi ndefu, Roho Mtakatifu alinionyesha jinsi ya kufanya hivyo.

Bila shaka, nilikuwa na mambo ya kujifunza katika ulimwengu wa asili, kisha ilinibidi niwe na watu wa kunifundisha jinsi ya kuanzisha kampuni yangu, lakini Roho Mtakatifu alielekeza maendeleo na mikakati na mbinu za kipekee tulizotumia kuwasaidia watu. Kampuni hiyo ilinawiri na ndiyo iliyofadhili uhuru wetu wa kifedha.

Nafikiri ninajua unachofikiria: Lazima tulitoza pesa nyingi kwa usaidizi huo ikiwa hapo ndipo tulipopata pesa zote tulizohitaji ili kuwa huru.

La. Kama nilivyosema, Roho Mtakatifu alitupa mtindo wa kipekee wa biashara, na ndio huu hapa:

Tunafanyia wateja wetu kazi BILA MALIPO.

Je, ninawezaje kumlipisha mtu ambaye tayari anatatizika kulipa bili? La hasha, siwezi kufanya hivyo. Mungu alinipa njia tofauti ya kufadhili kampuni yangu. Sijawahi na kamwe sitawahi kulipisha wateja wangu malipo ya kuwatayarishia mpango wa kibinafsi wa kutoka kwa madeni. Kampuni yangu ina utaalam wa kuwaonyesha wateja jinsi ya kutoka kwa madeni katika chini ya miaka saba, ikijumuisha rehani yao ya nyumba, kwa kawaida bila kubadili mapato yao.

Hatulipwi na wateja wetu bali na kampuni nyingi, wachuuzi na wataalamu ambao tumechagua kutoa masuluhisho na njia tofauti za kujijenga upya kwa wateja wetu. Wanatulipa kwa kuwaambia wateja wetu kuwahusu.

Kwa mfano, katika mchakato wetu wa kuleta suluhu, ikiwa najua kwamba kampuni ya fulani inaweza kupunguza malipo ya bima ya mteja wangu, huwa namwambia aangalie kampuni hiyo. Anapozungumza na kampuni hiyo anafanya uamuzi wake binafsi ikiwa anavutiwa na viwango vyake vya bei nafuu kama sehemu ya mpango wake wa kujijenga upya au la.

Kwa hiyo, kwa mteja, kila kitu ni bila malipo. Na nina hakika hii ilikuwa sababu kuu iliyochangia ukuaji wa kushangaza wa kampuni yetu. Soma kuhusu kampuni yetu katika forwardfinancialgroup.com.

Pia tunasaidia watu kufahamu kile ninachoita uwekezaji salama: kuwekeza bila hatari ya misukosuko iliyo katika masoko kuwaibia pesa zao za thamani za kustaafu.

Nimesema hayo yote kusema kwamba katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, tumezungumza na mamia ya maelfu ya watu, na tumeona tatizo ambalo Wamarekani wengi wanakabiliwa nalo.

Nina mfano mmoja ninaokumbuka dhahiri kuhusu jinsi Wamarekani wengi wanavyoishi.

Mwanamke mmoja alinipigia simu nimtembelee, kwa kuwa alihitaji msaada kuhusu deni lake. Mimi na mmoja wa washirika wangu tulienda kukutana naye, na niliketi pale nikiwa nimepigwa na butwaa alipokuwa akieleza hali yake. Alikuwa na kadi 32 tofauti za mikopo, zote zikiwa zimetumika hadi mwisho. (Ndio, umesikia vyema—alikuwa na kadi 32 za mikopo.)

Alikuwa amefaulu katika kujenga gereza lake mwenyewe, na alikuwa akiniomba ufunguo wa kutoka. Akilini mwangu, jibu lilikuwa rahisi: Koma kutumia kadi za mikopo. Huo ungekuwa mwanzo mzuri. Kwa hiyo, nilimwambia akate-kate kadi hizo na kusisitiza kwamba aishi kulingana na mapato yake. Kisha nikampa kazi ya kutengeneza orodha ya gharama zake zote ili nijue nianzie wapi katika kumshauri. Pia nilipendekeza aanze kutumia kadi ya benki inayotumiwa wakati kuna pesa kwa akaunti tu badala ya kadi yoyote nyingine ya benki ili kuepuka kufanya hali yake kuwa mbaya zaidi.

Kwa pendekezo la kukata-kata kadi zake, alijawa na machozi papo hapo na kuuliza swali hili la kushtua: “Nitawezaje kununua viatu?”

Je, nilisikia vyema? Hakuwa na pesa za kutosha kununua chakula, lakini alikuwa akiuliza kuhusu viatu?

Unaweza kufikiri kwamba mwanamke huyo hakuwa mtu wa kawaida. Katika idadi ya kadi za mikopo alizokuwa nazo, haikuwa kawaida. Lakini inapohusu kuwa katika jela kifedha, ni kawaida. Angalia takwimu za hivi punde nchini Marekani:

- 57% ya watu hawana $1,000 katika benki.
- 44% hawawezi kulipa bili isiyotarajiwa ya $400.
- 23% ya Wamarekani hawawezi kulipa bili zao za kila mwezi na wanaingia zaidi na zaidi katika madeni kila mwezi.

Rafiki, Waamerika ni kama vile Mungu alivyoniambia—ni watumwa. Tafakari kuhusu kile ambacho mtumwa hufanya.

- Hafanyi kazi kwa manufaa yake mwenyewe. Ingawa anafanya kazi na anazalisha faida, faida hiyo hutumwa kwa wakopeshaji kila mwezi, na kuacha pesa za kutosha tu ili familia iweze kuendelea kuishi kwa mwezi mwingine.
- Mtumwa huishi katika nyumba asiyoimiliki (maana yake ana rehani).
- Yeye huendesha gari asilolimiliki kwenda kazini ili kulipia nyumba asiyoimiliki.
- Mavazi yake ya kwenda kazini aliyanunua na kadi za mikopo, ili kulipia gari na nyumba asiyoimiliki, pamoja na mkopo wa shule ambao bado analipia baada ya miaka 20.

Unaelewa.

*Tajiri humtawala maskini, naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.*
— Mithali 22:7

Je, unajua kwamba watu wengi hawapendi kazi zao? Kwa kweli, kura ya maoni ya Gallup inasema kwamba 85% ya wafanyikazi wanachukia kazi zao.

Kwa nini basi wameajiriwa pale? Kwa sababu wao ni watumwa, na watumwa hawana njia nyingine!

Kwa hiyo, je, kuna njia ya kutoka katika utumwa? Ndio!

Huniamini? Ngoja nikuonyeshe.

*Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu.*

*Kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote.*

*Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!*
— 2 Wakorintho 9:12-15

Hebu tuzingatie jibu hilo—neema ya Mungu, yaani uwezeshaji wa kufanikiwa!

Tambua pia kwamba adui anataka uishi maisha ya madeni na usijifunze njia ya kuwa huru. Ndiyo maana kuna *trilioni* 1.1 za kadi za mikopo zinazotumika Marekani. Pia ndiyo sababu ofa za kadi za mikopo bilioni nne hadi nane hutumwa kwa watu kila mwaka.

Kuna yule anayetaka uishi katika madeni, na sio benki au wauzaji tu wanaokuomba ujaribu kadi zao.

Shetani anajua kama anaweza kukuweka katika madeni, kamwe hutaweza kutimiza hatima yako ya kiroho, jambo ambalo anajua linaweza kuleta matatizo katika ufalme wake.

Kwa hivyo, hebu nikukumbushe kidogo. Kitabu hiki kinahusu kuwa mkarimu, sivyo? Jibu ni ndio na la. Ndio, tutazungumza juu ya faida zote za kutoa na kuwa mkarimu baada ya muda mfupi. Lakini kutoa peke yake sio jibu. Inakupasa kuwa na maarifa ya jinsi ya kupata neema, yaani uweza wa Mungu.

Kwa hivyo, hebu niseme tena: Mfumo wa kutoa peke yake, kama fomula, sio ufunguo. Ni sehemu yake, bila shaka, lakini ili kufanikiwa, wewe na mimi tunahitaji ule uwezo usio wa kawaida, wa ajabu uitwao neema.

Dustin na Kendall waligundua ninachosema. Walikuwa wanandoa wachanga ambao hawakuelewa kabisa kwamba walihitaji neema ya Mungu katika fedha zao hadi walipojikuta katika hali mbaya. Walikuwa wamepata wazo jipya la biashara na kuamua kuendelea nalo. Gharama? $150,000, na yote kupitia kwa madeni.

Mwezi huo huo walipoanza biashara hiyo, walikaguliwa na shirika la ushuru na walitozwa $53,000 kulipia kodi za awali. Dustin alisema walijikuta katika deni la zaidi ya $200,000 bila njia ya kutoka, haswa kwa vile mambo tayari yalikuwa magumu kifedha kabla ya kuanzisha biashara hiyo.

Hapo awali walikuwa wamekopa pesa za kulipa bili ya hospitali ya mtoto wao wa mwisho na walikuwa wakilipia hilo. Ukaguzi uliwasukuma kupita kiwango cha fedha walizokuwa nazo, na Dustin alihangaika kutafuta suluhisho.

Baada ya kutafuta, hatimaye alipata ofa ya mkopo wa $30,000, ambao uliidhinishwa, na akapeleka wazo hilo kwa mke wake ili kusikia maoni yake. Hakujua kwamba Kendall alikuwa akisoma na kutafakari kuhusu kitabu changu, *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kupumzika*, ambacho

pia kinashughulikia jinsi ya kupata neema ya Mungu.

Kwa hiyo Dustin alipomwendea na wazo hilo la mkopo, Kendall hakufurahia hilo, alitumaini kwamba angemgeukia Mungu badala ya madeni. Aliamua kuzungumza naye kuhusu uamuzi wao na kumtia moyo amtumaini Mungu. Kwa neema, Dustin alipokea hekima ya mke wake.

Walipokuwa wakiomba, walimsikia Roho Mtakatifu akisema watoe matoleo kama mbegu. Bila shaka, wakati huo hawakuwa na kiasi cha pesa ambacho Mungu alikuwa akiwaonyesha watoe, kwa hiyo walifanya kazi kwa siku 28 zilizofuata ili kupata pesa za kutosha kupanda.

Matokeo? Biashara yao ilistawi.

Katika mwaka uliofuata, waliweza kulipa deni la $175,000, na Dustin alisema alipata pesa mara KUMI NA MBILI zaidi mwaka huo kuliko pesa zozote alizowahi kupata maisha yake yote!

Kendall na Dustin walipata kujua kwamba Ufalme unafanya kazi kila wakati!

Jibu lao lilikuwa nini? Ufalme na neema ya Mungu!

Jibu lako ni lipi? Ufalme na neema ya Mungu!

## SURA YA 2

# JIBU: NEEMA

Katika sura iliyopita, tulizungumza kuhusu jinsi ukarimu unavyogusa watu kiroho—jinsi unavyofanya mioyo yao kuwa miororo na kujawa na shukrani kwako na kwa Mungu. Pia tumeweka wazi kile Paulo alichosema, kwamba uwezo huu wa kuwa mkarimu ni matokeo ya neema ya Mungu katika maisha yetu.

> *Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!*
>
> — 2 Wakorintho 9:14-15

Tulizungumzia msisitizo Paulo alioweka juu ya neno *iliyozidi* wakati anaeleza kuhusu neema ya kufanikisha ambayo Mungu ametupa. Tuligundua kwamba neema ni uwezeshaji wa ajabu wa kukamilisha jambo fulani. Paulo anauita uwezeshaji huu wa neema ya Mungu kipawa kisichoweza kusifiwa kama ipasavyo! Nafikiri kila mtu anaweza kukubali kwamba ikiwa Mungu, Mwenyewe atawasaidia kufanikiwa maishani, hiyo ni faida kubwa sana.

Ili kukusaidia kufahamu ukubwa wa kile ambacho Mungu anataka kufanya katika maisha yako na uwezo mkubwa uliopo kwa ajili yako, hebu turudi nyuma kidogo na tusome kuanzia mstari wa sita.

> *Hili ndilo ninalomaanisha: Apandaye haba atavuna haba. Apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mmoja na atoe kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa kusita au kwa mkazo, kwa maana Mungu humpenda mtoaji mkunjufu. Mungu aweza kuwajaza neema*

*yote, ili katika mambo yote, siku zote, mkiwa na riziki za kila namna, mpate kujawa na matendo mema. Kama ilivyoandikwa: Alitawanya, akawapa maskini. Haki yake inadumu milele.*

*Naye ampaye mbegu mpandaji, na mkate kwa chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye ataongeza mavuno ya haki. Mtatajirishwa kwa kila namna ili mpate kuwa wakarimu kwa kila jambo, jambo linaloleta shukrani kwa Mungu kupitia kwetu.*

—2 Wakorintho 9:6-11 (Tafsiri ya 'EHV')

Sasa, hapa ndipo mambo yanasisimua sana!

Tunaona neno lile lile *neema* limetumika hapa, isipokuwa katika kifungu hiki Paulo anaongeza kivumishi yote ili kumsaidia msomaji kuelewa kwamba nguvu ZOTE za Mungu ziko nyuma ya neno hilo neema. Paulo anazungumza waziwazi kuhusu kutoa na kupokea hapa na anatoa hoja kwamba mara tu unapotoa, neema yote ya Mungu inapatikana kwako ili kuleta mavuno.

Neema yote ya Mungu inamaanisha kwamba nguvu zote, hekima, kibali, na ufahamu Wake sasa vinapatikana kwako ili kunyakua mavuno kutoka kwa mbegu hiyo. Sijui kukuhusu, lakini hilo hunipa msisimko!

Lakini hiyo bado haimaanishi kwamba mavuno yatatokea peke yake.

Ikiwa mkulima tajiri sana angekuambia kwamba atakukopesha vifaa vyake vyote vya kilimo, vyenye thamani ya mamilioni ya dola, ili uweze kupanda na kuvuna mazao, lakini hujui chochote kuhusu kilimo, haitakufaidi chochote.

Mungu amefanya nguvu Zake zote zipatikane kwetu, lakini bado tuna sehemu ya kufanya, kama jinsi mkulima anavyojua kuna mengi zaidi katika kilimo kuliko kupanda mbegu ardhini tu.

Kwa sasa, ninachotaka uelewe ni kwamba uwezo wote wa Mungu unasimama karibu sio tu kukusaidia kuvuna baada ya kupanda lakini pia hata kukusaidia kujua wakati na mahali pa kupanda. Na kwa sababu hiyo, una mustakabali usio na kikomo wa kifedha!!!!

**WEWE SHUGHULIKIA KAZI YA MUNGU, NAYE ATAISHUGHULIKIA YAKO.**

Sasa, tunahitaji kwenda hatua nyingine mbele na kuzungumzia ufunuo ulio wazi katika kifungu hiki kuhusu madhumuni ya kuwa na pesa kwanza.

*Mungu aweza kuwajaza neema yote, ili katika mambo yote, siku zote, mkiwa na riziki za kila namna, mpate kujawa na matendo mema.*

Tunaona jambo la kwanza alilotaja Mungu ni kuwa na riziki za kila namna. Tazama, haihusu pesa tu. Anasema katika mambo yote na siku *zote*!

Daima nasema hivi, "Wewe shughulikia kazi ya Mungu, Naye ataishughulikia yako." Kwa hiyo, "katika mambo yote na siku zote" inamaanisha kwangu kwamba hutawahi kuwa na ukosefu, haijalishi hali ya uchumi. Mungu anaposema mahitaji yako yatatimizwa, Yeye hamaanishi kuwa na riziki ya kutosha tu.

> *Nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya.*
>
> — Kumbukumbu la Torati 28:12b-13

Mungu anapozungumza kuhusu mahitaji yako yote kutimizwa, anamaanisha kuishi huru kikamilifu kifedha bila madeni, kutekeleza kazi yako kwa shauku, na kula mema ya nchi. Pia ni kuwa na afya na amani kamili.

Pili, baada ya mahitaji yako kutimizwa, unaanza kustawi sio kuishi tu,

*Mtatajirishwa kwa kila namna ili <u>mpate kuwa wakarimu kwa kila jambo</u>.*

Matokeo ya mwisho ni kuwa na uwezo wa kifedha wa kuwa mkarimu, kutoa na kuwa msaada kwa watu na kwa kazi ya Mungu duniani.

Kusudi la Mungu ni kuujulisha moyo Wake kwa watu na kuelekeza mioyo ya watu Kwake.

Kama ninavyosema kila mara, "Mungu yuko katika biashara ya watu."

Hebu nitumie muda mfupi kushughulikia dhana potofu ambayo mimi huisikia mara kwa mara.

Nilikuwa nikizungumza na mtu tajiri sana hivi majuzi, naye akasema, "Sihitaji pesa zaidi; ninazo tele."

Sasa, najua kile alichokuwa akijaribu kusema—kwamba anatunzwa vyema sana, na hahitaji pesa zaidi kibinafsi. Lakini ukweli ni kwamba anahitaji pesa zaidi na nyingi.

Ikiwa tutazingatia tu kile ambacho pesa zinaweza kutufanyia *kibinafsi*, basi nafikiri kuna mahali ambapo msukumo wa kupata pesa zaidi unaweza kupungua. Lakini ikiwa unaelewa moyo wa Mungu wa kufikia watu na

mamilioni ambao bado hawajagundua maisha mazuri yaliyoko katika Ufalme—wangali wanaelekea mahali halisi paitwapo kuzimu—basi utaelewa kwamba Mungu anahitaji pesa zaidi!!!!

Hebu nirudie tena, **"MUNGU ANAHITAJI PESA ZAIDI!"**

Bado kuna kazi nyingi ya kufanywa.

> *Mungu aweza kuwajaza neema yote, ili katika mambo yote, siku zote, mkiwa na riziki za kila namna, <u>mpate kujawa na matendo mema.</u>*

Una matendo mema ya kushughulikia. Matendo mema ni kazi unayofanya kwa niaba ya Mfalme. Hakika, una kazi maalum sana ya kufanya, kulingana na Waefeso 4:7, 11-12a.

> *Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa Chake Kristo. Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata <u>kazi ya huduma</u> itendeke.*
>
> — Waefeso 4:7, 11-12a

Wajua, watu wengi huwa na lengo la kuwa huru kifedha kwa sababu wamechoshwa na mbio za panya. Wanatafuta amani. Na kwa kuwa wengi hufanya kazi wasizopenda, wanatafuta uhuru unaoletwa na kuwa na pesa. Wanatafuta uhuru wa kufanya *wanachotaka* kufanya badala ya kile *wanachopaswa* kufanya. Wanataka kufuata shauku yao na kupata kusudi la maisha yao.

Hapa kuna kauli inayowatia wazimu watu wa dini:

*Mtatajirishwa kwa kila namna.*

Ndio, neno linasema hivyo. Utatajirishwa!

Sasa neno utajiri bila shaka ni la kibinafsi, na mara nyingi halieleweki vyema katika tamaduni zetu. Kwa kweli hatuwezi kusema kwamba mtu ambaye ana dola bilioni moja ana furaha zaidi kuliko mtu aliye na $100,000. La, kuwa "tajiri" kunamaanisha vitu tofauti kwa watu tofauti. Lakini, bila shaka, kunadokeza kwamba mahitaji yetu yote yametimizwa, kwamba tunaishi bila madeni, na kufurahia mema ya nchi.

*Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi.*

— Isaya 1:19

Lakini kuwa tajiri sio pesa tu. Pia kunahusu kucheza na wajukuu wangu, kushikana mikono na mke wangu, na mengine mengi ya ajabu maishani.

Mimi na Drenda tuna watoto watano wazuri, wote wanampenda Mungu na kwa njia moja au nyingine wanahusika katika huduma. Sote tunaishi karibu kila mmoja, na, kwa kweli kabisa, tunapenda kubarizi pamoja. Naita huo utajiri!

Wajua, watu wa dini hufikiri kwamba kuwa na pesa nyingi ni uchoyo. Lakini huwezi kuwa na pesa nyingi sana ikiwa uko katika biashara ya watu na Mungu. Daima kuna kazi mpya na maeneo mapya ya kuchukua.

**KWA HIVYO TENA, MUNGU ANATAKA UWE NA RIZIKI NYINGI ILI KUENDELEZA KAZI YAKE ULIMWENGUNI.**

Kwa hivyo tena, Mungu anataka uwe na riziki nyingi ili kuendeleza kazi Yake ulimwenguni.

Mungu anataka uwe mkarimu kwa niaba Yake, kuwasaidia watu, na kufadhili kazi Zake. Lazima uwe na pesa ikiwa unatakiwa kuwa mkarimu kila wakati.

Kila wakati inaweza kuwa *kila siku au mara kadhaa kwa siku*. Hebu tuseme ukweli—ili kuweza kufanya hivyo, hupaswi kuishi mwezi hadi mwezi; unapaswa kuwa na pesa zaidi ya zile zinazohitajika kulipa bili zako, nyingi zaidi! Nafikiri kila mtu atakubaliana na hilo.

Lakini hebu sasa tuzingatie kwa umakini maana ya kuwa mkarimu au kutoa kwa ujumla:

Unapaswa kukabiliana na hofu unapotoa.

Sikusema lazima *uvumilie* hofu. Nimesema lazima UKABILIANE na hofu unapotoa. Na njia bora ya kukabiliana na hofu ni ukweli!

Kwa hivyo kuna hofu gani katika kutoa? Kifupi, ni kwamba hatutakuwa na pesa za kututosha sisi wenyewe, sivyo?

*Ninahitaji pesa hizo,* unaweza kufikiria, na bila shaka unazihitaji. Lakini Mungu anazihitaji pia. Na Mungu hatakuomba umpatie pesa zako ili azitumie bila ahadi ya kukurudishia, marejesho ya uwekezaji wako, sivyo? Nafikiri Mungu yuko wazi katika Neno Lake:

*Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa,*

*na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu.*

— Luka 6:38a

Mungu hutumia muda mwingi kukueleza faida ya kutegemeza Ufalme Wake kuliko anavyotumia kukuelekeza la kufanya. Anasema neno moja tu, *"Toa,"* lakini anatumia maneno 23 kukueleza *manufaa* yake kwako. Nafikiri ningependa kutia saini mkataba wowote wa namna hiyo!

Fahamu Mungu ana nia kwamba ufaulu maishani. Tafakari juu yake: Mungu atapata wapi pesa anazohitaji ili kufadhili ajenda Yake?

Bila shaka pesa hizo itabidi zitoke kwako, mimi, na waamini wenzetu wengine. Watu wa Shetani hawawezi kufadhili kazi ya Mungu.

Jambo la kusikitisha ni kwamba waumini wengi husema ni makosa kumwamini Mungu kuwarudishia wanapotoa. Wanaamini kumtolea Mungu na kutarajia kurudishiwa chochote kuna msingi wa uchoyo na kunadhoofisha tendo safi la kumwabudu Mungu.

Je, unaamini mkulima hukosea anapoamini kwamba kutoa kwake kutaleta faida kwake na familia yake? Yeye hutumia tu sheria alizopewa na Mungu.

Mungu hufurahi anapoona tukisitawi. Alitupa sheria ya kupanda na kuvuna kwa faida yetu. Ibilisi amelidanganya kanisa kuhusu utoaji na pesa tangu mwanzo wa nyakati. Baadhi ya madhehebu hujivunia viapo vyao vya umaskini, bila kutambua kwamba wanaanguka moja kwa moja katika uongo wa Shetani. Ilimbidi Yesu kukabiliana na mtazamo huo mara nyingi katika huduma Yake. Alisimulia moja ya mifano Yake maarufu kuhusu suala hili hili, mfano wa Msamaria Mwema.

*Na tazama, mwana-sheria mmoja alisimama amjaribu; akisema, "Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?"*

*Akamwambia, "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?"*

*Akajibu akasema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako."*

*Akamwambia, "Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi."*

*Naye akitaka kujidai haki, alimwuliza Yesu, "Na jirani yangu ni nani?"*

*Yesu akajibu akasema, "Mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo,*

*wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona, akapita kando. Lakini, Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; na alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema, 'Mtunze huyu, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa.'"*

*Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?*

*Akasema, "Ni huyo aliyemwonea huruma."*

*Yesu akamwambia, "Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo."*

— Luka 10:25-37

Nafikiri sisi sote tumesikia hadithi hii somo likiwa: Mungu angefanya nini kama angekuwa anatembea barabarani na kumwona mtu huyo? Tunajua Bwana asingemwacha afe kando ya barabara.

Somo ambalo makanisa mengi katika mafundisho ya Jumapili asubuhi hufunza kuhusu hili ni kwamba tuwe majirani wema. Tutunze wengine. Kutunza wengine ni moyo wa Mungu, na naweza kusema nakubaliana asilimia mia moja na tathmini hiyo. Walakini, kuna mengi zaidi ambayo mara nyingi husahaulika.

Ili kuelewa kweli karipio la Yesu kwa mtaalamu huyu wa sheria, unahitaji kuelewa hali ya kijamii ya wakati huo. Wayahudi waliwadharau Wasamaria na kuwaona kuwa watu wasio safi na wasio wa kiroho. Kwa hiyo, Wayahudi walijiona kuwa watakatifu na waadilifu zaidi machoni pa Mungu kuliko Wasamaria kiasi kwamba hawakutaka kushirikiana nao. Kwa hiyo hadithi ya Yesu kimsingi ni kofi usoni kwa mtaalamu huyu wa sheria, kemeo kwa mtazamo wake kuhusu kumcha Mungu. Nafikiri sote tunaelewa hili.

Lakini sehemu ambayo sijawahi kusikia hata kidogo ikifundishwa katika mafundisho yoyote ya Jumapili asubuhi, ni sehemu kuhusu hadithi ya sarafu mbili za fedha. Kwa nini Yesu alizungumzia sarafu mbili za fedha ikiwa wazo Lake lilikuwa tayari limetolewa juu ya moyo mbaya wa mtaalamu huyu kuhusu Wasamaria? Hebu tujue.

*Akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba*

*ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema, "Mtunze huyu, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa."*

— Luka 10:34a-35

Katika hadithi hii ni dhahiri kwamba huu ulikuwa mlinganisho wa kile ambacho Yesu alikuwa akitaka kutufanyia. Tunaona jinsi wanadamu wanavyopigwa na kupondwa na Shetani, mwizi. Tunaelewa mafuta na divai vinawakilisha kinabii Roho Mtakatifu na agano la damu ambalo Yesu huwapa wote wanaokuja Kwake. Pia tunaona kwamba, baada ya kumpaka mafuta na divai, Msamaria alifanya zaidi kwa kumpeleka mtu huyo aliyejeruhiwa kwenye nyumba ya wageni ili apone. Msamaria huyo alifahamu kwamba mtu huyo alihitaji wakati ili apone, na akampeleka mahali salama, yote kwa gharama yake.

Ninaamini nyumba ya wageni inawakilisha kanisa la mtaa. Hapa ndipo Yesu huwaleta watu waliopigwa na kuachwa kufa katika safari hii ya maisha. Wanazaliwa mara ya pili, wanatakaswa kutoka kwa dhambi kwa agano la damu na kufanywa hai na Roho Mtakatifu, lakini bado wana madoa na maumivu ya mfumo wa laana ya dunia. Wanahitaji muda wa kupona na kujifunza njia mpya kabisa ya kuishi. Yesu anawaweka katika kanisa la mtaa na chini ya mlinzi wa nyumba ya wageni, mchungaji wa mahali hapo, ili kusimamia maendeleo yao.

Lakini cha kusikitisha ni kwamba, tunapata mtazamo huuhuu wa mwalimu wa sheria katika kanisa. Watu hawataki kutoa ili kusaidia kazi iliyo katika nyumba ya wageni. Kama wale waliompita yule mtu aliyejeruhiwa, wao huona kwamba hilo ni tatizo la mtu mwingine. Kwa nini wajihusishe? Ni faida gani iliyopo kwao isipokuwa kuwagharimu wakati na pesa?

Kwa sababu ya mtazamo huu, wachungaji hutumia wakati wao mwingi kuwasihi washirika wa kanisa wasaidie kwenye kitalu au kuongoza kikundi kidogo. Lakini inaonekana watu tayari wana shughuli zao wenyewe na wanaona ni vigumu kujitolea. Dini yenyewe haina motisha, bali wajibu na sheria tu. Dini hujaribu kuwatia hatia watu kusaidia kwa kusema, "Unawiwa na Mungu kutunza hili au lile. Tazama yale Mungu amekufanyia." Na ninakubali, tunapaswa kuwa na mioyo iliyo tayari na inayotoa shukrani kwa Mungu, na kuwa na hamu ya kusaidia wengine, lakini Mungu hatumii mfumo wa "kudai" kutoka kwa watu anapofanya kazi. Anasema, "Ninakuachia sarafu mbili za kulipia gharama na nitakulipa gharama YOYOTE nyingine nitakaporudi."

Tena, mawazo ya kidini husema kauli hii inamaanisha kwamba tutakapofika mbinguni, Yesu atatupa thawabu kwa kazi tuliyoifanya hapa duniani kwa ajili ya Ufalme Wake. La, Yesu alipokuwa akisimulia hadithi hiyo, alikuwa akimaanisha wakati ambapo mfanyabiashara huyo angepitia pale alipokuwa akirudi mjini. Yesu alikuwa akizungumzia msaada wa kifedha wa wakati halisi kwa yule mtunza nyumba ya wageni. Lakini watu wanaweza kusema, "Vema, Mungu atalipia gharama za nyumba ya wageni, nami nitalipia gharama halisi hapa nyumbani kwangu. Sina wakati wa kuhusika wala pesa za kutoa." Mtazamo huu wa kufidiwa tu kwa gharama yoyote waliyoitumia kujihusisha hauwachochei watu wengi. Bila shaka unawasaidia lakini haufunui hadithi nzima ya upendo wa Mungu kwa wale wanaojihusisha.

Ndio, najua utakachosema: "Sote tunapaswa kusaidia katika nyumba ya wageni kwa sababu tunampenda Mungu tu." Ndio, unaweza kufanya hivyo kwa sababu ya uaminifu wako kwa mchungaji wako na upendo na wajibu wako kwa Mungu, na hilo linahitajika wakati mwingine… Lakini Mungu anataka uwe na *shauku* ya "kufanya kazi katika nyumba ya wageni" pamoja Naye.

Na hiyo ndiyo hoja—hatumfanyii Mungu kazi bali tunafanya PAMOJA naye. Mungu, Mwenyewe anasema yafuatayo kupitia kwa Paulo:

> *Ni askari gani aendaye vitani wakati wowote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi? Je! Ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo? Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, "Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka." Je! Hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe? Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake.*
>
> — 1 Wakorintho 9:7-10

Mungu hataki umtumikie kwa sababu ya woga au wajibu tu.

Tazama alisema, *"Alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake."* Mungu hajali tu mavuno ambayo ni matokeo ya kazi aliyokupa. Yeye pia huwajali wale wanaofanya kazi pale pale pamoja Naye, na anataka washiriki shangwe ya mavuno kama Yeye afanyavyo.

Yesu alichagua kutumia mfano wa mtunza nyumba wa wageni katika hadithi hiyo kwa sababu muhimu sana. Tunaelewa kwamba mwenye nyumba ya wageni ni mfanyi-biashara. Ameingiza katika bei ya kila siku malipo ya wafanyikazi. Lakini juu ya gharama zote za kuendesha nyumba ya wageni, yeye huongeza faida. Hiyo ni kweli, *faida*.

Kila wakati mwenye nyumba ya wageni anapomtoza mgeni wake kwa ajili ya kukaa usiku, yeye hupata faida. Kwa sababu hiyo, mlinzi wa nyumba ya wageni ana mtazamo tofauti sana kuhusu mtu yeyote mwenye majeraha anayeletwa kwake. Haimgharimu chochote kumtunza, kwani msafiri ameahidi kulipia gharama zake. Lakini mwenye nyumba ya wageni anajua ukweli unaomfanya kumsaidia mtu huyu bila kinyongo. Kwa kweli, ana msisimko mwingi kuhusu fursa aliyo nayo.

Wajua, mlinzi wa nyumba ya wageni anaelewa kwamba kila usiku mtu huyo anakaa huko, atapata faida, na maana mfanyabiashara amemruhusu kuwa huru kumtunza yule aliyejeruhiwa, basi ana furaha. Naweza kuwazia tu mazungumzo ya mwenye nyumba ya wageni pamoja na mfanyabiashara msafiri anapoondoka katika safari yake: "Haya, ukiona mtu mwingine yeyote anayehitaji msaada kando ya barabara, hakikisha umemleta hapa. Nitachukua wote unaoweza kuniletea, na nikikosa mahali, nitapanua nafasi!"

Kama unavyoona katika hadithi hii, kuna mengi zaidi kuliko tu hadithi inayojulikana kuhusu kile ambacho Yesu angefanya. Yesu alikuwa anasahihisha mtazamo wa kidini ambao yule mtaalamu wa sheria alikuwa nao kumhusu Mungu na Msamaria. Pia alikuwa akimsisitizia kwamba alikuwa anakosa fursa kubwa sana ambayo Msamaria alikuwa amenyakua—faida!

Kila wakati mimi huhuzunika ninaposikia watu wakisema kwamba Mungu huwafanyia watu wema mambo mabaya, au ninapoona watu wakimtumikia Mungu kwa sababu ya wajibu wao wa kidini badala ya kuwa na maisha ya furaha ambayo wangeweza kuwa nayo. Shetani amejaribu kuficha wema wa Mungu kutoka kwa watu wa Mungu ili wasimtumikie kwa hiari na mioyo yao yote.

**CHA KUHUZUNISHA NI KWAMBA HAWAUELEWI MOYO WA MUNGU, KWAMBA YUKO TAYARI KULIPA GHARAMA YOYOTE ILI KUWAFIKIA WATU, NA YEYE WAKATI WOTE HUTUPATIA ZAIDI YA KILE TUNACHOWEKEZA. KILA MARA.**

Kwa watu wengi, kanisa ni jambo lingine tu kwenye kalenda zao wala hawaelewi kwamba wao

ndio kanisa, yaani nyumba ya wageni ambapo Mungu huwatuma watu kuwa wakamilifu. Cha kuhuzunisha ni kwamba hawauelewi moyo wa Mungu, kwamba yuko tayari kulipa gharama yoyote ili kuwafikia watu, na Yeye wakati wote hutupatia zaidi ya kile tunachowekeza. Kila mara.

Ninakumbuka tulizungumza kuhusu jambo hili hili pamoja na kaka ya Drenda miaka mingi iliyopita—kwamba Mungu ni mwema na ni mtuzaji, na ametupa Ufalme unaotosheleza mahitaji yetu yote. Ukweli huu kuhusu Ufalme ulikuwa jambo geni kwa Johnny na mke wake, Candi, kwa kuwa walikuwa wametoka katika kanisa la kitamaduni ambako hawakufundishwa ukweli wote.

Johnny na Candi walikuwa walimu kule Georgia, na wakati huo huo Johnny alikuwa akifanya kazi ya muda kwa kampuni yangu ya kifedha, Forward Financial Group. Ilionekana kwamba Johnny alikuwa mtu wa asili katika biashara. Katika mwaka wake wa kwanza katika kampuni, alipata mapato zaidi kwa mwaka kuliko yale aliyoyapata alipokuwa mwalimu, kwa hivyo aliamua kuacha kufundisha na kuanza kufanya biashara ya fedha pekee.

Mwanzoni, Johnny alifanya biashara vizuri sana. Lakini baadaye katika mwaka huo, niliona kwamba shughuli yake ilianza kupungua, na nilijua kwamba hangeweza kuendelea kwa mwendo huo kwa muda mrefu.

Mimi na Drenda tulikuwa tumepanga safari ya kwenda Georgia katika msimu wa Krismasi, na ilikuwa nia yangu kabisa kuwa na wakati pamoja na Johnny ili kuona kama ningeweza kutambua baadhi ya sababu za kutozalisha pesa ambazo angehitaji ili kuweza kuendelea na biashara. Kabla ya kumpigia simu, Johnny alinipigia simu na kuniuliza ikiwa ningepitia kumwona ili tuzungumzie biashara. Bila shaka, nilikuwa tayari kufanya hivyo.

Niliweza kuona kwamba Johnny na Candi walikuwa na hofu. Tayari walikuwa na bili za mwezi huo za thamani ya $5,000, na hawakutarajia $5,000 katika mwezi uliokuwa ukifuata. Nilipoketi na Johnny, maneno yake ya kwanza yalikuwa, “Haifanyi kazi.” Nilijua kwamba ufahamu kuhusu Ufalme ulikuwa jambo jipya kwa Johnny na Candi, na nilihisi kwamba nilihitaji kuwazoeza jinsi ya kushughulikia hilo kiroho. Kwa sababu nilifahamu kwamba Ufalme hufanya kazi kila wakati! Kwa hiyo nilitumia karibu masaa mawili pamoja nao nikiwafundisha sheria za Ufalme na jinsi ya kuachilia imani yao. Nilipokuwa nikizungumza, nilihisi hofu ikififia na imani ikianza kuongezeka. Nilijua Johnny alikuwa tayari kuchukua hatua iliyofuata.

“Johnny,” nikasema, “Unahitaji kutoa matoleo kama mbegu na

kumwamini Mungu kupata pesa unazohitaji."

Johnny na Candi walikubali, lakini hawakuwa na pesa. Ilifanyika tu kwamba nilikuwa nimekuja na malipo ya Johnny ya $160 kutoka ofisi yetu kuu. Nilijua walihitaji pesa hizo, lakini niliwahimiza badala ya kuzitumia wazitoe kama mbegu maana sote wawili tulijua kwamba dola 160, peke yake, hazingeweza kulipa bili za $5,000 walizokuwa nazo au bili za $5,000 zilizokuwa zikija. Walikubali.

Tulipokuwa karibu kuomba na kuachilia imani yetu pamoja, nilimuuliza Johnny, "Unaamini kupokea nini unapopanda pesa hizi?" Maneno yale yalipotoka kinywani mwangu, Roho Mtakatifu aliniambia nimzuie asiniambie, na nilijua kwa nini. Johnny angesema aliamini kupata $5,000, kwa sababu ni wazi, hapo ndipo shinikizo lilikuwa. Badala yake, Roho Mtakatifu aliniambia, "Muulize ikiwa $12,000 kwa siku 30 zitatosha."

Kwa hiyo, nilifanya hivyo tu. Nilimzuia asijibu na kumuuliza ikiwa $12,000 kwa siku 30 zitatosha. Niliona macho yake yamefunguliwa wazi nilipotamka kiasi ambacho Bwana aliniambia nimuulize. Nilijua kwamba Johnny hakuwa amewahi kupata $12,000 ndani ya siku 30 katika maisha yake yote. Alikaa pale kwa dakika moja kisha akasema, ndio, angeweza kuamini hivyo pamoja na mimi. Nilimuuliza Candi swali lile lile, naye akajibu ndio pia. Tuliunganisha mikono, tukaiweka kwenye hundi hiyo, na kuachilia imani yetu kwa dola 12,000 ndani ya siku 30.

Baada ya majuma matatu, nilipokea simu kutoka kwa Johnny. Jamani, alikuwa na furaha. Alikuwa amefanya biashara ya kutosha katika wiki hizo tatu ambayo ingemlipa sio tu $12,000 bali $17,000. Alisema sasa alikuwa amefanyika muumini wa kweli.

Kwa bahati mbaya, baada ya miezi miwili, Johnny alipokuwa akielekea nyumbani usiku mmoja katika mvua nyingi, baada ya kukutana na mteja, alikuwa na ajali ya gari. Gari liliharibika kabisa, lakini Johnny alinusurika, jambo ambalo lilikuwa muujiza wa Mungu. Hata hivyo, kutokana na ajali hiyo, Johnny hakuweza kufanya kazi kwa sababu bado alikuwa anapata nafuu. Katika kipindi hicho, nyumba yake ilikuwa karibu kuuzwa na Afisa Mkuu Mtendaji wa Utekelezaji wa Sheria wa kaunti yao. Alihitaji $10,000 ili kuokoa nyumba isiuzwe.

Hata hivyo, wakati huo Johnny na Candi walikuwa wameamua kuhamia Ohio ili kupata mafundisho zaidi kuhusu Ufalme ambayo yalikuwa yakibadili maisha yao. Kwa hiyo, waliweka nyumba yao kwenye orodha ya nyumba zilizokuwa zikiuzwa, ingawa walijua walikuwa na mwezi mmoja tu kabla ya yule Afisa Mkuu kuja kuiuza.

Kadiri tarehe ilivyokuwa inakaribia, hakuna wanunuzi halisi waliokuja hadi siku chache tu kabla ya Afisa Mkuu kuiuza wakati mtu mmoja alipitia kwao na kujitolea kununua nyumba hiyo. Lakini alikuwa na ombi. Alitaka kujua kama angempa Johnny $10,000 saa hiyo, ili asiuze nyumba hiyo kwa siku 30 hadi amalize biashara nyingine ambayo ingefadhili ununuzi huo.

Johnny alishtuka. Alijua kwamba ikiwa angeitoa nyumba hiyo kutoka kwa orodha ya mauzo ya Afisa Mkuu, ilibidi awe na mnunuzi ambaye angempa pesa taslimu maana siku ya mauzo ilikuwa inakaribia. Mnunuzi huyo alitaka kumwandikia Johnny hundi ya $10,000 papo hapo kisha amalize baadaye. Hiki ndicho kiasi halisi cha pesa ambazo Johnny alihitaji. Johnny alijua ni Mungu, alichukua hundi hiyo ya $10,000, na kulipa malipo yaliyohitajika hadi wakati huo. Ajabu! Na hizo $10,000 hazikuwa sehemu ya malipo ya nyumba bali *juu ya* bei waliyoinukuu.

Kwa hiyo Johnny na Candi walihamia Ohio na kuishi katika nyumba ya kukodisha. Walijihusisha na Kanisa la Faith Life, na Johnny akarudi kwenye biashara ya fedha kwa nguvu mpya. Lakini sasa walikuwa na tatizo jipya. Walikuwa na gari moja tu, na Johnny alilihitaji ili kugharamia miadi mingi aliyokuwa nayo wakati wa juma alipokutana na wateja. Naam, walijua la kufanya. Walipanda mbegu kwa ajili ya gari jipya na wakaamini walilipokea walipoomba, kulingana na Marko 11:24.

Kisha jambo lisilo la kawaida likatokea. Rafiki wa utotoni wa Johnny alimpigia simu…

"Johnny, niliwahi kukulipa wakati ulinipa ile baiskeli tulipokuwa katika darasa la sita?" Akauliza.

"La," Johnny akasema.

Kisha rafiki yake akasema, "Sawa, nitakulipa sasa. Nitakununulia gari aina ya BMW."

Walipokuwa watoto, walizungumza kila mara kuhusu magari, na alijua kwamba Johnny alikuwa akitaka BMW. Rafiki huyo alikuwa mwaminifu kwa neno lake na alimtumia Johnny pesa za kujinunulia BMW. Lakini mara tu Johnny alipopata pesa hizo, alitambua kwamba kwa sababu familia yake ilikuwa ikikua, hakuhitaji gari aina ya BMW. Yeye na Candi waliamua kumnunulia Candi gari kubwa la familia na dogo la Johnny la kuendesha biashara maana gari dogo la Candi walilokuwa nalo lilikuwa kuukuu na lilikuwa na matatizo. Hivyo ndivyo ilivyotokea.

Nakumbuka usiku ambao Johnny alinipigia simu. Alikuwa amekaa ndani ya gari lake jipya aina ya SUV katika kibarabara cha nyumbani kwake kando ya gari lake lingine jipya huku akitokwa na machozi na kuniambia

alikuwa ameshtuka kwa sababu hii ilikuwa mara yake ya kwanza maishani kuwa na magari mawili bila madeni.

Johnny alikuwa amefanyika mtu mpya. Alijua basi kwamba Mungu anaweza kufanya lolote.

Siku moja alikuja ofisini kwangu na kusema alikuwa amechoka kukodisha nyumba, kwamba yeye na Candi walitaka mali yenye shamba na walikuwa wakitafuta. Kweli nilijua kwamba mkopo kwa Johnny haukuwa sawa kwa sababu ya ile ajali aliyokuwa nayo na nikamtia moyo akodishe kwa muda zaidi ili aweze kujenga akiba yake ya pesa, na pia kuwa na muda wa kutosha wa kuongeza alama zake za mkopo. Lakini Johnny hakuonekana kutilia maanani sana nilichosema.

Kisha akaniambia kwamba alikuwa ameona shamba mbele kidogo kutoka kwangu ambalo lilikuwa linauzwa, na alikuwa anaenda kuliangalia ili kulinunua. Bila shaka, kwa kuwa nilikuwa na kampuni ya rehani wakati huo, nilijua hangeweza kumudu shamba hilo. Nilijua pia hakuwa na malipo ya kwanza yanayolipwa mtu anaponunua shamba.

Nilishtuka aliporudi ofisini mwangu baada ya juma moja akiwa na tabasamu na kusema kwamba shamba ni lake. Aliponiambia hivyo, nilijua lazima nisikie hadithi hiyo. Bila shaka, yeye na Candi walikuwa wamepanda mbegu ya kifedha katika kazi ya Mungu kama walivyofundishwa kuamini kwamba walikuwa wamepokea walipoomba. Kisha Johnny akanieleza kilichotokea.

Alikwenda kwa benki yake kuhusu ununuzi huo, na meneja akatoa ripoti yake ya mkopo na kuketi naye na kumwambia, "Johnny, ulikuwa sahihi kuhusu mkopo wako. Huna uwezo wa kununua chochote."

Lakini meneja alisema jambo la kushangaza. Alisukuma faili ya mkopo pembeni na kusema, "Lakini nakupenda. Ngoja nione ninachoweza kufanya."

Ili kufipisha hadithi ndefu, benki ilifadhili 100% ya ununuzi, ikampa miezi minne hadi upangishaji aliokuwa nao wakati huo uishe, walilipia gesi ya kupikia, wakalipa ushuru wa mali hiyo uliosalia, na baada ya kila kitu wakampa Johnny hundi ya $5,000 ili kurekebisha ufa katika saruji ya ukumbi wa mbele.

Niliketi pale nikiwa nimeduwaa huku Johnny akiendelea na kuendelea kuhusu Ufalme. "Ajabu!" ndicho tu ningechoweza kusema.

Baada ya mwezi mmoja, Johnny aliniambia alikuwa amepanda mbegu ya trekta aina ya Ford. Aliniambia alihitaji trekta kwenye shamba lake jipya na alikuwa amepanda mbegu maalum kwa ajili ya trekta ya dizeli aina ya

Ford, yenye rangi ya samawati. Tena, kwa vile alikuwa mfanyikazi wangu, na nilijua bei ya matrekta, nilifahamu kwamba bado hakuwa na kiasi hicho cha pesa.

Lakini kwa hakika, baada ya majuma machache nilipotazama kuelekea barabarani, nilimwona Johnny akiendesha trekta ya dizeli aina ya Ford ya bluu kuelekea nyumbani kwake. Nilipomuuliza aliipata wapi na kwa jinsi gani, alisema mwanamke mmoja alimfuata kanisani na kumuuliza ikiwa alijua mtu yeyote ambaye angehitaji trekta. Walikuwa wakifilisi shamba la wazazi wake, na kulikuwa na trekta waliyokuwa wakitaka kuondoa. Johnny alimwambia alikuwa na haja nayo.

Alimwambia asiwe na wasiwasi juu ya kumlipa, kwamba alipe alipoweza; hakuwa na haraka. Hivyo basi alipata trekta yake.

Mafanikio yake yaliendelea. Mwezi uliofuata, mapato ya biashara yake yalikuwa dola 72,000 kwa mwezi mmoja tu. Unapomuuliza Johnny jinsi hilo lilivyotukia, yeye husema lilitukia kwa kuwa mkarimu kwa Mungu na kuelewa sheria za Ufalme.

Hadithi iliyoje! Ningali ninakumbuka nilipoketi pamoja na Johnny na Candi katika nyumba yao kule Georgia usiku ule tuliposhiriki nao kuhusu Ufalme. Walikuwa wamelemewa na bili ya $5,000 na msimu wa Krismasi ulikuwa unakaribia, na bili nyingine ya $5,000 ya mwezi uliofuata ilikuwa ikija wala hawakuwa na chochote. Nafikiri una hamu ya kusikia kile nilichowaambia usiku huo.

Nilifahamu kwamba nilipaswa kuwasaidia kumwona Mungu katika giza la hali zilizowakabili. Nilianza kwa kuwaonyesha kile ambacho tumekuwa tukizungumzia katika 2 Wakorintho 9:10-11:

> *Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*

Nimetaja kwamba Paulo alikuwa akisema kwamba Mungu hatakupa mbegu unayopanda tu bali pia kwamba atatoa mkate kwa mahitaji yako mwenyewe. Mkate unarejelea kila kitu unachohitaji kibinafsi katika maisha yako. Kutokana na hilo, Mungu ataongeza uwezo wako wa kutoa hata zaidi. Hiyo ina maana kwamba utazidisha.

Tena, hofu katika kutoa ni nini? Kwamba hutakuwa na pesa za kutosha kulipia mahitaji yako mwenyewe.

Lakini zingatia yale ambayo Mungu anasema. Anampa mpanzi mbegu na mkate kwa chakula. Sasa, hapa kuna swali muhimu sana, na hili ndilo swali nililomuuliza Johnny.

**Je, ulicho nacho mkononi mwako ni mbegu au ni chakula? Ni chaguo lako.**

Baba ya mamangu, babu yangu, alikuwa mkulima maisha yake yote. Nakumbuka nilipokuwa mvulana mdogo nilikuwa nikicheza kwenye gari lake la mbegu. Huenda hujawahi kusikia kuhusu gari la mbegu. Labda hata kwa kawaida hakuna kitu kama hicho lakini kwa babu yetu kilikuwepo. Kila mwaka wakati wa mavuno, Babu alihifadhi mbegu za kutosha kujaza gari alilokuwa nalo ghalani. Gari hilo lilikuwa limejaa mbegu alizokuwa akihifadhi ili kupanda katika majira ya kuchipua kwa ajili ya mazao ya mwaka uliofuata.

Wakati wa miezi ya majira ya baridi kali, ilimbidi Babu alitazame lile gari kubwa lililojaa maharagwe ya soya, akijua kwamba alikuwa na chaguo la kuyauza ili kulipia mahitaji au kuyahifadhi ili kuyapanda katika majira ya kuchipua ambako alijua angepata mavuno mengi. Alikuwa na chaguo, lakini alisadiki sheria za wakati wa mbegu na mavuno, na aliziamini kabisa.

Iliwabidi Johnny na Candi wakabiliane na uamuzi huu huu nilipowapa ile hundi ya $160. Bila shaka wangeitumia kulipia hitaji kubwa, lakini badala yake, walifahamu kwamba ukarimu kwa Mungu huleta mavuno makubwa zaidi mwishowe. Na walikuwa sahihi.

> *Kuna atawanyaye, lakini huongezewa zaidi; kuna azuiaye isivyo haki, lakini huelekea uhitaji.*
>
> — Mithali 11:24

Kabla ya kumaliza sura hii, kuna mfano mmoja zaidi ambao ningependa kuutazama—Mathayo 25:14-30, mfano wa talanta.

> *Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda, akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini, akaificha fedha ya bwana wake.*
>
> *Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale, akafanya*

*hesabu nao. Akaja yule aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema, "Bwana, uliweka kwangu talanta tano; tazama, talanta nyingine tano nilizopata faida."*

*Bwana wake akamwambia, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako." Akaja na yule aliyepokea talanta mbili, akasema, "Bwana, uliweka kwangu talanta mbili; tazama, talanta nyingine mbili nilizopata faida."*

*Bwana wake akamwambia, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako." Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema, "Bwana, nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama, unayo iliyo yako."*

*Bwana wake akajibu, akamwambia, "Wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi, ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoao riba; nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake.*

*Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."*

— Mathayo 25:14-30

Hadithi hii inajulikana. Bwana aliondoka mjini na kuwaacha watumishi wake watatu wawe wasimamizi. Alimpa mmoja mifuko mitano ya dhahabu, mwingine mifuko miwili ya dhahabu, na mwingine mfuko mmoja wa dhahabu.

Wawili wa kwanza walienda kufanya kazi mara moja na wakazidisha mifuko ya dhahabu mara mbili. Bwana aliwapongeza kwa kazi yao. Lakini nataka tutazame mtumishi wa tatu. Alipewa mfuko mmoja wa dhahabu lakini hakufanya chochote. Kwa kweli, aliuzika mpaka bwana wake akarudi.

*Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema, "Bwana, nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama, unayo iliyo yako."*

Sikiliza kwa makini sentensi ya kwanza: *"Bwana, nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya."*

Alikuwa akisema nini? Nitakwambia kile alichosema hasa. Alisema, "Kwa nini nijihusishe? Ikiwa unavuna mahali ambapo hukupanda, basi ni nani aliyelipia mbegu na ni nani aliyeitawanya na kufanya kazi yote ya kuikuza?"

Sasa, tunaelewa kwamba bwana huyo alimpa pesa za kununua mbegu, lakini mtazamo wake ulikuwa kwamba haikufaa wakati wake kujihusisha. Hakuwa na faida yoyote katika hilo. Faida yote, matokeo ya kazi yake, ingeenda kwa bwana wake. Kwa sababu ya taswira yake kuhusu bwana wake, kwamba alikuwa mgumu, kimsingi alikataa kujihusisha. Alijaribu kuficha ukweli kwamba alimdharau bwana wake kwa kusema nia yake ya kuficha pesa ni kwa sababu aliogopa kuzipoteza, na hivyo kuficha dhahabu ili kuilinda. Lakini bwana huyo alitambua uwongo wake na kusema kwamba ikiwa kweli alimjali, angeweka pesa hizo kwenye amana kwenye benki, na hapo, zingepata faida.

La, mtumishi huyo hakuogopa kupoteza dhahabu; alihofia gharama ya kujihusisha. Alikuwa na taswira potovu na mbaya kumhusu bwana wake, potovu kwa sababu kinyume chake ndicho kilichokuwa ukweli. Yule bwana hakuwa mgumu. Wale watumishi wengine wawili walithawabishwa kwa kupandishwa vyeo na kualikwa kufurahia mali ya bwana baada ya kufanya kazi kwa mafanikio na pesa za bwana. Mtumishi huyu, kwa sababu ya taswira yake mbaya kumhusu bwana wake, alichagua kutoshiriki. Na hivi ndivyo hasa dini inavyotufundisha—kwamba Mungu ni mgumu na hakuna faida katika kufanya kazi Naye, kwa hivyo kwa nini kujihusisha?

Lakini taswira hiyo kumhusu Mungu ni potovu kabisa na si kweli. Kusema Mungu hana haki ni uovu. Mungu ni kinyume kabisa na taswira hiyo.

Yeye ni mwema na ni mtuzaji.

Lakini sasa nataka kusisitiza jambo muhimu sana ambalo limetolewa katika hadithi hii. Sikiliza kwa makini kile bwana alichofanyia dhahabu aliyoichukua kutoka kwa mtumishi mwovu.

> *Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."*

Je, nilisoma hilo vyema? Bwana alichukua mfuko wa dhahabu kutoka kwa mtumishi asiyefaa na kumpa yule aliyekuwa na kumi wala si yule aliyekuwa na nne? Sina hakika kwamba kufanya hivyo ni sahihi kisiasa, lakini ndivyo alivyofanya. **SIKILIZA KWA MAKINI!!!!**

Mungu hutoa mawazo na kazi Zake kuu kwa watoto Wake ambao wana faida Yake akilini na wale waliojithibitisha kuwa waaminifu katika kazi ndogo kwanza.

Mungu si mjinga. Yeye huweka pesa Zake mahali ambapo zitapata faida kubwa zaidi.

Tafadhali tafakari kile ambacho nimesema—Mungu huweka pesa Zake mahali ambapo zitapata faida kubwa zaidi!

Sasa, bila shaka, Mungu hafanyi biashara ya *pesa*, bali anafanya biashara ya *watu*. Na tunapokuwa waaminifu kufanya kazi Naye kwa bidii, atatukuza na kutupa kibali katika mambo Yake mema.

Ndio, Mungu ana wale anaopendelea inapohusu wale anaowaamini kutekeleza kazi mbalimbali. Wale ambao wamethibitika kuwa waaminifu huaminiwa na Mungu kushughulikia kazi Zake kubwa na zenye thawabu kubwa zaidi.

Angalia mtazamo wa wale watumishi wawili waliofaulu—walienda mara moja na kutumia pesa za bwana wao! Kwa nini mara moja? Kwa sababu walijua hii ilikuwa *fursa*, si uzito wa utumwa.

Watu wengi wa Mungu huona kumtumikia Mungu kama jambo la kuchosha, wajibu unaopaswa kutimizwa.

**MUNGU HUTOA MAWAZO NA KAZI ZAKE KUU KWA WATOTO WAKE AMBAO WANA FAIDA YAKE AKILINI...**

Mimi na Drenda tulipokuwa tukijenga jengo letu la kanisa, The Now Center, ilitubidi tufanye uamuzi. Tulikuwa na washirika 300 pekee tulipoamua kujenga jumba la kudumu na kubwa zaidi kwa ajili ya kundi letu lilokuwa likikua.

Tuliazimia kuchangisha pesa nyingi kadri tuwezavyo ili kutekeleza mradi huo ambao ungegharimu $6 milioni. Hiki kilikuwa kiasi kikubwa cha pesa kwetu wakati huo. Mpango ulikuwa kujenga miundombinu ya msingi kwa takriban dola milioni 4.2 na kisha kuongeza vifaa vilivyobaki vya dola milioni 2, na kujenga kadiri tulivyopata pesa.

Hii haikuwa mara yetu ya kwanza ya kuwa wakarimu kwa miradi ya Mungu, lakini ilikuwa mara yetu ya kwanza kuhusika katika mradi mkubwa kiasi hicho.

Hata hivyo, kama wale watumishi wawili katika hadithi ambao walifahamu wema wa Mungu, mara moja tulitaka kuhusika katika kuchanga fedha, na tulitaka kutoa kwa kiwango ambacho kingehitaji imani na utiifu kwa kile tulichoamini Mungu alikuwa akituambia.

Siku ambayo kanisa nzima lilitangaza kile walichokubaliana kutoa kwa mradi huo, mimi na Drenda tulisema tungetoa $200,000. Wakati huo, hatukuwa na dola 200,000, lakini tulikuwa na mbegu ya takriban dola 20,000 ambazo tungepanda kama mbegu kusudi tupate pesa zilizosalia.

Tulijua, kama Mungu alivyokuwa amefanya hapo awali, kwamba angetuonyesha mahali na jinsi ya kuvuna kiasi hicho cha pesa ambazo mara nyingi zilipita kiasi tulichoagiza.

Baada ya kupanda kile tulichokuwa nacho, tulianza kuomba katika Roho, tukingoja mwongozo na maagizo kuhusu mahali na jinsi ya kupata kiasi cha pesa kilichobaki. Ili uelewe jinsi Mungu alivyoleta pesa hizo, nahitaji kukuambia kwamba tumemiliki kampuni ya kifedha kwa miaka 30 iliyopita. Kampuni hiyo inafanya kazi na wachuuzi na wataalamu mbalimbali, kama nilivyokueleza hapo awali. Wachuuzi wengi wakubwa tunaofanya kazi nao wana makongamano ya kila mwaka na mikusanyiko kwa ajili ya wateja wao.

Kulikuwa na mwaka fulani ambapo mmoja wa wachuuzi wetu alitualika mimi na Drenda twende London, kule Uingereza, kuhudhuria mkusanyiko wao. Tulikaa kwenye hoteli nzuri sana katikati ya jiji la London, na ilikuwa ya kupendeza tu, kama wanavyosema huko London.

Basi, hafla yao ilikuwa upande mwingine wa jiji la London, na makamu wa rais alinialika mimi na Drenda tusafiri pamoja naye kwenye teksi hadi huko, jambo ambalo tulikubali kwa furaha. Tulipokuwa njiani makamu wa rais alitushukuru kwa biashara yote tuliyowafanyia kisha akaanza kutueleza kuhusu programu mpya yenye bonasi waliyokuwa wakianzisha mwaka huo.

Aliendelea kueleza kuhusu muundo wa bonasi hiyo ambapo wangelipa washirika waliopendekeza bidhaa zao. Nilifurahi sana maana nilijua tuliwafanyia biashara ya kutosha kuweza kuhitimu kupata bonasi aliyokuwa akizungumzia.

Kisha, nilipouliza maelezo zaidi, ghafla alisema kwamba kampuni yetu haingefuzu kupata bonasi kulingana na muundo wa uhusiano wetu na kampuni yake.

Sikuamini. Kwa nini alinipa maelezo hayo yote kuhusu mpango huo mzuri kisha akaniondoa kwa dakika ya mwisho? Pia sikuelewa jinsi uhusiano wangu na kampuni yake ulivyoundwa ili nishindwe kuhitimu kupata bonasi.

Ingawa nilimuuliza maswali zaidi, hakunipa jibu lililoeleweka. Jambo pekee nililojua kwa uhakika ni kwamba singeweza kufuzu kupata bonasi; hilo lilikuwa wazi.

Mwaka ulipita na uzalishaji wetu ulikuwa mzuri kwa mwaka huo, kwa hivyo nilipata wazo la kumpigia simu na kuuliza tena juu ya bonasi. Hata hivyo, safari hii nilipompigia simu sikuweza kumpata, hivyo niliacha ujumbe kwa msaidizi wake kuhusu swali langu.

Siku iliyofuata, msaidizi wake alinipigia simu, na kwa sauti ya ukali, akasema kwamba makamu wa rais alikuwa tayari ameniambia mwaka mmoja awali kwamba sikuhitimu, na hakuna kitu ambacho angeweza kufanya kuhusu hilo.

*Naam, sawa, nikawaza, angalau nilijaribu.*

Sasa, nilipokuwa nikiomba kuhusu mahali pa kupata zile $180,000 zilizokuwa zimesalia, nilimsikia Roho Mtakatifu akiniambia nimpigie simu makamu wa rais na niombe hiyo bonasi tena. Nakuambia sikufurahi kusikia hilo. Baada ya majibu aliyonipa nilipomuuliza kwa miaka miwili, nilijua msimamo wake. Alikuwa ameliweka hilo wazi kabisa. Kwa hivyo, niliamua kumtumia barua pepe ili kujaribu kutathmini hisia zake.

Baada ya takriban siku saba nilipokea jibu lake, ambapo alisema kwamba alikuwa ametafakari jambo hilo na kuamua kuipa kampuni yangu bonasi. Ajabu ni kwamba bonasi ilikuwa $200,000! Sasa, hii ndiyo sehemu bora zaidi. Mabadiliko hayo katika mkataba wetu yamedumu sasa kwa MIAKA 14, na tumepokea bonasi hiyo ya $200,000 kila mwaka tangu wakati huo.

Wajua, Mungu ni mtuzaji! Na kuna faida katika kuwa mkarimu kwa kazi Yake.

**WAJUA, MUNGU NI MTHAWABISHAJI! NA KUNA FAIDA KATIKA KUWA MKARIMU KWA KAZI YAKE.**

Kwa hiyo ilitugharimu mimi na Drenda kiasi gani cha fedha kupanda hizo $200,000? Takriban miaka mitano ilipita, na tukaamua kwamba kama kanisa tulihitaji kutafuta pesa zaidi ili kukamilisha mambo machache kanisani na kununua vifaa. Tena, ilibidi mimi na Drenda tuamue ni kiasi gani tulitaka kupanda kwa miradi hiyo, na tukaamua kutoa $500,000.

Lo, hizo zilikuwa pesa nyingi sana. Lakini tulihisi tungeweza kumwamini Mungu baada ya kuona alichofanya na zile $200,000. Tena, tulipanda tulichoweza, ambacho nafikiri kilikuwa dola 50,000, na tulikuwa tukimwamini Roho Mtakatifu atuonyesha mahali na jinsi ya kupata dola 450,000 zilizosalia.

Nafikiri wiki sita zilipita, na nikapokea taarifa kwamba kungekuwa na mabadiliko machache ya kimkataba kuhusu jinsi kampuni yetu ingekuwa inalipwa. Baada ya kufanya hesabu ya mabadiliko hayo, tuliona kwamba katika miaka mitatu iliyokuwa ikija tungepata takriban $630,000 juu ya zile tulizokuwa tukipata. Vyema kabisa, sivyo? Naam, unajua nini? Mabadiliko hayo ya kimkataba yamedumu sasa kwa miaka 11, na tungali tunapata kiwango hicho cha fedha kila mwaka.

Tena, ilitugharimu mimi na Drenda kiasi gani cha fedha kupanda na kuwa wakarimu kwa miradi ya Mungu?

Kwa hiyo kumbuka kwamba Mungu ni Mungu wa faida. Yeye ni mwema na ni mtuzaji.

## SURA YA 3

# JE, UNASTAHILI?

Nafikiri kila mtu amesikia hadithi ya Krismasi na kuhusu wafalme watatu waliomletea Yesu dhahabu, uvumba, na manemane. Umewahi kujiuliza vitu hivyo vilikuwa na thamani gani? Swali bora zaidi ni, "Kwanza kabisa ni kwa nini walimletea vitu hivyo?"

Baada ya kufanya uchunguzi, niligundua kwamba ilikuwa kawaida katika siku hizo kumheshimu mtoto wa mfalme kwa kumletea zawadi kama hizo, maana alionwa kama mfalme mtarajiwa.

Makadirio bora ni kwamba zawadi hizi pengine zilikuwa na thamani kati ya $100,000 na mamia ya maelfu ya dola.

Ni lazima iwe kwamba wale mamajusi walisoma Maandiko na unabii mbalimbali kuhusu Masihi aliyekuwa akija, na walipoona nyota hiyo walikata kauli kwamba alikuwepo, kisha wakasafiri umbali mrefu ili kumletea zawadi hizo.

Dhana ya kwamba walikutana na Yesu horini si sahihi, ingawa inaonyeshwa hivyo katika tamthilia zetu za Krismasi. Tunajua hili kwa sababu Mathayo alisema yafuatayo.

> *Wakaingia <u>nyumbani</u>, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane.*
>
> — Mathayo 2:11

Walikutana na Yesu nyumbani Kwake, wala si horini. Kifungu kinaonyesha kwamba Yeye alikuwa mtoto mdogo, si mtoto mchanga. Kwa hiyo lazima iwe ilichukua muda mrefu kwa mamajusi kufika huko.

Pili, hakuna anayejua kwa hakika mamajusi walikuwa wangapi. Biblia haisemi, lakini imetaja walicholeta. Wakati huo, uvumba na manemane vilikuwa vitu vya thamani zaidi kuliko dhahabu, kwa hiyo zawadi walizoleta zilikuwa za thamani sana.

Kwa hivyo kwa nini ninazungumzia hili? Hebu nikuulize swali, "Kwa nini unafikiri mamajusi hawa walileta zawadi hizi?"

Nitakuambia kwa nini—Yusufu alihitaji riziki kwa ajili ya kazi yake.

Kumbuka...

Mungu daima hufadhili kazi Zake—daima!

Kanisa la Faith Life lilikuwa limejaa. Lilijaa wikendi, katikati ya wiki maana tulikuwa tukifunza zaidi ya watoto 200, na lilijaa vikundi vidogo na wafanyakazi. Tulihitaji nafasi zaidi. Tulianza kujadili ikiwa tulipaswa kufungua chuo cha pili au kujenga kwenye jengo letu. Tuliamua kufanya yote mawili kwa wakati mmoja.

Kwa hiyo, tulikusanya timu ya kuanza kutafuta eneo la kufungua shule, na tukawaelekeza kwa eneo la mji ambalo tulihisi tulipaswa kulitazama kwanza.

Kisha, wakati huo huo, tulianza hatua za kwanza katika kubuni majengo, masomo ya uhandisi, na kadhalika ili kuweza kujipanua. Tulimshirikisha mbunifu na mjenzi na kuanzisha bodi ya ushauri, wote wakiwa na uzoefu katika kazi ya ukandarasi.

Tuligundua kulikuwa na masuala mazito katika kujenga kwenye jengo letu. Muhimu hata zaidi ni kwamba hatukuwa na mabomba ya maji safi na maji taka ya halmashauri ya jiji. Tulikuwa tukitumia maji ya kisima na mfumo wetu wenyewe wa kudhibiti taka.

Maafisa wa kaunti tayari walikuwa wametuambia kwamba hatungeweza kujenga au kuongeza majengo ya ziada katika ekari zetu 36 isipokuwa tuwe na mabomba ya maji safi na maji taka ya halmashauri ya jiji kwenye jengo hilo, maana tulikuwa tumefikia kiwango kilichoruhusiwa. Tulijua hilo mwanzoni tulipoingia katika jengo letu, lakini kulikuwa na majengo mapya zaidi yaliyokuwa yakijengwa karibu nasi nilihisi kwa hakika lazima halmashauri iwe karibu kuweka mabomba ya maji safi na maji taka karibu vya kutosha kutufikia.

Lakini tuligundua kwamba mabomba ya maji safi na maji taka bado hayakuwa mtaani kwetu, kwa hivyo halikuwa suala la kutumia huduma zilizokuwepo. Hazikuwepo.

Tulianza kupata zabuni za kutuwekea mabomba ya maji safi na maji taka hadi kwenye jengo letu na tungerudishiwa sehemu kubwa ya gharama

hiyo maana tungelipwa ada ya kufanya maendeleo mapya. Hutaki kujua gharama yake.

Kwa hiyo, tulirudi kwa halmashauri na kukagua mipango yao na ratiba ya wakati huduma hizo zingepatikana na tukatumaini kwamba wangezingatia kusogeza tarehe hizo karibu kidogo kwa kuwa eneo hilo lilikuwa linakua na zingehitajika hatimaye. Lakini hawakukubali hata kidogo. Kwa hiyo hawakusema ingechukua muda gani kabla ya huduma hizo kupatikana.

Tulijua kwamba hatungeweza kusubiri miaka mingi kwa mabomba ya maji safi na maji taka kupatikana katika eneo letu, kwa hivyo tuliamua kutojenga kwenye jengo letu na kutafuta mahali pa kuweka shule yetu kulifanyika lengo letu kuu. (Imekuwa miaka minne sasa tangu mkutano huo hadi wakati wa kuandika sura hii, na bado hatujasikia chochote kutoka kwa halmashauri kuhusu wakati bomba la maji taka litapatikana.)

**MUNGU DAIMA HUFADHILI KAZI ZAKE—DAIMA!**

Naam, timu yetu ilitafuta eneo bora la kuweka shule yetu bila kufanikiwa. Ilionekana kwamba kulingana na maelezo yetu kuhusu kukodisha au kununua, hakukuwa na majengo yaliyotufaa. Kwa hivyo, tulifikiria kukodisha kituo cha hafla katika eneo hilo, na kila wikendi, hilo lingetugharimu $30,000 kwa mwezi. Juu ya gharama, ingetubidi kuweka vifaa vyetu na kuviondoa kila wiki. Kwa kweli sikutaka kuwatia watu wetu katika hali hiyo. Nilitaka mahali pa kudumu ambapo tungeweza kudhibiti. Hatukuwa na amani kuhusu kituo cha hafla.

Kisha tukafikiria kukodisha nafasi katika duka kubwa nzee. Lakini baada ya kutafakari kuhusu ukarabati na mabadiliko yote yaliyohitajika ili kulileta jengo katika kiwango kilichokubalika, tuliamua kutolichukua.

Mojawapo ya maadili yetu ya kimsingi katika kutafuta jengo ni kwamba lazima lifae katika kusaidia elimu ya watoto wakati wa wiki. Tuna mamia ya familia katika kanisa letu walio na shule ya nyumbani, na huwa tunashirikiana pamoja na kuwa na mafundisho kila wiki. Tumezungumza mara nyingi kuhusu kuanzisha shule siku moja ikiwezekana, kuwa na kituo cha kulelea watoto mchana, programu ya baada ya shule, na programu nyingi zaidi za kuhudumia jumuiya yetu ya mtaa. Tulitaka kupata nafasi ambayo ingetuwezesha kufanya hivyo. Tulikuwa tumepanda ili kupokea jengo hilo, huku tukidai kwamba tumepata jengo zuri lililofaa mahitaji yetu, lakini hatukulipata.

Mimi na Drenda tuliratibiwa kuhudhuria mkutano huko Fort Worth,

Texas, ili kuunga mkono mtandao mpya wa runinga unaoitwa Victory Television Network. Nilipokuwa pale, Bwana alinena nami. Alisema, "*Nataka wewe upande mbegu ya $100,000 katika mtandao huu. Nenda nyumbani kwa kanisa lako, andika hundi, kisha uishike mkononi katika kila ibada na kuitangazia mbegu hiyo kwamba utapata jengo linalofaa kabisa. Pia, mkemee Shetani na umwambie aache kuingilia kazi Yangu. Sema kwamba hili limetimia unapotoa*."

Hivyo ndivyo tulivyofanya. Tulienda nyumbani, na nikampigia simu mweka hazina wetu na kumwambia aandike hundi ya $100,000 kwa ajili ya Victory Television Network. Kisha nikapeleka hundi hiyo kwa kila ibada, na kanisa zima lilikubaliana nami tulipokuwa tukipanda mbegu hiyo kwa ajili ya jengo la kufaa kabisa. Tulimkemea Shetani na kumwambia aache kuingilia na kuchelewesha majibu yetu.

Siku iliyofuata, Jumatatu asubuhi, tulipokea simu kutoka kwa binti yetu, ambaye alisema kwamba tulipokuwa katika ule mkutano huko Texas, wakala wa mmoja wa mali alikuwa amejitolea kuwaonyesha mali fulani nzuri. Haikuwa ya kukodisha wala katika kiwango cha bajeti yetu, maana iliorodheshwa kuuzwa kwa $7.9 milioni. Lakini ilikuwa na thamani kubwa kuliko hiyo maana ilikuwa inauzwa na benki ili kurejesha deni lake. Alisema shule ingefaa sana mahali hapo, lakini, bila shaka, alijua haingewezekana kifedha. Lakini hata hivyo alitaka kujua ikiwa tulitaka kuona mali hiyo. Bila shaka tulikubali.

Kwa hiyo, Jumanne asubuhi, tulikwenda kuangalia mali hiyo. Ilikuwa kwenye ekari saba na hapo awali ilikuwa shule ya upili ya kibinafsi ya hali ya juu. Mali hiyo ilikuwa na jengo la shule ya upili lenye orofa tatu na majengo mawili makubwa zaidi, pamoja na nyumba. Ilikuwa na uwanja wa kukimbia, viwanja vinne vya tenisi, vyumba vya mazoezi ya kuinua uzani, jengo la sanaa lenye maabara ya picha, tanuu mbili za kutengenezea vyombo vya udongo, chumba kilichojaa cherehani na vifaa vya sanaa, makumi ya ala za muziki kwenye chumba cha muziki, na mengine mengi. Mali yote ilikuwa imejaa vifaa kikamilifu.

Tulipozunguka mali hiyo, ilikuwa nzuri ajabu. Lakini wakati huohuo, tulijua kwamba hatukutaka kuingia katika madeni kwa ajili yake. Tulikuwa na takriban dola milioni 3 katika hazina yetu ya ujenzi, lakini hilo lingetufanya tukope karibu dola milioni 5.

Jioni hiyo tulikuwa tumepanga kula chakula cha jioni pamoja na mmoja wa washirika wa huduma yetu. Tulikuwa tumepanga na kusogeza mkutano huu labda mara nne wakati wa msimu wa vuli maana sote tulikuwa

na shughuli nyingi, lakini jioni hiyo mkutano ulifanyika.

Tulipokuwa tukizungumza, yule bwana alianza kuniuliza kuhusu mradi wa ujenzi wetu, nami nikamweleza jinsi tulivyokuwa tukikabiliana na vikwazo. Alinitazama na kusema, "Wajua nini, sihisi kwamba uendelee na hilo. Nafikiri ni bora ufungue shule badala yake." Nilimwambia tulikubaliana na, kwa kweli tulikuwa tumetafuta jengo kwa muda wa miezi sita bila mafanikio. Hata hivyo, tulimwambia tulikuwa tumeona mahali pazuri siku hiyo, lakini hawakuwa wakikodisha na palikuwa nje ya kiwango cha bajeti yetu.

Aliuliza maswali machache juu yake, kisha akamtazama Drenda na kusema, "Je, kama mngeipata bila malipo?" Drenda hakujibu maana alifikiri anafanya utani. Kisha akasema tena, "Drenda, nimesema, je, kama mngeipata bila malipo?"

Akamwuliza, "Unamaanisha nini?"

"Nitaandika hundi kwa ajili ya mali hiyo!" akasema.

Mimi na Drenda tuliduwazwa.

Ili kufupisha hadithi ndefu, alilipa. Ilitubidi tutumie pesa kurekebisha na kubadili jengo ili lilingane na matumizi tuliyokusudia. Matokeo ni chuo kamili. Na jengo limelipiwa!

Singeweza kupanga shule bora zaidi kuliko hii kwa ajili ya mahitaji yetu. Kila kitu kuihusu ni kamili. Kampuni yetu ya bima ilifanya tathmini ya mali hiyo, na ilikuwa na thamani ya dola milioni 11, pamoja na vitu vyote vilivyokuwepo.

Tafakari hili: Sasa tuna mali ya shule yenye thamani ya $11 milioni iliyo na nafasi ya futi za mraba 89,000 bila madeni! Jamani si unapenda hadithi kama hizi?

Kama nilivyosema awali, Mungu daima hufadhili kazi Zake. Ni huduma Yake, si yetu. Tunafanya kazi pamoja Naye katika biashara ya familia.

Sasa, hebu nikwambie kile kilichomfanyikia yule mume na mke waliolipia jengo letu. Kwanza kabisa, kwa sababu ya mchango wao, malipo yao ya kodi yalipunguka kwa kiasi cha pesa zilizokuwa zaidi ya zile walizolipia jengo letu. Vipi? Ilibidi jengo liandikishwe kwa jina lao kwa miaka miwili. Kisha wakatoa jengo hilo kwa huduma yetu kwa thamani iliyokadiriwa wakati huo.

**UFALME HUFANYA KAZI KILA WAKATI!**

Huu ni mkakati ambao unapaswa kufahamu ikiwa wewe ni mchungaji Mmarekani na unahitaji jengo. Kwa hivyo, sote wawili tulipata jengo hilo

bila kulipa pesa zozote kwa sababu ya mpango wake wa busara kuhusu ushuru. Lakini huu haukuwa upande wa kushangaza wa hadithi hii.

Mshirika huyu alikuwa akijaribu kununua biashara nyingine mjini wakati tulipoangalia mali yetu. Ingawa alikuwa akitoa ofa ya pesa taslimu, ilibidi zabuni yake iidhinishwe na wamiliki wa biashara hiyo, na, kwa bahati mbaya, walimjibu kwamba wamempa mtu mwingine. Alikatishwa tamaa sana na uamuzi wao. Aliniambia hakutaka kuachilia; alihisi rohoni kwamba jambo hilo halikuwa limeisha.

Kwa hiyo alipotoa pesa hizo kwa jengo letu, aliniambia alizitoa akiamini kwamba wamiliki wa ile biashara wangebadili mawazo yao, kwa kuwa alikuwa na uwezo zaidi kifedha ilipolinganishwa na zile ofa zingine, na alikuwa akilipa pesa taslimu.

Naam, hakika, baada ya mali yetu kulipiwa, alipokea simu kutoka kwa wamiliki wa ile biashara wakisema kuwa mpango wa awali haukufua dafu na sasa biashara ilikuwa yake ikiwa aliitaka. Alisema ndio, kwa hakika, aliitaka.

Kisha wiki chache kabla ya kumaliza shughuli za ununuzi wa biashara hiyo, jambo lingine lisilotarajiwa kabisa lilitokea ambapo alipata pesa zote zilizohitajika kulipia biashara hiyo pesa taslimu. Hakuhitaji kugusa pesa alizokuwa ametenga hapo awali. Aliniambia ni kama kupata biashara bila kuilipia.

Mara tu aliponunua biashara hiyo, ilithamini zaidi ya mara mbili ya pesa alizolipa. Aliponipigia simu siku ambayo alimaliza kuilipia, alikuwa na furaha nyingi.

Ufalme hufanya kazi kila wakati!

Mshirika huyu alikuwa mkarimu kwa kazi ya Mungu na mtiifu hadi mwisho na tazama kile ambacho Mungu alitufanyia sisi sote. Tulipanda mbegu katika kituo kipya cha Televisheni, agizo lingine la Mungu, na tazama kilichotufanyikia.

Kuwa mkarimu kwa Mungu na watu wa Mungu hufungua milango ambayo hukujua kwamba ipo.

Watu huniuliza kila mara, “Gary, ikiwa ungenipa ufunguo mmoja muhimu leo kuhusu fedha katika Ufalme, ungekuwa upi?”

Kweli, kuna mambo mengi ambayo ningependa kukuambia. Lakini ushauri ufuatao ni wa thamani sana. Kwa hiyo, hakikisha kwamba umeandika maelezo kuhusu kanuni ya Ufalme ifuatayo.

<u>**Ikiwa hujaelewa chochote zaidi kutoka kwa kitabu hiki: Elewa hili!**</u>

Nataka kukupeleka katika Luka 4 ninapoanza kukufungulia sheria hii kuu ya Ufalme. Najua kifungu kifuatacho ni kirefu kidogo kuliko ambavyo ningenukuu kwa kawaida, lakini kusoma kifungu kizima kutakupa wazo kuhusu hali ilivyokuwa na sababu Yesu alijibu jinsi alivyojibu.

> *Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome. Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa:*
>
> *"Roho wa Bwana Yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa."*
>
> *Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, "Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu.*
>
> *Wakamshuhudia wote, wakiyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani Mwake, wakasema, "Huyu siye mwana wa Yusufu?"*
>
> *Akawaambia, "Hapana shaka mtaniambia mithali hii, 'Tabibu, jiponye nafsi Yako; mambo yote tuliyosikia kwamba yametendeka Kapernaumu, yatende na hapa pia katika nchi Yako mwenyewe.'"*
>
> *Akasema, "Amin, nawaambia ya kwamba, hakuna nabii mwenye kukubaliwa katika nchi yake mwenyewe. Lakini, kwa hakika nawaambia, palikuwa na wajane wengi katika nchi ya Israeli zamani za Eliya, wakati mbingu zilipofungwa miaka mitatu na miezi sita, njaa kuu ikaingia nchi nzima; <u>wala Eliya hakutumwa kwa mmojawapo</u>, ila kwa mjane mmoja wa Sarepta katika nchi ya Sidoni.*
>
> — Luka 4:16-26

Tukio hili lilikuwa baada ya Yesu kujaribiwa nyikani na kurudi katika mji Wake wa asili ambapo tunaendelea na hadithi kama ilivyoandikwa.

Kwa sababu Yesu alilelewa Nazareti, walimfahamu sana Yeye na familia Yake, na tunaweza kusema kwamba alikuwa amesoma Maandiko kwenye sinagogi la kwao mara nyingi. Sasa kuna jambo unalohitaji kujua kuhusu andiko ambalo Yesu alichagua kuwasomea. Alikuwa akisoma kutoka katika Isaya 61:1-2, na akasoma mpaka mahali andiko linasema, "***kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa***," kisha akaacha.

Sasa, jambo la kuvutia kuhusu mahali alipokoma ni kwamba ni katikati ya sentensi, kwa hiyo lazima kuwe na sababu ya kufanya hivyo.

Mwaka wa kibali cha Bwana ulikuwa mwaka wa Yubile, na uliwakilisha kurejeshwa kwa Ufalme wa Mungu katika ulimwengu. Ulikuwa kivuli cha yale ambayo Masihi alitaka kurejesha aliporudi. Kwa hiyo, Yesu alipomaliza kuzungumza maneno hayo alisema, "***Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu***," alikuwa akitangaza kwamba Yeye ndiye Masihi!

Kisha akatabiri kuhusu kile ambacho wangemwambia katika siku za usoni, ambacho kimsingi kilikuwa, "Hatukuamini wewe; tuthibitishieni," kwa sababu ya kutomwamini.

> *"Hapana shaka mtaniambia mithali hii, 'Tabibu, jiponye nafsi Yako; mambo yote tuliyosikia kwamba yametendeka Kapernaumu, yatende na hapa pia katika nchi Yako mwenyewe.'"*

Kapernaumu ndipo Yesu alipoweka makao makuu ya huduma Yake na ambapo miujiza Yake mingi ilifanyika. Aliwatabiria kwamba wangesikia maajabu makubwa ambayo yangetokea Kapernaumu, na kumwita aende Nazareti kufanya miujiza ileile huko ili waweze kumwamini. Ukweli ni kwamba, alikuwa akiwasadikisha kuhusu mioyo yao migumu na kutoamini kwao. Alijua hawakumwamini, na kamwe hawangemwamini. Tunajua hivyo kwa sababu aliongeza kwamba pia wangesema, "*Tabibu, jiponye nafsi Yako!*" kwa kurejelea kile ambacho kingesemwa wakati wa kusulubishwa Kwake.

> *Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana, wakitikisa-tikisa vichwa vyao, wakisema, "Ewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe nafsi Yako; ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani." Kadhalika na wale wakuu wa makuhani wakamdhihaki pamoja na waandishi na wazee, wakisema, "Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini."*
>
> — Mathayo 27:39-42

Tangu mwanzo wa huduma Yake hadi mwisho, alikuwa akisema kwamba licha ya yote wangesikia, hawangepokea ujumbe Wake. Kisha akawasimulia hadithi ya Eliya na mjane ili kufanya ujumbe Wake kwao kuwa dhahiri zaidi, ambapo ilimbidi Mungu amwondoe Eliya Israeli kwa

sababu watu wa Israeli walikuwa na mioyo migumu na hawakuamini. Jambo hilo liliwakasirisha sana walimu wa sheria hadi wakamtoa Yesu nje ili wamuue, lakini Biblia inasema alitoweka.

Sasa nataka uandike neno lifuatalo na uliweke mahali ambapo unaweza kulikumbuka, kwa sababu ni muhimu kwa maisha yako ya baadaye ya kifedha. Andika neno “KUTUMWA.” Ndio, neno “KUTUMWA.” Hili ni jambo muhimu sana!

## KUTUMWA

Nataka kwenda kwa 1 Wafalme 17:7-16 ambapo tutapata fumbo lenye nguvu sana litabadili maisha yako kabisa.

> *Ikawa, baada ya siku kupita, kile kijito kikakatika, kwa sababu mvua haikunyesha katika nchi. Neno la Bwana likamjia, kusema, “Ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni, ukae huko. Tazama, nimemwagiza mwanamke mjane wa huko akulishe.” Basi, akaondoka, akaenda Sarepta; hata alipofika langoni pa mji, kumbe! Mwanamke mjane alikuwako akiokota kuni; akamwita, akamwambia, “Niletee, nakuomba, maji kidogo chomboni nipate kunywa.” Alipokuwa akienda kuleta, akamwita akasema, “Niletee, nakuomba, kipande cha mkate mkononi mwako.”*
>
> *Naye akasema, “Kama Bwana, Mungu wako, aishivyo, sina mkate, ila konzi ya unga katika pipa, na mafuta kidogo katika chupa; nami ninaokota kuni mbili ili niingie nijipikie nafsi yangu na mwanangu, tuule tukafe.”*
>
> *Eliya akamwambia, “Usiogope; enenda ukafanye kama ulivyosema; lakini unifanyie kwanza mkate mdogo ukaniletee; kisha ujifanyie nafsi yako na mwanao. Kwa kuwa Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, ‘Lile pipa la unga halitapunguka, wala ile chupa ya mafuta haitaisha, hata siku ile Bwana atakapoleta mvua juu ya nchi.’” Basi akaenda, akafanya kama alivyosema Eliya; na yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi. Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha, sawasawa na neno la Bwana alilolinena kwa kinywa cha Eliya.*
>
> — 1 Wafalme 17:7-16

Hebu niweke msingi. Kulikuwa na ukame mkali, na kijito alichokaa Eliya kilikauka. Ilimbidi ahamie eneo jipya kutafuta chakula na maji.

Mungu alinena naye na kumwagiza "***Ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni, ukae huko. Tazama, nimemwagiza mwanamke mjane wa huko akulishe***." Kumbuka kwamba Sarepta ulikuwa mji wa Kanaani na haukuwa sehemu ya taifa la Israeli wakati huo.

Eliya alipokaribia jiji hilo, alimwona mjane akiokota kuni, na akamwita ampe maji. ***Alipokuwa akienda kuleta, akamwita akasema, "Niletee, nakuomba, kipande cha mkate mkononi mwako***." Alimjibu kwamba hakuwa na chakula, alikuwa na mlo mmoja tu wa kumtosha yeye na mwanawe.

Lakini nabii Eliya alifanya kitu cha ajabu sana, jambo ambalo huwezi kufikiria kwamba linaweza kufanywa unapozingatia jinsi hali ilivyokuwa. Alimwambia aende nyumbani amtengenezee mkate na kumletea kabla ya kujitengenezea. Akiwa na ufahamu jinsi maneno yake yangesikika, alitanguliza agizo lifuatalo kwa maneno yake, "Usiogope." Kisha akamwambia yafuatayo:

> *Kwa kuwa Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, 'Lile pipa la unga halitapunguka, wala ile chupa ya mafuta haitaisha, hata siku ile Bwana atakapoleta mvua juu ya nchi.'"*

Ajabu, angefanya nini? Je, angemwamini nabii na kumpa chakula cha mwisho cha mtoto wake?

> *Basi akaenda, akafanya kama alivyosema Eliya; na yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi. Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha, sawasawa na neno la Bwana alilolinena kwa kinywa cha Eliya.*

Mjane huyo alimwamini, hebu tutazame matokeo—Eliya na mwanamke huyo walikuwa na chakula kila siku. Hebu nibadilishe maneno kidogo na niseme hilo tena, "Kulikuwa na chakula kila siku kwa ajili ya kazi ya Mungu na kwa ajili ya mwanamke huyo na familia yake."

Katika sura iliyopita tulizungumzia woga wa kutoa, kwamba kusingekuwa na pesa za kutosha kulipia mahitaji yako ikiwa ungetoa kwa ajili ya kazi ya Mungu. Kama unavyoona, na utaona kila wakati, hilo halitatokea!

Kwa hiyo, hebu nikuulize swali, "Je, ilimgharimu mjane chochote kutoa mlo huo wa mwisho?" La. Kitendo hicho kiliokoa maisha yake.

Sasa, kabla sijafika kwenye mjadala wetu kuhusu neno KUTUMWA, nataka kuuliza swali lingine. Kwa nini nabii alisisitiza kwamba mjane ampikie keki yake kwanza kabla ya kupika yake mwenyewe? Hata alimwomba mjane amletee keki yake kabla ya kuanza kuoka yake mwenyewe. (Kumbuka, unataka kuwa mwanasayansi wa kiroho kwa kuuliza maswali.)

Hadithi hizi zote zinakuonyesha maarifa muhimu kuhusu sheria na utendaji wa Ufalme. Je, Eliya alikuwa na njaa sana kiasi kwamba hakutaka kungoja mjane atayarishie familia nzima chakula? La, kulikuwa na sababu muhimu sana iliyosababisha hilo. Nabii huyo alijua kwamba mjane alipompa keki kwanza, kabla ya kuoka yake mwenyewe, hatua hiyo ingeleta unga na mafuta yake yote chini ya mamlaka ya kisheria ya Ufalme wa Mungu na kazi Yake. Hebu nirudie tena.

Mjane alipompa nabii (kazi ya Mungu) keki ya kwanza, mafuta yake na unga vilibadili falme. Sasa vilikuja chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu. Hapo ndipo Mungu alipoweza kufanya unga na mafuta kuzidisha kisheria.

Kanuni hii hii ilifanya kazi baadaye katika huduma ya Yesu alipowalisha wale 5,000 kwa mikate mitano na samaki wawili.

Ikiwa unakumbuka hadithi hiyo, Yesu aliwaambia wanafunzi waende waone kile walichokuwa nacho. Walirudi na kusema kwamba walikuwa na mikate mitano tu na samaki wawili. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake wamletee mikate hiyo na samaki. Biblia inasema kwamba alivichukua na kuvibariki kisha akawarudishia wanafunzi Wake. Najua kwamba Yesu hakufanya jambo lolote la kidini, basi kwa nini alifanya hivyo?

Ilimbidi afanye hivyo ama sivyo mikate na samaki havingeongezeka. Wajua, ile mikate mitano na samaki wawili vilikuwa chini ya mamlaka ya wanadamu wakati huo. Mungu hangeweza kufanya lolote kisheria kuvihusu. Lakini vilipotolewa kwa Yesu hiari Naye akavibariki, vilikuja chini ya mamlaka ya kisheria ya Ufalme wa Mungu. Hapo tu ndipo mikate na samaki vingeweza kuzidisha.

Kanuni hii hii iko katika Luka sura ya 5 ambapo Petro, Yakobo, na Yohana walikuwa wamevua samaki usiku kucha na hawakupata chochote. Yesu aliazima mashua ya Petro, na akaisukuma kidogo ufuoni ili kuhubiria umati, kisha akamwambia Petro atupe wavu wake kilindini ili kuvua samaki.

Unakumbuka, mashua zao mbili zilijaa samaki kiasi cha kuanza kuzama. Yesu alipoazima mashua yao, alikuwa akiazima biashara yao ya uvuvi ili aitumie kuhubiri siku hiyo. Mara tu alipoimiliki, biashara yao ilikuja chini ya mamlaka ya kisheria ya Ufalme wa Mungu. Hilo lilifanya iwe halali kwa mbingu kutuma neno la ujuzi kwa Yesu kuhusu mahali samaki walikuwa,

na hivyo kuleta samaki wengi. (Siku zote mimi husema kwamba mtu yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa Yesu atamwambia mahali walipo na jinsi ya kuwavua. Hii ndiyo kanuni ile ile ambayo utakuwa ukitumia pia unapotoa kwa ajili ya kazi ya Mungu.)

Sasa, tunaporudi kwenye hadithi yetu na Eliya, mjane huyu kimsingi alishirikiana na Eliya katika kazi yake na hivyo kavuna thawabu kama yake. Kulikuwa na riziki kwa ajili ya Eliya NA mjane na familia yake. Je, unaona hili?

Nitazungumza zaidi juu ya kanuni hii baadaye kidogo katika kitabu hiki, lakini nataka kwenda kwenye ufunguo mkubwa katika hadithi hii, neno KUTUMWA.

Hebu tujikumbushe. Mungu alimtuma Eliya kutekeleza kazi fulani. Alihitaji riziki ili kutimiza kazi Yake. Tunajua kwamba Eliya alikuwa nabii, kwa hiyo alibeba neno la Bwana popote ambapo Mungu alimtuma. Lakini Mungu alihitaji kazi Yake ifadhiliwe, na hilo wakati wote huhusisha watu.

Katika tukio hili, Mungu hakuweza kupata mjane katika Israeli mwenye imani ambayo ingemtii. Mungu alijua alichotaka kufanya, lakini ilimbidi awe na mtu ambaye angekuwa na mapatano na mbingu ili kufanya iwe halali Kwake kuleta riziki aliyoihitaji Eliya.

Kumbuka, hapakuwa na chakula popote. Watu walikuwa wakifa kila mahali. Halikuwa suala la kutafuta chakula tu, au kwenda sokoni, kwa sababu hakukuwa na chakula chochote. Riziki ya Eliya ilipaswa kuja kupitia kwa Roho wa Mungu.

Maana hapakuwa na mtu yeyote katika Israeli aliyekuwa na imani ya kumwamini, Mungu alipaswa kwenda nje ya Israeli hadi taifa lingine ambapo alimpata mjane aliyekuwa na moyo wa imani. Na kama tulivyosema hapo awali, Eliya alitumwa kwa mjane huyu maalum kwa sababu Mungu alijua angemwamini.

Kwa kumtanguliza Mungu na kutii neno la Bwana kwake, kazi ya Mungu, Eliya, pamoja na familia ya mjane, wote walitunzwa katika kipindi chote cha njaa.

Kwa maana ya hadithi ndiyo hii...

Wakati Mungu ana kazi ya kufanya, Yeye hutafuta duniani ikiwa kuna mtu ambaye anaweza kumwamini, mtu ambaye atamtii na kutekeleza mipango Yake. Pia anahitaji watu ambao watafadhili ajenda Yake.

Kwa hivyo, hebeu niseme hili kwa udhahiri kabisa: Ikiwa unataka kuwa na mawazo makubwa, ikiwa unataka Mungu akupakulie dhana kuu za biashara, lazima ustahili kuzipata! Mungu anaujua moyo wako,

naye anatafuta duniani wale anaoweza kuwaamini kutekeleza kazi Zake. Anatafuta wale anaoweza kuwaamini kufadhili kazi Zake. Kisha atamtumia mtu huyo mpango alio nao kuhuau kukusanya pesa zinazohitajika. Je, unaelewa hili?

Kumbuka, neno la Bwana LILITUMWA kwa mjane huyu, nalo likaokoa maisha yake!

Nakumbuka neno la Bwana lilinijia nianzishe biashara yangu nikiwa na kipaumbele na mamlaka mpya. Nilifanya hivyo, na hilo liliokoa maisha yangu.

Mungu hutafuta wale walio na mioyo ya utiifu ili kufadhili kazi Zake!

Hebu tupitie kanuni tunazoziona katika hadithi hii.

1. Mungu ana kazi anazotaka kukamilisha duniani.
2. Kila kazi inahitaji watu.
3. Kila kazi inahitaji ufadhili.
4. Mungu anatafuta watu duniani watakaotekeleza majukumu Yake.
5. Na Mwenyezi Mungu anatafuta wale duniani watakaofadhili kazi Zake.
6. Tunapofadhili kazi ya Mungu, tunaipa mbingu kisheria mamlaka sio tu ya kututumia kufadhili kazi Yake, lakini pia riziki ya ziada inayokuja hufadhili maisha yetu wenyewe.

Kamwe haitakugharimu kuwa mkarimu! Huwa naliambia kanisa langu, “Daima sema ndio.”

## SURA YA 4

# PESA NI ZA NANI JE?

Je, umewahi kugundua kwamba si pesa zote ulizonazo sasa hivi zilizo zako?

Najua hilo linasikika kama jambo la kichaa, lakini je, umewahi kutambua kwamba huenda Mungu ameweka pesa hizo mikononi mwako kwa ajili ya mtu mwingine?

Najua, najua, labda hujafikiria kuhusu maisha kupitia kwa mtazamo huu, lakini unapaswa kufanya hivyo kwa sababu ni jambo lingine muhimu linalosababisha kuzidisha katika maisha yako.

Tafakari kile ninachosema. Tumekuwa tukizungumzia kufadhili kazi za Mungu, sivyo? Na tulisema kwamba Mungu hutafuta duniani ikiwa atapata watu walio na mioyo inayounga mkono Ufalme na kufadhili kazi Yake. Tunajua kwamba pesa ziko mikononi mwa wanadamu, na ikiwa Mungu atafadhili kazi Zake, atapaswa kupata pesa mikononi mwa watu ambao wako tayari kuziachilia na kuwa wakarimu Kwake na kwa watu Wake.

Kwa hivyo, ni kitu gani kilicho mikononi mwako? Unapotazama kile ulicho nacho, je, unatambua kwamba huenda Mungu ameweka kitu hicho hapo kwa ajili ya mtu mwingine? Au labda amekileta kwako ili ufadhili mradi anaotaka utekelezwe?

Bila shaka, kisheria, ulicho nacho ni chako na ni juu yako kuamua unachotaka kukifanyia. Lakini ikiwa Mungu atakupa pesa, unahitaji kuwa mmoja wa wale walio na kibali mbele Zake. Sivyo?

> *Na Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, Naye atayaongeza mazao ya*

*haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*

— 2 Wakorintho 9:10-11

Tayari tumeangalia aya hizi, lakini kuna jambo hapa ambalo labda hukuona. Mstari wa 10 unasema kwamba Mungu humpa mpanzi mbegu na mkate wa kula.

Tafakari kile kinachosemwa hapa: Mungu *humpa* mpanzi mbegu na mkate wa kula. Mkate wa kula unawakilisha yote unayohitaji katika nyumba yako ili kuishi maisha tele ambayo Mungu amekuandalia. Lakini Yeye humpa *mpanzi mbegu*.

Je, umewahi kupanda bustani au kupanda mbegu za nyasi kwenye ua lako? Unaanza kwa kuweka mbegu ardhini, na unapopanda, unaendelea kuchukua mbegu zingine huku ukipanda kile ulicho nacho tayari mkononi mwako. Kuna mtiririko fulani katika hilo. Unapoachilia mbegu kutoka mkononi mwako, mkono wako unajazwa tena na mbegu mpya ambazo unazipanda pia. Maneno haya, *Mungu humpa mpanzi mbegu*, una maana sawa, kwamba Mungu anampa mbegu mtu aliye katika mchakato wa kupanda.

## MUNGU HUMPA MBEGU YULE ANAYEPANDA!

Paulo pia alisema kwamba Mungu bila shaka hutupatia mkate tunaohitaji, lakini msisitizo katika kifungu hiki ni kuhusu upanzi na matokeo yanayokuja kwetu na kwa wale tunaowaonyesha ukarimu. Kama tulivyokwisha sema, kitendo hiki huisukuma mioyo ya watu kwenda kwa Mungu.

Kwa kuzingatia hilo, nafikiri sote tunaweza kukubaliana kwamba Mungu hutaka kupanda mbegu nyingi ili aweze kuvuna mavuno mengi. Kwa hiyo, kama ungekuwa Mungu, ungempa nani mbegu? Yule aliye mvivu na asiyepanda au yule anayepanda kwa bidii? Nafikiri jibu liko wazi.

Tunapokuwa waaminifu na kile tulicho nacho, Mungu anasema kwamba ataongeza akiba yetu ya mbegu ili tuweze kupanda zaidi na kuwa na athari kubwa zaidi hapa duniani katika Ufalme Wake.

Je, umeona kwamba Paulo alisema kwamba unapopanda na kuvuna, hifadhi yako ya mbegu itaongezeka, na kukuwezesha kuwa mkarimu kila wakati? Ikiwa hii ni kweli (na ni kweli), basi hifadhi yako ya mbegu ni pesa ulizo nazo sasa hivi unapongojea fursa ya kuwa mkarimu. Hifadhi yako ya

mbegu lazima iwe tayari awali kabla ya fursa ya kuwa mkarimu kujitokeza.

Tena, hoja yangu ni kwamba pesa ulizo nazo sasa hivi sio zako zote. Kuna kiasi ambacho Mungu amekupa kuwa mbegu. Mzunguko huu wa kupanda na kuvuna ni mtiririko. Tunapanda, kisha tunavuna; na kadiri tunavyoendelea kufanya hivyo, maadamu hatuli mbegu zetu, mavuno yetu yataendelea kuongezeka, na pia uwezo wetu wa kuwa wakarimu zaidi.

Bila shaka, ukiwa na njaa na kuhitaji mkate, utachukua unachohitaji kutoka kwa biashara yako ya mbegu. Kadiri biashara yako ya mbegu inavyoongezeka, uwezo wako wa kuchukua mkate kutoka humo pia huongezeka.

Lakini nataka kuzungumzia kwa kina zaidi kuhusu mtazamo huu.

Hebu nitoe hoja kwamba Mungu huwapa mbegu Yake wale walio na moyo wa kupanda, sio wale watakaofikiria kufanya hivyo siku moja. Yeye humpa mpanzi.

Kwa hiyo hapa kuna swali: Je, unataka kushughulikia pesa *zako* tu maishani mwako, au unataka kushughulikia pesa za Mungu pia?

**JE, UNATAKA KUSHUGHULIKIA PESA ZAKO TU MAISHANI MWAKO, AU UNATAKA KUSHUGHULIKIA PESA ZA MUNGU PIA?**

James na Ella walikuja kanisani kwetu kwa sababu walisikia mambo ambayo hawakuwa wamewahi kuyasikia katika jamii ya Waamishi ambako wote wawili walikulia. Dhana za Ufalme zilikuwa mpya kwao, na walikuwa wanafunzi makini wa Ufalme. Walisikiliza tena na tena jumbe tulizofundisha kuhusu kuishi maisha ya Ufalme katika Kanisa la Faith Life.

Siku moja, James alimwambia Bwana kwamba alikuwa akisikia hadithi hizi zote kutoka kwa watu kuhusu jinsi Ufalme unavyofanya mambo makuu katika maisha yao, na alitaka kuwa na ushuhuda huo huo. Aliamua kujaribu kutumia sheria za Ufalme alizokuwa amesikia kuhusu. Walienda likizo na wakatumia muda mwingi kusikiliza jumbe kuhusu sehemu maradufu, ambazo nilikuwa nikihubiri wakati huo. Kitabu changu, *Mapinduzi Yako ya Fedha: Nguvu ya Kupumzika* kilikuwa kimechapishwa, na nilikuwa nikifundisha kuhusu mafundisho yaliyomo. Waliamua kujizamisha katika Neno kabla ya kupanda mbegu.

Waliamua kupanda mbegu kwa ajili ya kuvuna dola 10,000, ambazo walihitaji kwa ajili ya matengenezo na mahitaji mengine ya familia zote zilizo na watoto wachanga. Hawakujua pesa zingetoka wapi, lakini walikuwa

wamejifunza kuhusu Ufalme kwa muda mrefu vya kutosha kufikia wakati huo kiasi cha kuhisi kwamba walikuwa na imani ya kutosha.

Wakati huo, James alikuwa mmiliki wa biashara ya kutengeneza magari. Alipokuwa akienda kazini, muda si mrefu baada ya kupanda mbegu ile ili kuvuna dola 10,000, alimwambia Ella kwamba baada ya kujifunza kuhusu sehemu maradufu, alihisi walipaswa kuamini kuvuna sehemu maradufu ya mbegu yao. Alisema aliamini kwamba watavuna $20,000. Ella alisema alishtuka kidogo, lakini alikubaliana na mume wake. James alipokuwa akitoka nyumbani, Ella alisema, "Sawa, $20,000."

Siku moja ya kawaida pale dukani, mmoja wa wateja wa James alikuja na shida ya gari, na alipomaliza kumwandikia oda yake, mteja aliketi ofisini na kumweleza jinsi ng'ombe wake walivyokuwa wakimsumbua. Inaonekana walikuwa wamevunja uzio wake wote na kutoka nje ya shamba. Shamba lake lilipakana na msitu wa kitaifa, kwa hivyo ng'ombe walitangatanga popote walipotaka. Mteja wa James alikuwa mzee kidogo kumliko, na alisema kwa sababu ya uzee hangeweza kuendelea kufuatilia ng'ombe hao, kwamba alikuwa amemaliza nao. Maneno yake yaliyofuata yalimshtua sana James hadi ikabidi ajiulize kama alikuwa amemsikia rafiki yake vyema.

Rafiki yake alisema, "Nimemaliza na ng'ombe hawa, na ndiyo maana ninakupa wote leo. Kuanzia leo na kuenda mbele, wote ni wako." James hakujua la kusema. Hakuwa na shamba. Alikuwa fundi wa magari aliyeishi mjini kwenye robo ya ekari. Ndio, alikulia kwa Waamishi karibu na ng'ombe, lakini hiyo ilikuwa miaka kadhaa awali. Alikuwa karibu kumshukuru na kukataa ofa hiyo wakati alikumbuka mbegu yao. Labda kulikuwa na jambo alilohitaji kuchunguza.

Baada ya kumhoji rafiki yake zaidi, aligundua kuwa alikuwa na ng'ombe 23 na farasi watatu. James alikumbuka mtu mmoja ambaye alimwambia zamani kwamba alitaka kununua ng'ombe kadhaa. Hakutaka kununua ng'ombe wachache taratibu lakini alitaka kuchukua kundi lote la mtu mwingine. James alimpigia mtu yule simu na ndio, alisema angependa hilo. James akamuuliza angetaka kulipia ng'ombe hao kiasi gani cha pesa, naye akawaza kwa muda kisha akasema, "Oh, labda dola 20,000."

James hakuamini kile alichosikia. Haya yote yalitokea baada ya kuondoka nyumbani siku hiyo wakati alipomwambia Ella kuhusu msukumo wa Roho Mtakatifu wa kuamini kuvuna sehemu maradufu. Rafiki yangu aliniambia ilikuwa kazi nyingi sana kuwafuatilia ng'ombe na kuwasafirishwa kwenda kwa mtu huyo, lakini alifanikiwa. Kisha James akaniambia alikuwa na hakika kabisa kwamba Ufalme wa Mungu unaweza

kufanya chochote na kwamba hangezuiliwa na uwezo wake mwenyewe.

Aliporudi nyumbani siku hiyo ya kwanza na kumwambia Ella kuhusu ng'ombe hao, alisema alishtuka tu. Ikiwa ungewauliza James na Ella kuhusu neema ya Mungu, ni bora uwe na masaa ya kutosha kwa sababu wana mengi ya kusema.

Huu ni mfano mwema ambapo Roho Mtakatifu anamuonyesha mtu mahali pa kuvuna mavuno kwa sababu ya kuwa mkarimu kwa Mungu. Mara tu tunapopanda mbegu, tutahitaji kukumbuka kwamba kile Roho Mtakatifu alichotuonyesha labda kinaweza kuonekana kama jambo la *kichaa!* Namaanisha, James hangepata wazo hili akiwa anaandika kwa karatasi na penseli na kufanya mazoezi ya mwili huku akitafuta suluhu mawazoni.

Tuseme Petro kwa mfano. Nina hakika katika mawazo yake hangewahi kufikiria kutazama ndani ya mdomo wa samaki kutafuta sarafu ya kulipa kodi, au kwamba Rabi anayetembea ufuoni wa bahari angeweza kumwambia mahali hasa pa kushusha wavu wake ili kuvua samaki wengi hivyo.

Mimi na Drenda tulipokuwa na madeni katika miaka hiyo tisa yenye dhiki na misukosuko, wazo kwamba siku moja tungemiliki kampuni inayosaidia watu kujikwamua kutoka kwa madeni au jambo la kushangaza hata zaidi kwamba tungekuwa na kipindi cha runinga kinachoonyeshwa kote duniani kinachoitwa, *halingewezekana.*

Kamwe usimwekee Mungu mipaka.

Kwa hiyo, hebu turudie, na tujikumbushe kwamba Mungu humpa mpanzi mbegu—yaani yule anayepanda na anayetamani kupanda!

Hebu tuendelee. Ninataka sasa tutazame kile ambacho mimi binafsi hukiona kuwa mojawapo ya mifano ya kina zaidi ambayo Yesu aliwahi kufundisha kuhusu Mungu kufanya kazi na watu na jinsi wanapaswa kustahili kutumiwa. Hili hakika litakufanya ukome na kutafakari.

> *Tena, aliwaambia wanafunzi Wake, "Palikuwa na mtu mmoja, tajiri, aliyekuwa na wakili wake; huyu alishitakiwa kwake kuwa anatapanya mali zake. Akamwita, akamwambia, 'Ni habari gani hii ninayosikia juu yako? Toa hesabu ya uwakili wako, kwa kuwa huwezi kuwa wakili tena.'"*
>
> *"Yule wakili akasema moyoni mwake, 'Nifanyeje? Maana, bwana wangu ananiondolea uwakili. Kulima, siwezi; kuomba, naona haya. Najua nitakalotenda, ili nitakapotolewa katika uwakili, wanikaribishe nyumbani mwao.'"*
>
> *"Akawaita wadeni wa bwana wake, kila mmoja; akamwambia wa*

*kwanza, 'Wawiwani na bwana wangu?' Akasema, 'Vipimo mia vya mafuta.' Akamwambia, 'Twaa hati yako, keti upesi, andika hamsini.'"*

*"Kisha akamwambia mwingine, 'Na wewe wawiwani?' Akasema, 'Makanda mia ya ngano.'"*

*"Akamwambia, 'Twaa hati yako, andika themanini.' Yule bwana akamsifu wakili dhalimu kwa vile alivyotenda kwa busara; kwa kuwa wana wa ulimwengu huu katika kizazi chao wenyewe huwa na busara kuliko wana wa nuru. Nami nawaambia, 'Jifanyieni rafiki kwa mali ya udhalimu, ili itakapokosekana wawakaribishe katika makao ya milele.'"*

*"Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia. Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli? Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?*

*Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana, ama atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali."*

*Basi Mafarisayo, ambao wenyewe ni wapenda fedha, waliyasikia hayo yote, wakamdhihaki. Akawaambia, "Ninyi ndinyi mnaojidai haki mbele ya wanadamu, lakini Mungu awajua mioyo yenu; kwa kuwa lililotukuka kwa wanadamu huwa chukizo mbele za Mungu."*

— Luka 16:1-15

Kuna mengi ya kuangalia katika mfano huu. Kwanza, tunaona kwamba mmiliki tajiri alikuwa amemweka meneja kusimamia shughuli zake, na inaonekana kwamba meneja alikuwa akifuja mali ya bwana wake na alikuwa amejiondolea sifa za kuendelea na kazi hiyo. Alipojua kwamba amepoteza kazi yake, haraka aliwaita wale wote waliokuwa na deni la bwana wake na kuwapunguzia pakubwa kiasi cha deni walilokuwa nalo, hata nusu ikiwa wangefanya haraka.

Sasa, bila shaka, mmiliki hakujua kabisa kile meneja alikuwa akifanya. Lakini meneja huyo mdanganyifu aliwaza ikiwa angewapa ofa nzuri, basi wangemwona kuwa mtu mwema mara tu atakapoachishwa kazi, na alitumaini kwamba wangempa kazi katika operesheni zao. Mmiliki aliposikia kile meneja mdanganyifu alichofanya, alimwita na:

*Yule bwana akamsifu wakili dhalimu kwa vile alivyotenda kwa busara.*

Ufafanuzi wa busara ni: Kuwa na au kuonyesha ufahamu wa werevu au ustadi, haswa katika masuala ya vitendo. Kuwa na nia ya au kuonyesha usanii na ujanja; hila.

Mmiliki aliona kwamba meneja alikuwa na uwezo wa kuunda na kutekeleza mpango ambao ungezalisha faida, katika tukio hili si kwa manufaa ya mmiliki bali yeye mwenyewe—jambo ambalo hakuwa ameona kutoka kwa meneja huyu ilipomhusu. Walakini, ilipohusu suala la kujitunza mwenyewe, alikuwa makini na alikuwa, kwa kweli, mwerevu sana na wa kina. Alionyesha uwezo wa kuanzisha jambo ilipohusu mambo na hali yake njema lakini hakuonyesha lolote kati ya hayo ilipomhusu bwana wake. Hebu niwe mkweli hapa—alikuwa mwajiriwa!

Sasa, hebu niulize swali gumu sana: Je, wewe ni Mkristo mwajiriwa?

Je, unajali zaidi kuhusu ustawi wako kuliko unavyojali biashara ya Mungu? Je, unajali zaidi yale yanayokuhusu kuliko unavyoyajali yale yanayomhusu Mungu? Je, unafuja mali ya Mungu?

Lo, najua haya ni maswali magumu. Ndio maana nikasema mfano huu ni wa maana sana, kwa sababu unakata hadi moyoni na kufichua mitazamo yoyote mibaya iliyofichwa humo.

Yesu alitupa picha iliyofafanua mwajiriwa ni nani katika Yohana 10:11-13.

> *Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. Mtu wa mshahara, wala si mchungaji, ambaye kondoo si mali yake, humwona mbwa-mwitu anakuja, akawaacha kondoo na kukimbia; na mbwa-mwitu huwakamata na kuwatawanya. Yule hukimbia kwa kuwa ni mtu wa mshahara; wala mambo ya kondoo si kitu kwake.*
>
> — Yohana 10:11-13

Tafsiri ya 'New King James' (mst. 13) inasema hivi:

> *Mwajiriwa hukimbia kwa sababu ni mwajiriwa, wala hajali kondoo.*

Katika hadithi hii, alikatazwa kushughulikia pesa za mmiliki kwa sababu hakujali ustawi wake; alijijali mwenyewe tu. Sasa, bila shaka, bado alikuwa na uwezo wa kujitengenezea pesa, lakini hangekuwa tena na fursa ya kushughulikia pesa zake NA za mmiliki.

Ninaamini tunaishi katika nyakati ambazo mtazamo wa kuajiriwa

unasifika sana nchini Amerika na ulimwenguni.

Nina hakika umekuwa katika mgahawa na kuona meza na sakafu chafu, na pale pembeni kuna wafanyakazi wachache wanaojivinjari. Au umeingia kwenye mgahawa wa vyakula vya haraka labda dakika 30 kabla ya kufungwa, na unashtuka kuona viti vyote juu ya meza na wafanyakazi wamejipanga karibu na saa wakisubiri kuondoka. Unajua, bila kuuliza, kwamba mmiliki hayupo. Hao wote ni waajiriwa. Hawajali faida ya biashara. Wapo ili kupata mshahara wala si kitu kingine.

Waajiri wengi huniambia hali inazidi kuzorota kiasi kwamba mfanyakazi anapowasili kazini katika wakati unaofaa, itakuwa dhahiri kwamba yeye ni tofauti na wengine. Waajiri wanalilia wamiliki, sio wachukuaji. Wanataka wafanyikazi ambao watafanya kazi na kujali kana kwamba wanaendesha biashara zao wenyewe. Huwa wananiambia kwamba mfanyakazi aliye na tabia kama hiyo hutafutwa na kupandishwa cheo.

Mungu si tofauti. Yeye hutafuta watu wanaojali kile anachokijali na kuchukia kile anachokichukia.

Katika 1 Samweli 15, Mungu alimwambia mfalme Sauli awashambulie Waamaleki kwa sababu ya yale waliyowafanyia Waisraeli walipokuwa wakitoka Misri. Mfalme Sauli aliambiwa asiache chochote hai. Hawakupaswa kurudi na mnyama yeyote, lakini hivyo ndivyo Sauli alivyofanya:

> *Lakini Sauli na watu wake wakamwacha Agagi hai, na katika kondoo walio wazuri, na ng'ombe, na vinono, na wana-kondoo, na chochote kilicho chema,*
>
> *Wala hawakukubali kuwaangamiza; bali chochote kilichokuwa kibaya na kibovu, ndicho walichokiangamiza kabisa.*
>
> — 1 Samweli 15:9

Tazama alichosema Mungu katika mistari 10-11:

> *Ndipo neno la Bwana likamjia Samweli, kusema, "Najuta kwa sababu nimemtawaza Sauli awe mfalme; maana amerudi nyuma, asinifuate, wala hakufanya nilivyomwamuru." Samweli akasikitika, akamlilia Bwana usiku kucha.*

Kisha tunamwona Mungu akinena na Samweli kuhusu Sauli katika 1 Samweli 16:1.

> *Bwana akamwambia Samweli, "Hata lini utamlilia Sauli, ikiwa Mimi nimemkataa asiwamiliki Israeli? Ijaze pembe yako mafuta, uende, nami nitakupeleka kwa Yese, Mbethlehemi; maana nimejipatia mfalme katika wanawe."*

Jinsi yule meneja mdanganyifu alivyokatazwa kushughulikia mambo ya mmiliki, ndivyo Sauli alivyokataliwa. Na unajua nini? Mimi na wewe tunaweza kunyimwa sifa pia pia.

Mungu hutafuta nini? Atamwamini nani?

> *Na alipokwisha kumwondoa huyo, akamwinua Daudi awe mfalme wao ambaye alimshuhudia, akisema, "Nimemwona Daudi, mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo Wangu, atakayefanya mapenzi Yangu yote."*
>
> — Matendo 13:22

Ikiwa tunaweza kunyimwa sifa, hiyo inamaanisha kwamba tunaweza kuhitimu pia. Unaweza kusema, "Vema, Gary nitafanyaje hilo?" Mfano huu unajibu swali lako.

> *"Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia. Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli? Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?*
>
> *Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana, ama atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali."*
>
> — Luka 16:10-13

Acha niseme wazi: Lazima upite mtihani wa kuwa mwaminifu. Ikiwa unaweza kuwa mwaminifu katika yale yaliyo madogo sana, unaweza kuaminiwa na mambo makubwa. Jaribio daima huanza katika mambo ya asili kisha linaingia katika milki ya kiroho. Lazima uwe mwaminifu na mali ya ulimwengu kabla ya Mungu kukuamini na mali Yake. Ikiwa wewe si mwaminifu na mali ya mtu mwingine, ni nani atakayekupa mali yako mwenyewe? Hakika si Mungu.

Hapa kuna matumizi ya mfano huu katika maisha yetu wenyewe.

**Wakristo wengi humpa Mungu mabaki.**

Wakristo wengi hutazama bajeti zao na kuamua, “Hiki ndicho ninachoweza kutoa.” Walakini hawana shida kwenda kununua mashua mpya kabisa siku hiyo hiyo.

Sasa, sijaribu kumfanya mtu yeyote ahisi hukumu, na Mungu hakika hajali kama una mashua nzuri au la. Ninauliza swali rahisi: Je! unataka kushughulikia pesa zako tu au zako na za Mungu?

Ukitafuta katika Google kile ambacho Mkristo wa kawaida hutoa, unaweza kushtuka. Niliona takwimu moja iliyosema Mkristo wa kawaida hutoa takriban $13 au zaidi kidogo kanisani kila juma.

Niliangalia takwimu nyingi kuhusu utoaji, na zote zilikuwa za kukatisha tamaa. Kama nilivyosema, Wakristo wengi humpa Mungu mabaki. Tena, tafadhali elewa kuwa sijaribu kuhukumu au kuibua hatia. Ninatoa hoja tu—na nafikiri Neno la Mungu lina mtazamo wangu—kwamba Mungu hatafuti waajiriwa; anatafuta wamiliki.

Pili, Mungu hatafuti watu wanaohisi hatia na kujilazimisha kutoa. Mungu humpenda mtoaji mwenye moyo mkunjufu, kulingana na 2 Wakorintho 9:7.

Sauli alikataliwa kwa kutofanya kile Mungu alichoagiza, lakini Daudi alichaguliwa kwa sababu alitii na kufanya kile ambacho Mungu alihitaji kifanywe.

Kwa hivyo, hebu nipendekeze mtazamo mpya. Je, ikiwa tungegeuza dunia yetu juu chini na kuamua kuishi maisha ya kumtanguliza Mungu na kuishi kwa mabaki? Ninaweza kukisia tu kwamba mabaki yako yangekupita haraka na ungeishi maisha yenye baraka.

Mtazamo huu ulifanya kazi katika maisha ya RG LeTourneau. Alianzia maisha ya unyenyekevu akiwa na elimu ya darasa la saba tu, lakini alijifundisha na, hatimaye, akajenga himaya ya viwanda. Mashine zake za kifahari zilisaidia kushinda vita vya pili vya dunia na kujenga miundombinu ya barabara kuu ya Amerika ya kisasa. Mwishoni mwa maisha yake, alikuwa na hati miliki 300.

Siri yake? Alimpa Mungu 90% ya pesa zake.

Sasa, sikuambii ufanye hivyo. Hayo yalikuwa mapatano ambayo yeye na Mungu walifanya alipokuwa na umri wa miaka 30 na alikuwa na madeni mengi. Alimfanya Mungu kuwa mshirika wake wa kibiashara (kama alivyomwita), na hilo lilimfanikisha.

Mungu aliponiita kuanzisha kanisa, tayari nilikuwa na kampuni yangu,

Forward Financial Group. Ilikuwa imefanikiwa sana na ilikuwa nambari moja kati ya ofisi 5,000 nchini kote. Nilimuuliza, “Vipi kuhusu Forward Financial Group? Je, niifunge na kulenga kazi ya uchungaji?”

Mwenyezi-Mungu akanijibu na kusema, *“La, endelea maana inasaidia watu wengi.”* Ndivyo nilivyofanya.

Nitakubali kwamba wakati mwingine ilikuwa vigumu kufanya yote mawili, lakini imesaidia maelfu kwa maelfu ya watu kwa miaka mingi. Nilipoanza kazi ya uchungaji, nilidhani kwamba kampuni ingepungua katika uzalishaji maana singeweza kuhusika sana. Lakini mimi na Drenda tulipoyatoa maisha yetu kutimiza maagizo ya Mungu, niliona kinyume na hilo kabisa. Ingawa nilikuwa nikifanya kazi ya kampuni katika muda wangu wa ziada tu, bado ilikuwa ikinawiri.

Kati ya mamia ya ofisi, tulikuwa katika ofisi tano hadi kumi za juu nchi nzima na tulitambuliwa. Nilitabasamu maana nilijua kwamba muda wangu mwingi ulitumika katika uchungaji wala si kwa kampuni. Mungu aliniheshimu kwa kunipa kibali na hekima hivi kwamba wale duniani waliokuwa wakitafuta pesa kwa mioyo yao yote walilazimika kukoma na kushangaa jinsi nilivyofaulu.

Nakumbuka wakati mmoja nilikuwa nimeketi mezani katika mkusanyiko fulani na yule jamaa aliyekuwa ameketi karibu nami alianza kuniuliza ni kiasi gani cha uuzaji nilichokuwa nimefanya. Ilinibidi nitabasamu huku nikisema, “Hakuna.” Kisha akauliza, “Basi unafanyaje biashara nyingi hivyo?” Nilimwambia tulifanya kazi ya kuambia watu tu na kwamba ni Mungu aliyetubariki. Alitikisa kichwa tu maana hakuweza kunielewa.

Wakati mmoja, msimamizi wa mmoja wa wachuuzi wetu alinipigia simu na kutaka kujua ikiwa ningehutubia wahudhuriaji wa konga-mano lao kuhusu jinsi nilivyoweza kuzalisha bidhaa nyingi sana. Nilisema nitafanya hivyo kwa furaha. Kisha akaanza kuniuliza maswali kuhusu jinsi operesheni yetu ilivyofanya kazi na jinsi tulivyofanya biashara. Bila shaka, ilibidi nimwambie jinsi tulivyomtumaini Mungu na jinsi alivyotubariki na kutupa kibali. Baada ya kumwambia kwamba nilifanya kazi masaa chache tu kwa wiki na nilikuwa mchungaji wakati wangu wote, akasema, “Vema, nilifikiri una mkakati wa kina wa uuzaji uliopo ambao ungeshiriki nasi. Sidhani kama hilo ndilo nililo nalo

**MUNGU ANAONA. KILA KAZI INAKUPA MAFUNDISHO YA SIKU ZIJAZO, KWA HIVYO USIDHARAU NYAKATI ZA MWANZO MDOGO.**

akilini, lakini nashukuru kwamba ulikuwa tayari kutushirikisha hilo." Lo, hiyo ilikuwa hasara kwao. Ningesaidia watu wengi huko.

Nimesema katika kitabu hiki chote kwamba ukiitunza kazi ya Mungu, Naye ataisimamia yako!

Kwa hivyo, hebu nikuulize swali tuliloanza nalo, "Pesa ni za nani je?"

Je! ungependa kushughulikia pesa zako mwenyewe, kama yule meneja mdhalimu, au unataka kushughulikia pesa za Mungu pia? Unaposhughulikia pesa za Mungu, biashara yako ya mbegu hutiwa nguvu na hekima na neema ya Mungu, ambayo inasababisha mavuno yako ya kibinafsi ya mkate pia kuongezeka pamoja na hilo.

Nina hakika kwamba Mungu hajali ikiwa una mamilioni maadamu ana moyo wako!

Kumbuka, yote huanza na kazi ndogo ndogo ambapo hakuna anayejua jina lako. Ingawa unaweza kufikiri hakuna anayejali unachofanya katika kazi hiyo ya muda, Mungu anaona. Kila kazi inakupa mafundisho ya siku zijazo, kwa hivyo usidharau nyakati za mwanzo mdogo. Ifanye kwa bidii yote kana kwamba unaimiliki. Ninakuhakikishia utang'aa kama nyota usiku na utajiweka mahali pa kupandishwa cheo na kupendelewa.

## SURA YA 5

# UNAHITAJI MSHIRIKA!

Kama unavyojua tayari, nimekuwa katika biashara ya kifedha kwa karibu miaka 40. Kwa miaka mingi, kumekuwa na watu wengi wanaoniuliza jinsi ya kuanzisha biashara na kile kinachofanya biashara kukua.

Bila shaka, kuna mambo mengi ambayo watu wanahitaji kujua, lakini jambo muhimu zaidi ninaloweza kusema ni kwamba unahitaji *mshirika*.

Sasa, kama mchungaji kwa miaka mingi, nimeona watu wengi sana ambao walifikiri ingekuwa vyema kufanya biashara na rafiki zao kutoka kanisani, lakini mambo yote yakaenda mrama. Marafiki hukosana, na mara nyingi hata huacha kuzungumziana, kisha uhusiano unaharibika. Kwa sababu nimeona jambo hili mara nyingi sana, ni nadra sana kwangu kupendekeza marafiki kuanzisha biashara pamoja isipokuwa kama mmeweka mipaka dhahiri iliyoandikwa.

Hata hivyo, kuna mshirika ambaye siku zote nasisitiza umchukue, naye ni Mungu.

Katika sura ya awali, tulizungumza kuhusu mwanamke aliyempokea nabii Eliya na kumpa chakula chake cha mwisho. Tuliona jinsi tendo hilo la imani lilivyoleta chakula kwa nabii, kazi ya Mungu, na kwa familia ya mwanamke huyo kila siku. Mwanamke alishirikiana na nabii katika kazi yake, na kwa kufanya hivyo, upako na riziki iliyokuwa juu ya kazi ya nabii ilifanyika yake pia. Walikuwa washirika.

Kote katika kitabu hiki, tumekuwa tukizungumzia ukarimu kwa kazi ya Mungu. Kisha nimekuambia jinsi ukarimu unavyokupa kibali na watu na Mungu pia.

Katika sura hii, ninataka kushiriki nawe kanuni nyingine yenye nguvu ya Ufalme wa Mungu ambayo itapeleka fedha zako katika kiwango kipya

kabisa—kanuni ya ushirikiano.

> *Ikawa makutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni.*
>
> *Hata alipokwisha kunena, alimwambia Simoni, "Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki."*
>
> *Simoni akajibu akamwambia, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu."*
>
> *Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.*
>
> — Luka 5:1-7

Najua tayari nilitaja hadithi hii hapo awali nilipozungumza kuhusu mashua na biashara ya uvuvi kubadilisha falme (au mamlaka) wakati Petro (Simoni) alipomkopesha Yesu mashua yake ili ahubiri kutoka humo. Nilitaja pia kwamba walivua samaki wengi sana mashua mbili karibu zizame. Kumbuka, Petro alisema alikuwa amevua samaki usiku kucha na hakupata chochote. Sasa, masaa machache tu baadaye, alikuwa na samaki wengi sana hivi kwamba hangeweza kuwavuta kwa haraka vya kutosha. Tofauti ilikuwa nini? Ufalme, bila shaka, lakini pia *ushirikiano*. Hebu nifafanue.

> *Akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani.*

Hebu tuelewe hali ilivyokuwa kwa udhahiri. Walikuwa wapi, na walikuwa wakifanya nini Yesu alipokuja? Hawakuwa wakivua samaki; walikuwa ufukweni wakiosha nyavu zao baada ya kuvua samaki usiku kucha na kukosa kupata chochote.

Yesu alipoona kwamba mashua hizo zilikuwa pale, alimwomba Petro ikiwa angeweza kusonga kidogo kutoka ufuoni ili aweze kuhubiria umati

akiwa ndani ya mashua. Kwa hiyo Yakobo na Yohana washiriki wa Petro, walikuwa wapi Yesu alipoingia ndani ya mashua? Walikuwa ufuoni pamoja na ile mashua nyingine na nyavu zao.

Baada ya kuhubiri, Yesu alimwambia Petro ashushe nyavu zake kwenye kilindi cha maji ili avue samaki. Na unajua hadithi hii. Alivua samaki wengi sana hata nyavu zake zikakaribia kukatika. Kwa hiyo akawaita washirika wake wamsaidie kuvuta samaki. Na Biblia inasema kwamba mashua zote mbili zilikuwa karibu kuzama, maana zilijaa samaki.

> *Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.*

Sasa, swali muhimu ndilo hili: Je, Yakobo na Yohana walitumia imani kiasi gani kufanya mashua zao zijae sana kiasi cha kukaribia kuzama?

Tafakari jambo hili—walikuwa ufuoni na nyavu zao. Petro ndiye aliyekubali kumpeleka Yesu ndani ya mashua yake. Yeye ndiye aliyesema, *"Lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu."* Kwa hivyo jibu sahihi ni hakuna! Yakobo na Yohana hawakuvuna shehena hiyo ya samaki kwa sababu ya imani yao; ilikuwa ni kwa sababu ya imani ya Petro. Petro aliwaita tu wenzake waliokuwa ufuoni waje kumsaidia kuvuta samaki. Ajabu ni kwamba, mashua yao ilijaa sawasawa na ile ya Petro, ilifurika.

> *Simoni akajibu akamwambia, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu."*

Kwa hiyo, ikiwa ni imani ya Petro iliyoleta samaki na kujaza mashua yake, basi kwa nini mashua ya Yakobo na Yohana ilijaa kiasi cha samaki sawa na mashua ya Petro?

Maandiko yanajibu swali hilo—inasema walikuwa *washirika*.

Ufafanuzi wa mshirika katika Kamusi ya Kiingereza ya Collins ni:

> **Mtu ambaye anashiriki au anahusishwa na mwingine katika hatua au jitihada fulani; kwa kawaida kushiriki hatari na faida zake.**

Ubia ni mfumo wa kisheria ambapo watu hushiriki katika hatari,

gharama na faida ya biashara. Kwa hiyo, Petro alipompa Yesu mashua atumie, kisheria alikuwa akimkopesha Yesu *biashara hiyo*, wala si mashua pekee. Kitaalam, Yakobo na Yohana pia walikuwa na sehemu katika mashua ambayo Petro alimkopesha Yesu atumie, na kwa sababu walikuwa washirika, mashua zote mbili zilijaa kwa usawa.

Yakobo na Yohana walivuna mavuno yaleyale ambayo Petro alivuna hata kama hawakutumia imani hata kidogo katika hali hiyo. Nafikiri siku hiyo walifurahi kwamba Petro alikuwa mshrika wao. Sivyo? Nafikiri ndivyo. Acha nikupe mfano wa kibinafsi zaidi kuhusu kanuni hii.

Mimi na Drenda ni wamiliki wa ekari 60 za ajabu, zenye mchanganyiko wa miti, mabwawa, na nyasi. Ni mahali pazuri kabisa pa kuwinda kulungu. Kuna mimea inayozunguka mali yetu, na misitu na mabwawa ni sumaku za asili kwa kulungu.

Nilijenga ofisi yangu juu ya karakana yetu, na ina rafu za mbao na mahali pa moto la gesi. Ni ofisi tulivu, yenye starehe, inafanana pango la watu, na ninapenda kufanyia kazi yangu humo. Kitu pekee kilichokosekana ni kulungu dume mzuri juu ya dawati langu. Kusema kweli, sijawahi kuwa na haja ya kuwinda kulungu wakubwa, kwa sababu mimi ni mwindaji wa nyama. Na sikuwa nimewahi kumwinda dume mkubwa vya kutosha kutufanya tutake kumweka juu ya dawati langu.

Tulikuwa tumeishi kwenye nyumba hiyo kwa miaka mitano Drenda aliposisitiza kwamba nimwinde kulungu dume mkubwa ili tumweke kwa ofisi yangu. Hadi wakati huo, sikuwa nimeona kulungu dume mkubwa kwenye mali hiyo. Kila msimu wa kulungu nilienda kuwinda na nilikuwa nimeua kulungu nzuri kadhaa zenye pembe nane, lakini sikupata dume ambaye angefaa kuwekwa ofisini mwangu.

Lakini nilipoendelea kutafakari, mwaka huo nilikubaliana na Drenda. Nilimwambia Drenda kwamba nilifikiri kuwinda dume mkubwa wa kuweka kwa ukuta wa ofisi yangu. Ingawa dirisha la jikoni letu liko upande unaotazama msitu na shamba letu, sikuwa nimewahi kuona dume mkubwa hata mmoja msituni.

Kwa hivyo mimi na Drenda tulipanda mbegu kwa ajili ya dume kulungu mkubwa. Niliandika kwenye hundi yangu kwamba nilikuwa nikipanda mbegu ya dume mwenye pembe kumi au zaidi. Tuliiombea mbegu hiyo, nami nikaiweka juu ya meza yangu ili kuituma. Bahasha hiyo ilikaa hapo kwa siku tatu, na sikuweza kuituma. Nilijua kwamba sikuwa na imani ya kumuua dume mwenye pembe 10. Nilikuwa na imani ya dume mwenye pembe nane, sita, au nne siku nzima. Lakini nilikuwa na shida kuona dume

mkubwa nikiwa na uhakikisho huo wa imani unaosema, "Ninajua kwamba nitamuua dume mwenye pembe 10 au zaidi nitakapokwenda kuwinda."

Nilikuwa na uzoefu wa kutosha katika Ufalme kujua kwamba sikuwa na imani. Kwa hivyo nilirarua hundi hiyo, nikaandika hundi iliyosema "kwa ajili ya dume mwenye pembe nne au zaidi," na kuituma.

Usiku kabla ya kwenda kuwinda, nilimweleza Drenda kuhusu kile nilichokifanya. "Sina imani ya dume mkubwa kiasi hicho," nilimwambia. Alinitazama na kusema, "*Wewe* una imani kwa ajili ya kulungu, *nami* nitakuwa na imani kwa ajili ya dume wa kombe. Mungu ana uwezo wa kufanya zaidi ya yote uyaombayo au uyawazayo!"

Asubuhi ilifika huku kukiwa na misukosuko ya kawaida ya panya wa msitu na ndege huku harufu ya majani ya msimu wa vuli ikirudisha akilini mwangu mawinda mengi ya kulungu. Sikuwa nimekaa hapo kwa muda mrefu sana, labda dakika 20, niliposikia sauti ya dume msituni. Dume alikuwa akielekea moja kwa moja kwenye mti wangu, na nilijitayarisha kumrushia mshale.

Kadiri dume alivyokaribia, niliona alikuwa na pembe nne, sawa kabisa na wale ambao kwa kawaida niliwawinda, maana ni wazuri sana kula. Alifika takriban yadi 25 kutoka kwangu, kisha nikaachilia mshale. Kwa chukizo nilitazama mshale ukimgonga na kuruka juu, kisha nikajua kwamba ingebidi nimfuate kulungu huyo.

Aliruka msituni kisha akaruka kwenye shamba la mahindi lililopakana na msitu na kutoweka. Niliweza kuisikia akikimbia kwenye mahindi na nilijua kutokana na jinsi alivyokuwa akitoroka kwa nguvu kwamba ningekuwa na kazi nyingi ya kumfuatilia. Nilingoja kwenye kisimamo changu cha mti kwa takribani dakika 20 kisha nikaamua kushuka chini ili kuukagua ule mshale. Hakika, nilimpiga dume, na niliona mkondo wa damu.

Nilipoufuata mkondo ule, nilitiwa moyo maana ulikuwa dhahiri. Lakini baada ya takriban yadi 100, mkondo wa damu ulikauka. Nilitazama na kutafuta lakini sikuweza kupata tone lingine. Baada ya masaa mawili ya kutafuta, niligundua kwamba dume alikuwa amekwenda. Nilikata tamaa sana. Kwanza, huwa sipendi kamwe kumjeruhi kulungu na kumpoteza; na pili, nilikatishwa tamaa na jinsi nilivyorusha mshale wangu.

Nikiwa nimesimama pale kwenye shamba la mahindi, nilianza kurudi nyumbani nikiwa na mawazo. *Bado nina nafasi. Ninaweza kupata kulungu ninaporudi nyumbani kupitia shamba la mahindi na kisha eneo la kinamasi.*

Niliandaa upinde wangu. Nilipokuwa nikitembea polepole kwenye korongo lililo kwenye shamba la mahindi, ghafla, kulungu aliruka na

kutoka mbele yangu. Bila kujua mimi ni nini, kulungu alisimama na kutazama nyuma. Kwa vile nilikuwa nimevaa mavazi ya kujisitiri, yule kulungu ambaye nilimona alikuwa dume, alisita maana hakuweza kujua mimi ni kitu gani. Yote yalitokea kwa sekunde moja. Niliona pembe, ingawa sikuweza kujua ukubwa wake au nambari yake.

Nilijua nilikuwa na sekunde moja ya kuamua kuhusu dume huyo. Alikuwa umbali ambao kwa kawaida mshale wangu haungefika, takriban yadi 55 kutoka kwangu na upande wake mmoja ulinitazama. Haraka nilimkaribia na kumlenga juu ya mgongo wake na kuuachilia ule mshale.

Dume alianguka mara moja mshale ulipomgonga na kubaki ndani yake. Nilishtuka kwa njia fulani. Je, hili limetokea hivi tu?

Nilipomkaribia dume, jambo la kwanza nililosema ni, "Imani ya Drenda!" Dume alikuwa mkubwa ajabu! Nilihesabu pembe 26, na nyingine ndogo iliyokuwa ikimea kuelekea chini. Sikuwa nimewahi kuona dume mkubwa kama huyo. Kweli, kusema nilifurahishwa ni kupuuza.

Umekisia vyema, dume sasa yuko juu ya meza yangu ofisini mwangu. Lakini nataka kuzungumza juu ya kulungu huyu kwa dakika moja. Vipi au kwa nini alijitokeza?

Kulungu mwenye pembe nne alijitokeza wakati uliofaa ingawa sikufyatua mshale vyema. Lakini Drenda alisema alikuwa anaamini kwa ajili ya dume wa kombe. Sasa, alikuwa na faida zaidi yangu. Yeye hawindi kulungu, na kwake, dume wa kombe anapaswa kuwa rahisi kuua kama mwenye pembe nne. Kwake wao ni kulungu tu. Kwa sababu yeye si mwindaji, hakuzungumziwa na picha ya kutowezekana. Sikuwa nimewahi kuona dume mkubwa mwenye pembe nane kwenye mali yetu, lakini imani yake haikutegemea kile kilichokuwa kwenye mali hiyo au kutokuwemo. Aliamini kwamba Mungu angeweza kumleta.

Uwindaji huu ulifanyika wakati wa msimu wa kuzaliana wa kulungu, na dume wanaweza kusafiri maili nyingi kutafuta kulungu wa kike. Kwa hivyo daima kuna uwezekano mzuri wa kuona kulungu ambao kwa kawaida huwaoni katika shamba lako wakati huo, kama ilivyokuwa hapa.

Imani ya Drenda ilileta dume huyo ingawa sikuwa na imani ya dume wa kombe.

Nataka usome hilo tena—Sikuwa na imani ya dume wa kombe!

Ninajua unachofikiria—*Subiri, Gary. Nimechanganyikiwa. Ikiwa hukuwa na imani ya kumpata dume huyo, kwa nini alijitokeza?*

Ndivyo ile mashua ya Yakobo na Yohana ilivyojazwa na imani ya Petro. Hiyo ndiyo nguvu ya ushirikiano.

Hebu nikupe mfano mmoja zaidi, kisha tuzungumze zaidi.

> *Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi. Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;*
>
> *Vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu na katika kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, <u>ninyi nyote mmeshirikiana nami neema hii.</u>*
>
> — Wafilipi 1:3-7

Paulo alisema alilikumbuka kanisa la Filipi kwa furaha kwa sababu ya kuendelea kushirikiana na huduma yake. Aliendelea kusema kwamba kwa sababu ya ushirikiano wao, sasa walishiriki neema ya Mungu iliyokuwa katika huduma yake.

Kumbuka tulisema kwamba neema ni uweza au uwezo wa Mungu uliokuwa juu ya Paulo kukamilisha kazi yake. Kanisa la Filipi lilikuwa likishiriki katika gharama ya kazi hiyo, na kama Yakobo na Yohana, walishiriki pia katika upako na neema iliyokuwa kwenye kazi hiyo.

Sasa hebu tuende kwa sura ya 4, na utaona matokeo ya kushangaza ambayo ushirikiano husababisha.

> *Lakini mlifanya vema, mliposhiriki nami katika dhiki yangu. Nanyi pia, ninyi wenyewe mnajua, enyi Wafilipi, ya kuwa katika mwanzo wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna kanisa lingine lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi peke yenu. Kwa kuwa hata huko Thesalonike mliniletea msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja. Si kwamba nakitamani kile kipawa, bali nayatamani mazao yanayozidi kuwa mengi, katika hesabu yenu. Lakini ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena nimejaa tele; nimepokea kwa mkono wa Epafrodito vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu. <u>Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.</u>*
>
> — Wafilipi 4:14-19

Paulo alikuwa amepokea matoleo mengine kutoka kwa kanisa la Filipi.

Sikiliza kile anacholijibu kanisa la Filipi, “Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji.”

Tazama kwamba Paulo hakusema, “Mungu wenu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa sababu mmekuwa wakarimu kwangu.” LA! Alisema, “Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji!”

Unajua, Wafilipi walikuwa washirika pamoja na Paulo, na kama washirika, walishiriki katika neema iliyokuwa juu ya kazi ya Paulo. Sasa, kama vile Yakobo na Yohana walivyovua samaki hao wote kwa sababu ya imani ya Petro, Paulo alitangaza kwamba mahitaji yao yangetimizwa kwa sababu ya imani yake!

Natumai unaweza kuona faida ya kanuni hii.

Hebu tuseme unahitaji gari na unashirikiana nasi kama huduma. Pia tuseme gari linagharimu $30,000. Sasa, unapotoa matoleo katika Garykeesee.com, unaelewa ushirikiano ni nini—unashiriki upako na neema kwenye huduma yetu.

Kama huduma, tunaweza kukubaliana nawe virahisi kuhusu matoleo hayo kwa sababu tulipita kiwango cha kuhitaji $30,000 zamani. Tunaweza kuwa na imani pamoja nawe virahisi kwa sababu kila mwaka tunatumia mamilioni ya dola. Lakini zamani nakumbuka ilinibidi kumwamini Mungu kupata dola 30,000, ambazo wakati huo zilionekana kama mlima mkubwa.

Kwa hiyo ukiniuliza ikiwa ninaweza kumwamini Mungu kupata dola 30,000, jibu litakuwa “Hakika.” Kwa hiyo kama Paulo, tunapokubaliana nawe kama mshirika, naweza kusema kwamba hitaji lako litatimizwa si kwa sababu ya imani *yako* bali *yangu*.

Sasa ni wazi kwamba unahitaji kuwa na imani unapopanda mbegu yako ya $30,000 kwa huduma yetu, unapaswa kuamini Neno la Mungu na kuniamini pia. Unapaswa kuniamini, kuwa na uhakika kwamba nimetiwa mafuta na nimeitwa na Mungu, kwamba ninafanya kazi kwa uadilifu, na unapaswa kuona *matokeo dhahiri* katika maisha yangu na katika huduma yangu. Ukiangalia tunachofanya na tulikotoka, utajua nina imani ya $30,000!

Huenda usiwe na imani ya $30,000, lakini tunaweza kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano na kuona mambo ambayo ni ya kushangaza. Ilikuwa vivyo hivyo na yule dume wa kombe. Drenda alisema jioni ile, “Unaamini kumpata kulungu, nami nitaamini kumpata dume wa kombe.” Hivi ndivyo ushirikiano unavyofanya kazi.

Kwa hivyo hebu nikuwekee sheria za kimsingi hapa kwa kukuuliza swali. Je, ikiwa unaanzisha kampuni ya kompyuta, ungetaka kijana aliye

katika muhula wake wa kwanza wa masomo ya sayansi ya kompyuta ambaye hana pesa awe mshirika wako au mtu ambaye ameunda biashara ya kompyuta yenye thamani ya mamilioni ya dola na ana fedha za kukusaidia kuzindua kampuni yako?

Kwa kweli, kuna anuwai nyingi hapa, lakini ninatoa kielelezo tu. Lakini nafikiri ni wazi kwamba utachagua mtu mwenye uzoefu, aliye na rekodi ya kuthibitishwa, na ambaye hatafilisika! Vile vile ni kweli unapotaka kupanda mbegu katika huduma fulani.

Tafadhali usichanganye ninachosema na uongozi wa moja kwa moja wa Mungu wa kushirikiana na mtu fulani. Uongozi wa aina hiyo ni wa kiwango kingine na hauhusu kile ninachozungumzia. Wakati mwingine Mungu anaweza kukuelekeza uwe mshirika katika kazi Yake, lakini kuna wakati utakuwa na fursa ya kuchagua ni ipi haswa. Ninazungumzia haswa kazi *unayoichagua* mwenyewe, wakati unapanda mbegu ili kwenda katika kiwango kingine.

Mimi hutoa matoleo kwa kazi ninazoamini kwa madhumuni ya kuharakisha pesa zinazohitajika maishani mwangu. Kanuni moja ambayo huwa sivunji ni kwamba mimi hutoa matoleo ya kila mara katika huduma inayoelewa imani na makubaliano ninapotaka kuharakisha mavuno yangu. Utoaji wa aina hii ni kutoa kuliko na lengo fulani na hakupaswi kuchanganywa na kutoa kwa maskini.

Kutoa matoleo kwa maskini ni moyo wa Mungu, na kuna mavuno ya hilo pia, lakini katika hili ninatafuta ushirikiano na kazi iliyo na ushahidi wa imani, ambayo najua ina uwezo wa kukubaliana nami.

Fikiria hivi: Ikiwa ningemwomba mtu asiye na pesa na hajakuwa na pesa kwa miaka mingi, na mapato yake ni $3 kwa saa, aungane nami katika imani ili nipate $10 milioni, kuna uwezekano gani kwamba makubaliano yenu yatakuwa halisi?

Ninaweza kumhudumia mtu yeyote, na nimeitwa kufanya hivyo, lakini inapohusu makubaliano katika imani, lazima kuwe na makubaliano. Mkulima hapandi mbegu zake kwenye shamba lenye uchafu. Anatafuta udongo unaofaa ambao mavuno yake yaliyokusudiwa yanahitaji. Ninazungumzia kushirikiana hapa katika ulimwengu na imani na upako wa mtu mwingine.

Jambo lingine ninalotafuta ninapopanda mbegu ni kupata huduma iliyo na matunda yale yale ambayo ninaamini kupata kutoka kwa Mungu.

Kwa mfano, kampuni yangu inamiliki ndege mbili. Kabla ya kuzinunua, nilipanda mbegu katika kazi ya Mungu, huduma ambayo

nilijua ilikuwa imelipia ndege nyingi mamilioni ya pesa hapo awali. Ninaposema nyingi namaanisha *nyingi*, na zote zililipwa kwa pesa taslimu. Walikuwa na matokeo dhahiri linapokuja suala la ndege. Nilijua wangeweza kukubaliana nami virahisi kuhusu ndege na kuwa na imani ili jambo hilo litimie. Sikutaka kushirikiana na huduma iliyosema kwamba ndege ni ghali sana au hazifai kumilikiwa. Hayo si makubaliano ya maana. La, nilitaka kukubaliana na huduma iliyoelewa mahali nilikuwa, huduma iliyoelewa imani yangu kuhusu kuamini Mungu kupata ndege, na kuwa na matunda ya kuthibitisha hilo.

Nimekuwa rubani tangu umri wa miaka 19 na nilijifunza kupeleka ndege kutoka kwa barabara ya changarawe yenye urefu wa futi 3,000 kule mashambani. Nilikuwa nimekodisha ndege maisha yangu yote hadi siku moja nilipowaza, *Wajua nini? Ninahitaji kupanda mbegu na kumwamini Mungu kupata ndege yangu mwenyewe.*

Hivyo ndivyo nilivyofanya. Nilijua ndege niliyoitaka kwa hivyo niliandika ndege hiyo kwenye hundi yangu, na mimi na Drenda tukakubaliana kuihusu. Kisha tukatuma hundi hiyo kwa huduma niliyoizungumzia hivi punde.

Karibu mwezi mmoja ulipita, na nilikuwa nimeenda kwa daktari kufanyiwa uchunguzi wa kawaida. Nilipokuwa nikizungumza na daktari siku hiyo, alisema, "Je, unamjua mtu yeyote ambaye angependa kununua ndege?"

Nilishangazwa kidogo na swali hilo kwa sababu katika maisha yangu hakuna mtu amewahi kuniuliza kuhusu kununua ndege. Kwa hiyo niliuliza ni ndege aina gani, na ilikuwa ndege haswa niliyokuwa nikiamini Mungu kupata.

Bila shaka hili lilikamata usikivu wangu. Nilikwenda nikaiona ndege, nikawasiliana na mmiliki, naye akaniendesha ndani yake. Ilikuwa nzuri sana. Kulikuwa na tatizo moja tu—wakati huo, sikuwa na pesa za kuilipia.

Lakini Mungu alikuwa na mpango. Katika msimu wa vuli uliotangulia, (sasa ilikuwa Machi), nilikuwa nimepokea jengo kutoka kwa babangu ambalo ningelikarabati na kulifanya ofisi katika msimu wa masika. Babangu aliniambia kwamba alikuwa amefunga mabomba ya maji kabla ya msimu wa baridi kali, kwa hiyo sikuyachunguza hata kidogo.

Siku chache tu baada ya kuona ile ndege, kakangu alinipigia simu na kusema kwamba jengo langu lilikuwa limeharibika. Kisha akaniambia kwamba mbao za kuta zote ndani ya jengo hilo zilikuwa zimeharibika na nyingi zao zilikuwa zimeanguka kutoka kwa ukuta.

Ilikuwa dhahiri kwamba mabomba ya maji hayakuwa yamefungwa na yalikuwa yameganda wakati wa baridi. Sasa kwa sababu ulikuwa mwezi wa Machi na joto lilikuwa limeongezeka, maji yalianza kumwagika ndani ya jengo na hakuna anayejua kwa muda gani, angalau wiki chache.

Kitu ambacho kakangu hakujua ni kwamba tayari nilikuwa nimefanya mkataba na kampuni ya ujenzi ambayo ingevua kuta zote na ubavu wa nje. Hii ilikuwa sehemu ya mchakato wa ujenzi upya wa kubadilisha jengo kuwa ofisi yangu mpya.

Sasa, hapa ndipo jambo la kupendeza lilipotokea. Kampuni ya bima ililipa madai ya uharibifu wa maji, na hizo ndizo pesa nilizotumia kulipia ndege yangu.

Niliilipia ndege pesa taslimu!

Kwa hivyo kumbuka, ushirikiano ni kanuni yenye nguvu ya kiroho ambayo unahitaji kuifahamu na kufaidika nayo.

## SURA YA 6

# SIRI YA ZAKA

Mara kwa mara mimi hupokea barua pepe kutoka kwa watu wanaojaribu kunishawishi kwamba sheria hii ya Ufalme—zaka—imepita na haitumiki tena.

Walakini nimegundua kwamba kanuni hii ya Ufalme ni muhimu sana kwa hivyo nimeweka wakfu sura nzima kuizungumzia.

Najua kwamba ikiwa umekuwa karibu na kanisa hata kidogo, umesikia kuhusu zaka. Lakini pia najua kwamba ulichosikia pengine si sahihi kabisa, na ni muhimu tusahihishe baadhi ya mawazo ya zamani ya kidini kuhusu zaka kabla hatujaendelea.

Kwanza kabisa, ikiwa hujui, maana halisi ya neno zaka ni sehemu ya kumi. Neno hili lilitumika kuelezea watu wa Mungu kiasi cha mapato yao ambayo walipaswa kutoa kwa kazi Yake, sehemu ya kumi, au zaka.

Sasa, maelezo haya kuhusu zaka ni rahisi sana, na ninataka kuzungumzia mada hii kwa undani zaidi katika sura hii. Lakini ikiwa dhana hii ni mpya kwako, kimsingi hii ndiyo maana ya zaka, kutoa sehemu ya kumi kwa Mungu.

Pili, watu wengi wanapofikiria kuhusu zaka huwa pia wanafikiria Agano la Kale na Sheria ya Musa ambapo zaka ilitakiwa kwa raia wote katika taifa la Israeli.

Leo, kuna utata mwingi katika mwili wa Kristo kuhusu maana ya zaka, na ikiwa ingali inatumika au ilipita Yesu alipokuja.

Labda umenisikia nikizungumza kuhusu wakati Mungu aliniambia nijifunze yote niwezayo kuhusu jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi, hakika nilifanyika mwanasayansi wa mambo ya kiroho. Nilitaka kuelewa jinsi kila kitu kinavyofanya kazi, na suala la zaka lilikuwa swali kubwa

ambalo nilipaswa kujibu.

Kwa hiyo, tuangalie zaka, ilitoka wapi, inafanya nini, na kwa nini ipo leo.

Ingawa kwa kweli tunaona sehemu ya kumi kama takwa muhimu sana lililoandikwa katika Sheria ya Musa, zaka haikuanza na Sheria ya Musa. Ili kuelewa asili yake, tunahitaji kurudi mwanzoni katika maisha ya Adamu na Hawa.

Kama nilivyotaja hapo awali, Adamu aliumbwa na kuwekwa duniani kama mtawala juu ya dunia kwa niaba ya Ufalme wa Mungu.

> *Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake. Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake.*
>
> — Waebrania 2:7-8a

Adamu alivikwa taji ya utukufu na heshima, na hapakuwa na kitu chochote duniani ambacho hakikuwa chini yake. Neno *taji* linatupa picha nzuri ya jinsi jambo hili lilivyofanya kazi.

Unapomtazama mfalme wa asili, amevaa taji, na, ingawa yeye ni mtu tu, taji hiyo inaonyesha kwamba serikali nzima inaunga mkono maneno yake. Ndivyo ilivyokuwa na Adamu. Alitawala dunia na mamlaka kamili, huku mbingu ikiunga mkono yote aliyoyafanya. Lazima tukumbuke kwamba alikuwa mtu tu na alitawala tu kupitia kwa mamlaka iliyokabidhiwa. Alikuwa na utukufu (nguvu) na heshima (cheo na mamlaka) na Ufalme wa Mungu ulimuunga mkono.

Tunaona kwamba Adamu alipoumbwa Shetani alikuwa duniani, maana tayari alikuwa ametupwa duniani awali. Shetani alimdharau kiumbe huyu wa hali ya chini (kiasili) aliyemtawala kwa niaba ya Ufalme wa Mungu. Alitaka kutafuta njia ya kuchukua mamlaka hayo kutoka kwa Adamu, kimsingi kubatilisha mamlaka ya Adamu ya kutawala.

Bila shaka, Shetani hakuwa na uwezo wa kudhoofisha au kupindua cheo cha Adamu, kwa hiyo ilimbidi aunde mpango wa kumdanganya Hawa ili aamini kwamba Mungu hawezi kutegemewa na kwamba yeye na Adamu walipaswa kumwasi Mungu na kumfuata.

Mpango wa Shetani ulifanikiwa. Adamu na Hawa walimwasi Mungu na kupoteza vyeo vyao vya mamlaka. Wakati huo, maana ulimwengu wote ulikuwa chini ya utawala wa Adamu, Adamu kimsingi alimfukuza Mungu

kutoka duniani ilipohusu mamlaka ya kiroho ya Mungu, na mwanadamu akatengwa na Mungu.

Mengi yalitokea kiroho wakati huo, lakini sina muda wa kuyazungumzia hapa kwa sababu ninataka kuzingatia mada yetu ya zaka. Kwa hiyo, turudi katika wakati ule Adamu na Hawa walipoasi na tuone kilichotukia.

> *Akamwambia Adamu, "Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi."*
>
> — Mwanzo 3:17-19

Kifupi tunaona kwamba mwanadamu alipoteza riziki yake (alifukuzwa bustanini), sasa kusudi lake likawa kuishi maisha ya unusuru, na alianza maisha ya taabu, uchungu na jasho. Mungu pia alimwambia kwamba angerudi ardhini, kwamba *angekufa* siku moja. Dhana za kifo na maisha ya unusuru na uchungu vilikuwa vitu vigeni kabisa kwa Adamu, na hofu na kutokuwa na tumaini viliingia ulimwenguni.

Kama unavyoona, na kama Adamu alivyogundua, ulimwengu ulikuwa umebadilika sana.

Sasa nataka kwenda katika Luka 4 ambapo tutapata mabadiliko mengine muhimu sana yaliyotukia.

> *Akampandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, "Nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako."*
>
> — Luka 4:5-7

Katika kifungu hiki, Shetani alidai kwamba fedha zote za falme za dunia (mataifa) zilikuwa chini ya mamlaka yake na kwamba mamlaka haya alipewa yeye. Na katika kauli hiyo alikuwa sahihi, maana Adamu ndiye aliyempa mamlaka katika kuasi kwake.

Tazama mstari huu unasema kwamba fahari zote za mataifa au enzi zote za ulimwengu zilikuwa chini ya mamlaka yake. Je, fahari ya taifa ni

nini? *Utajiri* wake.

Pesa zote ulimwenguni zina mhuri wa ufalme au taifa juu yake, kwa hiyo pesa zote ni sehemu ya au ziko chini ya mamlaka ya ufalme wa kidunia. Sasa Shetani alidai kwamba pesa, au mali, za mataifa zilikuwa chini ya mamlaka yake, na kwamba angeweza kumpa yeyote aliyetaka. Kifupi, Shetani alidai mamlaka juu ya utajiri na ufanisi wa mataifa. Hili ni muhimu sana maana tutagundua kwamba zaka ina kusudi maalum sana linalohusiana na ukweli huo.

> *Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, "Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana." Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili.*
>
> *Habili alikuwa mchunga kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi. Ikawa hatimaye Kaini akaleta* <u>*mazao*</u> *ya ardhi, sadaka kwa Bwana. Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na* <u>*sehemu zilizonona za wanyam*</u>*a. Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake; bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana.*
>
> *Bwana akamwambia Kaini, "Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana?* <u>*Kama ukitenda vyema*</u>*, hutapata kibali?*
>
> *Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde."*
>
> — Mwanzo 4:1-7

Sawa, ni kitu gani kilichotokea hapa? Hiki kilikuwa kizazi cha kwanza cha watoto. Kwa nini walikuwa wakitoa sadaka? Hakukuwa na sheria iliyoandikwa iliyohitaji wafanye hivyo wakati huo, kwa hivyo kwa nini walifanya hivyo?

Tunaweza kusema kwamba labda wazazi wao, Adamu na Hawa, *waliwafundisha* kutoa matoleo. Pia tunaweza kusema kwamba Mungu hafanyi mambo kwa ajili ya desturi tu kwamba lazima kulikuwa na sababu ya *kisheria* iliyowafanya Adamu na Hawa wawafundishe kutoa sadaka.

Unapotazama maandiko, utaona kwamba kulikuwa na tofauti kubwa katika matoleo ya vijana hawa wawili. Sasa, usijihusishe na kile walichopaswa kutoa, mmoja alitoa wanyama na mwingine mimea, hilo halikuwa suala. Suala lilikuwa *jinsi* walivyokuwa wakitoa kile walichokuwa nacho na kwa nini walikuwa wakifanya hivyo.

Kaini alitoa "baadhi" ya mazao ya udongo. Lakini Habili alileta

"sehemu nono kutoka kwa baadhi ya wazaliwa wa kwanza" wa kundi lake. Je, unaona tofauti? Mmoja alitoa "baadhi" na mwingine "sehemu bora," ambayo ilikuwa sehemu nono kutoka kwa wazaliwa wa kwanza wa kundi.

Kwa nini Habili alileta sehemu nono, na kwa nini kutoka kwa mzaliwa wa kwanza?

Lazima iwe kwamba Mungu tayari alikuwa amemwambia Adamu matakwa ya matoleo haya.

Je, unaliona hili? Hii ndiyo mara ya kwanza zaka ilionekana.

Ukisoma kuhusu zaka katika Sheria ya Musa, ilikuwa ni 10% ya **kwanza** iliyotolewa kutoka kwa kile kilichokuwa **bora**. Katika hadithi hii, tunaweza kuona wazi kwamba Habili alikuwa akitoa zaka, sehemu ya kwanza iliyokuwa bora kabisa. Hata hivyo, Kaini hakufurahia kuachilia sehemu ya kwanza ya mazao yake kumheshimu Mungu, kwa hivyo aliamua kuleta "baadhi" ya mazao yake, si sehemu bora zaidi.

Inaonekana Kaini alijua zaka ni nini na jinsi ya kuitoa kwa Bwana maana Mungu alimwambia, *"Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde."*

Lakini Kaini alikataa kitia-moyo cha Mungu cha kufanya yale aliyofundishwa na badala yake akamuua Habili, nduguye. Huenda alifikiri kwamba ikiwa Habili angeondolewa, angeweza kudhibiti shamba na mifugo, au uchoyo wake ulimshawishi kuleta tu baadhi ya mazao, na hivyo kutii huku moyo wake ukiwa mbali na Mungu. Ninakisia tu. Jambo moja tunalojua ni kwamba Kaini hakutaka kutoa zaka kama alivyofundishwa.

Kufikia hapa, unaweza kuuliza, "Kwa nini zaka? Mbona Mungu alitaka watoe zaka?" Nitajibu maswali hayo, lakini kwanza, hebu tuone ni kitu gani kingine tunachoweza kujifunza kuhusu zaka kabla ya kushughulikia maswali hayo.

Wakati uliofuata ambapo fungu la kumi lilionekana ndio mara ya kwanza neno zaka lilitumiwa.

> *Abramu aliporudi kutoka kumpiga Kedorlaoma na wale wafalme waliokuwa pamoja naye, mfalme wa Sodoma akatoka amlaki katika bonde la Shawe, (nalo ni Bonde la Mfalme). Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye juu sana. Akambariki, akasema, "Abramu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi. Ahimidiwe Mungu Aliye juu*

> *sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako." Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote.*
>
> — Mwanzo 14:17-20

Swali tunalohitaji kuuliza hapa ni: Je, Abramu alijuaje kutoa zaka na kwa nini?

Bila shaka zaka ilipitishwa kupitia kwa vizazi kutoka wakati wa Adamu. Na tunajua kwamba Adamu alifundishwa na Mungu Mwenyewe kuhusu zaka, baada ya kuasi. Hapa neno zaka limetumika kuonyesha sehemu ya kumi iliyotolewa.

Watu wengi wanaweza kusema kwamba zaka ilikuwa chini ya Sheria ya Musa, kumaanisha kwamba mwamini wa Agano Jipya hayuko chini ya hitaji la kutoa zaka. Matukio haya mawili niliyotaja kuhusu Kaini na Habili na kisha Ibrahimu, yanathibitisha kwamba zaka iliagizwa *kabla* ya Sheria ya Musa kuandikwa. Nakubali, zaka iliagizwa katika Sheria ya Musa, na taifa la Israeli lilitakiwa kutoa zaka. Lakini zaka ilikuwa kitu ambacho taifa la Israeli lilikuwa likifanya tayari wakati Musa alipojitokeza.

Basi kwa nini zaka iliandikwa katika Sheria ya Musa? Sheria ya Musa ilipoandikwa, ilipaswa kuongoza maisha yote ya taifa jipya la Israeli ambalo lilikuwa limetoka Misri. Mahitaji yote ya kisheria na ya kiutawala yalikuwa yamewekwa katika kanuni hizo za maadili ambazo watu wangeishi kwazo. Hivyo, zaka iliandikwa katika Sheria ya Musa ili kuhakikisha imehusishwa katika maisha ya taifa. Zaka ilikuwa muhimu sana hivi kwamba Mungu aliifanya iandikwe katika sheria ya taifa. Baada ya muda mfupi tutajua kwa nini Mungu alitaka kuhakikisha kwamba imehusishwa, lakini hebu kwanza tuangalie mifano michache zaidi kuhusu zaka.

> *Basi sasa, Bwana wa majeshi asema hivi, "Zitafakarini njia zenu. Mmepanda mbegu nyingi mkavuna kidogo; mnakula lakini hamshibi; mnakunywa lakini hamkujazwa na vinywaji; mnajivika nguo lakini hapana aonaye moto; na yeye apataye mshahara apata mshahara ili kuutia katika mfuko uliotoboka-toboka."*
>
> *Bwana wa majeshi asema hivi, "Zitafakarini njia zenu. Pandeni milimani, mkalete miti, mkaijenge nyumba; nami nitaifurahia, nami nitatukuzwa," asema Bwana. "Mlitazamia vingi, kumbe vikatokea vichache; tena mlipovileta nyumbani nikavipeperusha. Ni kwa sababu gani?" Asema Bwana wa majeshi. "Ni kwa sababu ya nyumba yangu inayokaa hali ya kuharibika, wakati ambapo ninyi mnakimbilia kila*

> *mtu nyumbani kwake. Basi, kwa ajili yenu mbingu zimezuiliwa zisitoe umande, nayo nchi imezuiliwa isitoe matunda yake. Nami nikaita wakati wa joto uje juu ya nchi, na juu ya milima, na juu ya nafaka, na juu ya divai mpya, na juu ya mafuta, na juu ya kila kitu itoacho nchi, na juu ya wanadamu, na juu ya wanyama, na juu ya kazi zote za mikono."*
>
> — Hagai 1:5-11

Katika kifungu hiki, nabii Hagai alilikemea taifa la Israeli kwa kutojenga upya hekalu mara waliporudi kutoka uhamishoni Babeli. Hawakuwa wakifanikiwa, walipungukiwa, mazao hayakuwa mazuri, na taifa zima lilikuwa likiteseka. Mungu aliliambia taifa hilo watafakari **njia zao** kwa uangalifu, akimaanisha kwamba kulikuwa na jambo fulani walilokuwa wakifanya au kutofanya ambalo lilisababisha ukosefu huo.

Mwenyezi Mungu alisema, "**Kwa ajili yenu** *mbingu zimezuiliwa zisitoe umande*." Alisema Ilibidi aachilie ukame kwa sababu ya kile **walichokuwa** wakifanya. Wote walikuwa wakijenga nyumba zao wenyewe na kuliacha hekalu la Mungu katika hali ya uharibifu. Hii inaashiria kwamba hawakuwa wakitoa zaka.

Tazama kwamba zaka ilipaswa kuletwa kwa Walawi—makuhani—na kutumika kwa ajili ya huduma ya hekalu. Maana zaka hazikuwa zikiletwa kwa Walawi, na hekalu halikuwa limejengwa, ilimbidi Mungu aondoe mkono Wake wa baraka kwa sababu ya kile walichokuwa wakifanya.

Hakikisha kwamba unaelewa kuwa haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba aondoe baraka Zake kutoka kwa taifa la Israeli. Hakuwa na la kufanya, maana lilikuwa suala la kisheria kuhusu zaka.

Tunapoendelea kusoma sura ya pili, inaonekana watu walikuwa wameanza kutii maneno ya nabii.

> *"Na sasa nawaomba, tafakarini; tangu siku hii na siku zilizopita; kabla halijatiwa bado jiwe juu ya jiwe katika nyumba ya Bwana; katika wakati huo wote, mtu alipofikia chungu ya vipimo ishirini, palikuwa na vipimo kumi tu; na mtu alipofikia shinikizo apate kuteka divai ya vyombo hamsini, palikuwa na divai ya vyombo ishirini tu. Naliwapiga kwa ukavu, na ukungu, na mvua ya mawe, katika kazi zote za mikono yenu; lakini hamkunielekea Mimi," asema Bwana. "Tafakarini, nawaomba; tangu siku hii ya leo na siku zijazo; tangu siku ya ishirini na nne ya mwezi wa kenda, naam, tangu siku hiyo ulipowekwa msingi wa hekalu la Bwana tafakarini haya. Je! Mbegu ingali ghalani? Naam, huo mzabibu,*

> *wala mtini, wala mkomamanga, wala mzeituni, haikuzaa kitu; tangu siku hii ya leo nitawabariki."*
>
> — Hagai 2:15-19

Maana walitanguliza hekalu tena, Mungu aliwaambia wakumbuke siku na saa kwa sababu wangeona ongezeko kubwa katika ufanisi wao. Alitaka wakumbuke mabadiliko hayo ili wajitie moyo kutoacha kutoa zaka tena, si kwa faida yake bali kwa faida yao wenyewe.

Kuna kweli muhimu hapa ambazo utaelewa baada ya muda mfupi, lakini jambo la kwanza nataka utambue ni kwamba zaka ni suala la *kisheria. Ilimbidi* Mungu aondoe mkono Wake wakati hawakutoa zaka, si kwa sababu *alitaka* bali kwa sababu *ilimpasa*.

> *"Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu; ndio maana ninyi hamkuangamizwa, enyi wana wa Yakobo. Tokea siku za baba zenu mmegeuka upande, mkayaacha maagizo yangu, wala hamkuyashika. Nirudieni Mimi, nami nitawarudia ninyi," asema Bwana wa majeshi.*
>
> *"Lakini ninyi mwasema, 'Turudi kwa namna gani?'" "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, 'Tumekuibia kwa namna gani?'"*
>
> *"Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia Mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo," asema Bwana wa majeshi, "mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba," asema Bwana wa majeshi. "Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana," asema Bwana wa majeshi.*
>
> — Malaki 3:6-12

Hapa tunamwona nabii tofauti akilikemea taifa, akisema kwamba wamemnyang'anya Mungu uwezo Wake wa kuwabariki. Alisema wao—taifa zima—walikuwa chini ya laana kwa sababu ya *kutofanya* kile walichohitajika kufanya. Waliagizwa kuleta zaka yote ghalani, ili kuwe na chakula katika nyumba ya Mungu.

Tena, zaka ilipaswa kuletwa kwa Walawi, yaani makuhani. Watu

walikuwa wakileta kiasi fulani lakini si zaka nzima (kumbuka dhambi ya Kaini). Bwana aliwaambia watu ikiwa wangeleta zaka nzima kwamba baraka za mbinguni zingekuwa zao tena. Mbingu zingepata mamlaka ya kisheria ya kuingia katikati yao. Mungu aliwaambia kwamba ikiwa wangerudi Kwake na zaka, basi wangebarikiwa isiwepo na nafasi ya kutosha kupokea.

Sasa tukome hapo na tuzungumzie jambo hili kwa dakika moja kabla sijaenda mbele zaidi.

Kufikia sasa, tumeona kwa udhahiri kwamba zaka ilianza hapo mwanzo, na tumeweza kuona kwa nini. Tumeona kwamba zaka humpa Mungu mamlaka ya kisheria ya kuingilia kati kati ya mlaji, Shetani, na watu wa Mungu na kumkemea Shetani.

Kimsingi, Mungu alikuwa akisema, “Ondoa mikono yako, Shetani! Huwezi kugusa vitu vyao!”

Unajua, Adamu alipoasi, Shetani angalipenda tu kumtoa kabisa ulimwenguni kupitia kwa ukosefu. Lakini, mara moja, Mungu aliweka zaka ili kuwahifadhi Adamu na Hawa. Adamu na Hawa walipochagua kutoa zaka, walikuwa wakimtanguliza Mungu. Walikuwa wanamchagua Mungu.

**ZAKA ILIWEKWA ILI KUWA KAMA UZIO WA KISHERIA ULIOWAZUNGUKA ADAMU NA HAWA WAKATI HUO, NA INGALI NGAO YA KISHERIA INAYOTUZUNGUKA LEO.**

Hebu tukumbuke kwamba Shetani aliingia duniani kwa njia iyo hiyo. Kwa kuwasadikisha Adamu na Hawa kumwamini badala ya Mungu, alipata mlango wa kisheria. Hivyo kutoa zaka—kumpa Mungu 10% ya kile walichokuwa nacho—kulimpa Mungu haki ya kisheria ya kulinda riziki ya Adamu na Hawa.

Tunahitaji kukumbuka kwamba zaka ilikuwa sheria iliyohusu tu riziki ya mwanadamu duniani katika milki ya Shetani. Haikubadilisha hali yao kuhusu urejesho wa kiroho. La, dhabihu ya dhambi ilipaswa kutolewa kwanza kabla hilo halijatokea. Lakini sehemu ya kumi ilimruhusu Mungu kumzuia Shetani asiibe chakula kutoka kwao, na kuwawezesha kuishi duniani.

Watu wengi husema kwamba zaka ni sheria ya Agano la Kale na imepitwa na wakati, kwamba imetimizwa kupitia kwa dhabihu ya Yesu. Lakini tumeona wazi kwamba sheria ya zaka ilianzishwa mwanzoni wakati mwanadamu aliasi, kabla ya Sheria ya Musa kuandikwa.

**Zaka iliwekwa ili kuwa kama uzio wa kisheria uliowazunguka**

**Adamu na Hawa wakati huo, na ingali ngao ya kisheria inayotuzunguka leo.**

Zaka ni sheria ya ulimwengu na inabakia kutumika maadamu Shetani yuko huru duniani, kama alivyo sasa. Maadamu Shetani yuko hapa, sheria ya zaka ingali inafanya kazi.

Kitu kingine unachoweza kuona kanisani ni watu wanaotoa zaka na bado hawafanikiwi. Hii ni kwa sababu ya mafundisho mapotovu kuhusu zaka. Watu hufikiri ikiwa watatoa zaka, baraka za Bwana zitawafanya kufurahia ufanisi unaofurika, zaidi ya uwezo wao wa kupokea. Wanapoanza kutoa zaka na kukosa kuona ufanisi wao ukifurika, wanahitimisha kwamba zaka haifanyi kazi. Lakini dhana yao si sahihi, na tunahitaji kuangalia kwa makini maandiko ili kujua kwa nini.

Mungu aliwaambia watu kwamba ikiwa wangetoa zaka, "*Nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu* ***mazao ya ardhi yenu;*** *wala* ***mzabibu wenu*** *hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba*,"

Je, unaona hili? Inasema kwamba madirisha ya mbinguni yatafunguliwa na Mungu atabariki mazao *yao*. Hoja ninayotoa ni kwamba ungali *unapaswa* kukuza kitu ndani ya uzio wako wa zaka.

Zaka peke yake haiwezi kukufanya ufanikiwe. Inalinda tu kile unachofanya ndani ya uzio wako.

Kwa hivyo ikiwa una mimea mitatu ya nyanya, itafanikiwa. Lakini ikiwa yote uliyo nayo ni mimea mitatu ya nyanya, utakuwa na mimea mitatu mikubwa, lakini hautastawi sana.

Ni kile *wewe* unachojenga au kukuza ndani ya uzio wako kinachokufanya ufurike na utele.

Cha kusikitisha ni kwamba, kupitia kwa mafundisho yasiyo sahihi, watu wengi wa Mungu hutoa zaka na kisha kukaa chini na kikombe cha chai na kungojea mwanzo wa kufurika kwa utele. Kufurika kutaanza tutakapoelewa sehemu yetu katika mchakato huu.

Kwa hivyo tena, hebu tujikumbushe.

1. Zaka ilianzishwa duniani mwanzoni, mwanadamu alipoasi.
2. Iliandikwa katika Sheria ya Musa kwa sababu Sheria ya Musa iliamuru jinsi taifa la Israeli lilivyopaswa kuishi. Mungu katika kutaka kuwa na uhakika kwamba angeweza kuendelea kuwabariki, aliiandika katika sheria hiyo ili kuhakikisha iendelee. Sheria ya zaka haijapita. Lakini hitaji la kisheria la kutoa zaka limepita. Sasa, tuna *chaguo* la kutoa zaka na kunyakua faida yake.
3. Sheria ya zaka ni sheria ya ulimwengu na itabaki maadamu Shetani

yuko huru.

4. Zaka haikufanyi ufanikiwe moja kwa moja, bali humruhusu Mungu kumzuia Shetani asiingilie kile unachokuza au kujenga ndani ya uzio wako wa zaka.
5. Zaka haitakuzuia kwenda mbinguni. Utaenda mbinguni ukiliitia jina la Yesu. Lakini zaka huathiri ustawi wako hapa duniani.
6. Zaka ni mali ya ghala ya Mungu. Katika Agano la Kale, ilitumika kuwalisha na kuwatunza makuhani waliofanya kazi katika huduma. Sio tofauti leo. Zaka inapaswa kutolewa kwa kanisa lako la mtaani. Mungu ameweka fungu la kumi kutunza huduma.

   Nina watu wanaoniambia hawapendi kanisa lao na huwa wananiuliza ikiwa ni lazima watoe zaka huko. Jibu langu? Tafuta kanisa jipya, linalofundisha imani na Ufalme.

   Ikiwa uko katika mchakato wa kutafuta kanisa, au unaishi katika eneo lisilo na kanisa linalokufaa, unaweza kutoa zaka kwa huduma inayokuhudumia kiroho, lakini kuwa katika kanisa zuri la mtaa ndilo jambo bora zaidi kwa Mungu.
7. Hutamki chochote unapotoa zaka yako. Kwa mfano, huwezi kusema, “Ninapanda zaka yangu kama mbegu kwa ajili ya ________.” Zaka tayari ina kazi yake. Unaweza kunena jambo fulani unapotoa matoleo lakini sio zaka.
8. Zaka ni 10% ya mapato yako. Hii ni *kabla* ya kulipa ushuru. Kumbuka, Mungu alisema kupitia kwa Malaki, “Leteni zaka yote ghalani.” Asilimia tisa sio zaka. Asilimia sita sio zaka. Zaka ni 10%. Ukisema, “Sina uwezo wa kulipa hiyo 10%,” fanya kile Mungu alichokuwa akiwaambia Waisraeli wafanye walipokosa kuleta zaka nzima: “Nijaribuni katika hili,” alisema. Toa zaka yako kwa imani, ukijua kwamba Mungu ataiheshimu.
9. Nitajuaje kile ninachopaswa kutolea zaka? Kanuni yangu muhimu ni hii: Je! Mapato hayo yanastahili kutozwa ushuru?
10. Ikiwa yanastahili kutozwa ushuru, basi ninayatolea zaka. Na, je, biashara yangu? Tena, inatozwa ushuru? Sitoi zaka kwa mapato ya jumla ya biashara yangu. Huwa ninatoa matoleo kutoka kwa biashara yangu jinsi ninavyotaka, lakini hiyo sio zaka. Wakati wowote ninapoondoa pesa kwenye biashara yangu, huwa ninatoa zaka kulingana na pesa ambazo nimeondoa.
11. Je, ikiwa sina kanisa wakati huu? Unaweza kutoa zaka kwa yule anayekuhudumia kiroho hadi upate kanisa. Ndio, watu wengi

> huchagua kanisa lililo mbali kuwa kanisa lao la nyumbani kupitia kwa utiririshaji wa moja kwa moja wa kisasa na matangazo ya moja kwa moja ya Facebook. Ikiwa hakuna kanisa zuri linaloamini Biblia katika mji wako, unaweza kutoa zaka kwa kanisa lililo mbali. Watu wengi katika maeneo ya mashambani wamefanya Faithlifechurch.org kuwa kanisa lao la nyumbani kwa sababu ya jambo hilo hilo.

Sawa, tuendelee.

Bwana alinionyesha kwamba Wakristo wengi hutoa zaka zao kama bili wanayowia (ikiwa huwa wanatoa zaka, na wengi huwa hawatoi). Hii inamaanisha kwamba hawana imani katika kile wanachofanya lakini wanajua tu kwamba wana bili ya zaka na wanailipa kama bili.

Ingawa ni vyema kulipa zaka yako, daima unapaswa kulipa zaka yako kwa imani. Vinginevyo, utoaji wako unachochewa na mtazamo wa kisheria badala ya imani.

Hebu kila neno kutoka kwa Mungu liwe ufunuo kwako wa nia ya Mungu kukuhusu. Zaka si mzigo mzito kubeba, na hupaswi kuwa na huzuni unapoitoa. Mungu hajaribu *kuchukua* kitu kutoka kwako, bali *kukupa* kitu. Tunapaswa kuamini na kuelewa faida ya zaka na kuifurahia. Zaka ni ibada inayotangaza kwamba Mungu ndiye chanzo chetu. Ina faida zilizoainishwa vizuri kwamba, tunapotoa zaka, tunapaswa kuwa katika imani kupokea.

Kila mara huwa ninapendekeza familia kujiandaa kutoka nyumbani siku zinapoleta zaka kanisani. Pia napendekeza kwamba, kabla ya kuja kanisani, waweke mikono yao juu ya zaka hiyo, watangaze manufaa yake, na watangaze kwamba madirisha ya mbinguni yamefunguliwa na kwamba Shetani amekemewa kutoka kwa mavuno yao. Wanapaswa pia kutangaza kwamba Shetani hawezi kuwaibia na kile wanachoweka mikono yao kitafanikiwa, kwa jina la Yesu.

Sasa, katika kumalizia hebu nizungumzie kuhusu zaka jinsi ilivyoandikwa katika Agano Jipya. Oh, ndio, zaka imetajwa hapo! Kifungu kifuatacho ndicho tulisoma hapo awali.

> *Abramu aliporudi kutoka kumpiga Kedorlaoma na wale wafalme waliokuwa pamoja naye, mfalme wa Sodoma akatoka amlaki katika bonde la Shawe, (nalo ni Bonde la Mfalme). Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye juu sana. Akambariki, akasema, "Abramu na abarikiwe na Mungu*

> *Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi. Ahimidiwe Mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako."* <u>*Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote*</u>*.*
>
> — Mwanzo 14:17-20

Sasa, hebu tuone kile ambacho mwandishi wa Waebrania anasema kuhusu zaka.

> *Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki; ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; (tafsiri ya jina Lake kwanza ni "mfalme wa haki," tena, "mfalme wa Salemu," maana yake, "mfalme wa amani;" hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku Zake, wala mwisho wa uhai Wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele.*
>
> *Basi, angalieni jinsi mtu huyo alivyokuwa mkuu, ambaye Ibrahimu, baba yetu mkuu, alimpa sehemu ya kumi ya nyara. Na katika wana wa Lawi nao, wale waupatao ukuhani, wana amri kutwaa sehemu ya kumi kwa watu wao, yaani, ndugu zao, kwa agizo la sheria, ijapokuwa wametoka katika viuno vya Ibrahimu. Bali Yeye, ambaye uzazi Wake haukuhesabiwa kuwa umetoka kwa hao, alitwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimu, akambariki Yeye aliye na ile ahadi. Wala haikanushiki kabisa kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa. Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi; bali huko Yeye ashuhudiwaye kwamba Yu hai.*
>
> — Waebrania 7:1-8

Tafadhali ona kwamba andiko hili linasema, "*Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi,*" ikimaanisha Walawi wa Agano la Kale. Kisha linaendelea kusema, "*bali huko* <u>***Yeye ashuhudiwaye kwamba Yu hai.***</u>"

Melkizedeki alikuwa mfalme wa haki, mfalme wa amani, asiye na mama wala baba, asiye na mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa maisha Yake, aliyefanana na Mwana wa Mungu, kuhani hata milele. Melkizedeki aliyesimama mbele ya Ibrahimu siku ile ni Yesu Kristo. Hata hivyo, hakujulikana kama Yesu wakati huo.

Kumbuka, Yusufu aliambiwa na malaika amwite mtoto wa kiume

atakayezaliwa Yesu. Jina Yesu maana yake ni Mwokozi, hivyo kuonyesha angekuwa nini kwetu. Kristo sio jina la pili la Yesu. Tunaposema Yesu Kristo, tunamwita Mwokozi aliyetiwa mafuta. Yesu hakujulikana kwa jina hilo aliposimama mbele ya Ibrahimu, kwa sababu mpango huo ulikuwa bado umefichwa kutoka kwa Shetani wakati huo.

Kwa hiyo, jina Melkizedeki lilikuwa jina lililoonyesha Yeye alikuwa nani, Mfalme wa Haki na Mfalme wa Amani. Hata hivyo, kiunabii, Melkizedeki alikuwa akitangaza wakati ujao wa Ibrahimu kwa kumpa mkate na divai, jambo ambalo lilizungumzia agano jipya (mkate, mwili Wake uliovunjwa kwa ajili yetu, na divai, damu Yake iliyotolewa kwa ajili yetu) ambalo lingefanywa na warithi wa Ibrahimu baadaye kutimiza ahadi ambayo Mungu alimpa Ibrahimu kuhusu warithi wake katika Mwanzo 12.

Kuhusu zaka, Waebrania inasema zaka sasa hupokelewa na "Yeye ashuhudiwaye kuwa hai." Ni Yesu sasa anayepokea zaka, Yeye anayetangazwa kuwa hai! Yeye ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Kwa hiyo, kumbuka, sheria ya zaka ingali inatumika leo. Kitu pekee ambacho kimebadilika ni ukuhani. Katika Agano la Kale, kabila la Lawi lilipokea zaka kwa ajili ya kazi ya Mungu. Leo, Yesu (aliyetoka kabila la Yuda, si Lawi, jambo linaloonyesha mwanzo wa utaratibu mpya wa ukuhani) hukupokea zaka kutoka kwa kanisa Lake kwa ajili ya kazi ya huduma. Bila shaka, ninatambua kwamba Yesu mwenyewe, hayuko hapa kibinafsi kupokea zaka. Lakini kumbuka kwamba Biblia inasema kanisa ni mwili wa Kristo, kumaanisha ni wawakilishi Wake hapa kisheria, kama vile miili yetu inavyotuwakilisha hapa kisheria. Tunapotoa kwa kanisa Lake, mwili Wake, hakika tunamtolea Yesu. Walawi, chini ya agano la kale, walipokea zaka kwa niaba ya huduma ya Mungu wakati huo, na sasa kanisa hupokea zaka kwa niaba ya huduma ya Mungu.

**ZAKA NI UZIO WA KISHERIA UNAOZUNGUKA MAISHA YAKO KUMZUIA SHETANI ASIPATE FURSA YA KUIBA RIZIKI YAKO.**

Kumbuka, zaka ni uzio wa kisheria unaozunguka maisha yako kumzuia shetani asipate fursa ya kuiba riziki yako. Kumbuka, zaka peke yake haikusababishi kufanikiwa! Ustawi wako huamuliwa na kile unachofanya *ndani* ya uzio huo!

Zaka ni sheria muhimu katika maisha yako ya kifedha. Hii ndiyo sababu nilichukua muda mwingi kuzungumzia sheria hii muhimu ya Ufalme.

Kwa hiyo, wakati mwingine utakapokuwa kanisani na mchungaji akasema ni wakati wa kupokea zaka, unapaswa kupiga kelele kwa furaha, kwa sababu sasa unajua faida za zaka.

SURA YA 7

# UNAHITAJI MKOBA WA FEDHA: SEHEMU YA KWANZA

Mmoja wa marafiki zangu wa karibu zaidi, Mchungaji Peter Mortlock, ni mchungaji katika Kanisa la City Impact huko Auckland, New Zealand. Amejenga huduma ya ajabu na ana moja ya makanisa makubwa zaidi huko New Zealand.

Katika urafiki wetu kwa miaka mingi, labda tumefanya safari 20 au zaidi kwa pikipiki kote Amerika Kaskazini na New Zealand. Yeye ndiye ambaye hatimaye alinifanya ninunue pikipiki aina ya Harley. Nilikuwa ninapenda pikipiki aina ya Honda kwa miaka mingi, lakini tuliposafiri, kila mara alisisitiza nikodishe pikipiki aina ya Harley. Mwanzoni, sikupenda pikipiki hiyo kama nilivyopenda Honda yangu, lakini ikiwa unajua mengi kuhusu pikipiki aina ya Harley, walifanya mabadiliko makubwa katika muundo wake miaka michache iliyopita, ambayo nilipenda. Kwa hivyo, mwaka huu uliopita, Drenda alininunulia pikipiki aina ya Harley mpya kabisa ambayo tunapenda kusafiri nayo.

Wakati wa safari zetu, kila mara niliona kwamba Mchungaji Peter alikuwa na mkoba wa ngozi—niliuita mkoba wa kiume—ulioning'inia kwenye mabega yake. Siku moja baada ya kuumizwa kwa kukalia mfuko wangu wa fedha, nilimuuliza kuhusu mkoba wake. Naam, mazungumzo hayo yalimfanya aninunulie mkoba huo kama zawadi ya siku yangu ya kuzaliwa. Haupendwi sana hapa Marekani kama kule Ulaya na New

Zealand, lakini ninaupenda.

Kwa kawaida kila mara nilikuwa nikipoteza miwani yangu ya kuzuia mwanga wa jua kwa kuiweka mahali fulani na kusahau mahali nilipoiacha. Lakini tangu nianze kuutumia sijawahi kupoteza miwani yangu. Sasa ninaelewa kwa nini wanawake wanapenda kubeba mikoba. Kila kitu kimo humo. Ni ajabu kweli. Sijaribu kukushawishi ununue mkoba wa kiume, lakini nataka kupendekeza ufikirie juu yake.

Je, unajua kwamba Yesu alituambia tubebe mkoba?

> *Ninyi msitafute mtakavyokula wala mtakavyokunywa; wala msifanye wasiwasi, kwa maana, hayo yote ndiyo watafutayo mataifa ya duniani, lakini Baba yenu anajua ya kuwa mna haja na hayo. Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa.*
>
> *Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na mioyo yenu.*
>
> — Luka 12:29-34

Sifikiri kwamba Yesu alikuwa akipendekeza mtindo fulani, bali mchakato ambao unahitaji kuelewa. (Na tunaweza kuuita pochi badala ya mkoba ikiwa unataka.)

Jambo ambalo Yesu alikuwa akimaanisha ni kwamba unahitaji mahali unaweza kufikia hazina yako.

Kwa mfano, ninaweza kuwa na dola milioni moja katika benki, lakini hazinifai kitu ikiwa siwezi kuzipata na kuzitumia, sivyo? Hii ndiyo sababu unapaswa kubeba mkoba wako karibu nawe—ni mahali unaweza kufikia mali yako.

Moja ya mambo yenye usumbufu yanayoweza kutokea ni kupoteza mkoba wako. Mimi hujitahidi kila niwezavyo kuhakikisha hilo halifanyiki. Pochi langu, ambalo mimi huweka ndani ya mkoba wangu wa kiume, huwa nami kila wakati.

Maneno haya machache ya Yesu ambayo nimenukuu yana hekima nyingi na kanuni kuu za Ufalme kuhusu pesa zako katika Ufalme. Kwanza kabisa, maneno “Msifanye wasiwasi” yametumiwa zaidi ya mara moja. Yesu alituambia kwamba Mungu anajua mahitaji yetu yote na akatoa mwelekeo maalum wa jinsi ya kupata riziki Yake.

*Ninyi msitafute mtakavyokula wala mtakavyokunywa; wala msifanye wasiwasi, kwa maana, hayo yote ndiyo watafutayo mataifa ya duniani, lakini Baba yenu anajua ya kuwa mna haja na hayo. Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa.*

Yesu alikuwa akisema tusiwe na wasiwasi kwa sababu Mungu tayari ameshughulikia jambo hili; Mungu anajua unachohitaji. Lakini Yesu aliingiza maagizo fulani.

*Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa.*

Yesu alikuwa akisema kwamba Mungu ana jibu, lakini kuna mchakato wa kuweka madai kisheria. Mungu analo jibu, LAKINI unahitaji kujua jinsi Ufalme unavyofanya kazi kabla ya kuweka madai.

Tazama kwamba Yesu hakusema tumtafute Mungu kwanza bali *Ufalme*. Nafikiri wengi wetu tumefasiri Maandiko hayo kuwa na maana ya kumtafuta Mungu kwanza, lakini hayasemi hivyo. Yesu aliweka wazi kabisa. Ikiwa kumtafuta Mungu tu ndio jibu, angesema, "Bali mtafuteni Mungu, na hayo yote mtaongezewa." Mungu anajua unachohitaji, lakini kuna mchakato wa kisheria ambao lazima ufanyike kabla ya kile kilicho mbinguni kuletwa kwako kihalali hapa duniani.

Hebu nikukumbushe kwamba Ufalme wa Mungu ni serikali iliyo na Mfalme. Mamlaka na mapenzi ya Mfalme yanatekelezwa kwa kila raia wa Ufalme kupitia kwa utekelezaji wa sheria za Ufalme.

Katika vitabu vyangu vinne vilivyotangulia juu ya Ufalme, nilizingatia masuala ya maisha katika Ufalme, imani, na mamlaka. Kwa nini? Kwa sababu kanuni hizi ni muhimu sana kwa mafanikio yako na uelewaji wako wa maisha katika Ufalme. Nimezungumzia viungo hivi muhimu vya Ufalme katika vitabu vyangu vyote, nikijua kwamba wengi wanaweza kusoma kitabu chochote na wanahitaji kuwa na ujuzi wa kimsingi wa kile ambacho hakika kilibadilisha maisha yangu.

Unahitaji kujifunza jinsi Ufalme unavyofanya kazi!

Taarifa katika sura hii zimetolewa kutoka kwa vitabu vyangu vingine katika mfululizo wa Mapinduzi Yako ya Fedha. Ikiwa umevisoma, uko huru kuendelea na kusoma sura ya nane. Ikiwa hujavisoma, au unataka kusoma tena kanuni hizi za kimsingi na muhimu za Ufalme, kaa hapa pamoja nami katika sura ya saba.

## Suala la mamlaka

Kama nilivyosema awali, ninaishi mashambani kwenye ekari 60 zenye ardhi ya kupendeza sana huko Ohio. Hapo awali nilikuwa na ekari 55, lakini jirani yangu aliniuzia kipande cha shamba lililopakana na langu, jambo ambalo lilinisababisha kuwa na jumla ya ekari 60. Hakika tumefurahia shamba hili kwa miaka 22 iliyopita. Kuwa na msitu wa kuwinda kulungu, bwawa la kuwinda bata, na shamba la kuwinda sungura na ndege, na pia kuendesha magari yetu humo ni baraka.

Ukiangalia mali yangu kwa ukaribu, utaona kwenye uzio la shamba alama zinazosema HAKUNA KUINGIA. Alama zipo ili watu wajue ni wapi mstari wa mali yangu unapoanzia. Sheria katika Ohio inasema kwamba yeyote anayetaka kuingia katika shamba langu lazima awe na fomu ya kibali wakati wowote aingiapo. Asipofanya hivyo, hilo linaitwa kuingilia mali, na anaweza kuondolewa kisheria, kuadhibiwa na kulipa faini katika mchakato huo.

Kwa hivyo kwa ufupi…

**Huwezi kumiliki kitu usicho na mamlaka juu yake kisheria.**

Kwa hivyo kama nilivyosema, kuwa na fomu ya kibali, iliyotiwa saini na mimi, itakupa ruhusa kisheria kuingia katika shamba langu. Mtu akikusimamisha shambani mwangu na kukuuliza unafanya nini humo na umjibu kwamba nilikupa ruhusa kuwinda huko, hiyo haitoshi. Sheria inasema kwamba lazima uwe na fomu iliyotiwa saini ili kupata kiingilio.

**JIFUNZE KILICHO CHAKO NA JINSI YA KUKIFIKIA. KISHA VITU HIVI VYOTE UNAVYOHITAJI VITAONGEZWA KWAKO.**

Mchakato huu huu unahitajika unapoenda kwa benki kudai pesa zako; watataka kuona kitambulisho chako. Karani wa duka ana haki sawa ya kuomba kitambulisho chako unapotumia kadi ya mkopo kulipia bidhaa. Uwasilishaji wa kitambulisho haukusudiwi kukuzuia usitoe pesa kwa akaunti zako; ni kukulinda dhidi ya wengine wasije wakatoa pesa zako kwa njia ya ulaghai.

Yesu aliposema tutafute kwanza Ufalme, alikuwa akisema, "*Jifunze sheria za Ufalme ili kujua jinsi ya kufanya kazi kisheria na kwa ufanisi ndani ya haki zako za kisheria kama raia wa Ufalme*." Jifunze kilicho chako na jinsi ya kukifikia. Kisha vitu hivi vyote unavyohitaji vitaongezwa kwako.

Mfano mwingine ni kwamba ikiwa nimewekeza hazina ya uaminifu kwa ajili ya mwanangu. Akifika umri halali wa kumhamishia akaunti

hiyo, itabidi nimwambie ni benki gani, na kumwonyesha jinsi ya kutoa na kuweka pesa katika akaunti hiyo. Ingawa ni akaunti yake kisheria, lazima awajibike kwa mchakato wa kisheria wa kuitumia.

Hebu nifanye muhtasari wa kile ninachosema hapa. Yesu aliposema tutafute Ufalme, alikuwa akisema tujifunze jinsi Ufalme unavyofanya kazi, akimaanisha sheria na taratibu katika Ufalme ambazo lazima tujifunze ili kunyakua kile kilicho chetu tayari. Kwa hivyo kama tulivyoona katika mfano kuhusu akaunti ya benki, unaweza kuwa na mamlaka ya kisheria juu ya mali fulani lakini usiimiliki kwa sababu haukufuata mchakato wa kisheria unaohitajika. Kwa mfano, ukiacha kitambulisho chako nyumbani unapoenda kwa benki, hawatakuruhusu kuchukua pesa kutoka kwa akaunti ingawa ni pesa zako.

Kuelewa suala la mamlaka katika Ufalme ni sharti la kufanya kazi kwa ufanisi katika Ufalme.

Nina hakika labda umesikia hadithi kama hii. Mtu mashuhuri anaugua sana, na watu wanaambiwa wamwombee. Mamilioni ya watu wanajiunga katika maombi kwa ajili ya uponyaji wa mtu huyu, na bado mtu huyu anakufa. Kwa nini?

Au mtu anakuambia bibi yake alifariki japo walikuwa wakimuombea, na anataka kujua kwa nini. Au mtu anakuambia kwamba ametoa matoleo kwa sababu ya hitaji la kifedha, na bado anaendelea kuwa na ukosefu. Je, kuna majibu kwa maswali kama haya?

Kabla sijajibu hilo, hebu tukubali kwamba hatujui kila kitu kinachofanyika katika ulimwengu wa Roho, na sijifanyi kwamba ninajua. Hata hivyo, kwa kutegemea Neno la Mungu, tunajua kwamba ikiwa mtu fulani alikuwa mgonjwa, Yesu alilipa gharama ya uponyaji wao. Tunajua kwamba tukiwa wakarimu na kutoa, Biblia inasema tutapokea. Hata hivyo kila siku, tunaona kile kinachoonekana kama kushindwa dhahiri kwa Maandiko katika maisha ya watu wengi. Je, ni Mungu anayepaswa kulaumiwa?

Ninapozungumzia mada hii katika sura hii, utapata jibu ni LA HASHA! Ikiwa ni la, basi shida ni nini? Maana watu wengi humlaumu Mungu kuhusu misiba. Wanajua ana uwezo wa kuzuia mambo mabaya yasitokee lakini hafanyi hivyo, kwa hiyo wanafikiri kwamba *alichagua* hilo. Hapa ndipo yanapotoka mafundisho potovu yanayosema "Mungu huruhusu mambo mabaya yawapate watu wema." Watu wanaamini kwamba ikiwa hakuyazuia au kuingilia kati, lazima iwe kwamba aliyaruhusu. Lakini ikiwa una ufahamu kwamba Mungu ni mwema na hawezi kusema uwongo,

utajua lazima tatizo liwe mahali pengine, na utaanza kutafuta jibu.

Ni kama vile unapoingia kwenye chumba kilicho na giza, huwezi kudai moja kwa moja kwamba kampuni ya umeme imekukatisha tamaa. Hapana, lazima utafute swichi, na ikiwa hilo halifanyi kazi, angalia balbu. Una ufahamu kwamba, kuna uwezekano mkubwa shida iko upande *wako*.

Ikiwa una ujuzi kwamba kamwe tatizo haliko upande wa Mungu, kwa vile Yeye ametupa Neno Lake na ahadi zinazofunua mapenzi Yake kwetu, basi utaanza kutafuta kwa bidii sababu inayokatisha jibu Lake.

Wanafunzi walionyesha walikuwa na mawazo ya aina hii wakati hawakuweza kutoa pepo kutoka kwa mvulana aliyepagawa katika Mathayo 17:14-23. Badala ya kuuliza, "Kwa nini Mungu aliamua kumwacha pepo huyo mchafu hapo?" walimwuliza Yesu, "Kwa nini *hatukuweza* kumtoa? Hili linapaswa kuwa swali letu la kwanza hali zinapoonekana kana kwamba zinapingana na Neno la Mungu.

Kwa hiyo tena, ni muhimu kwamba lazima, kwanza kabisa tujue Mungu ni mwema, na pili, kwamba hasemi uwongo. Ni lazima usome Biblia na kuuliza maswali ikiwa unataka kujifunza jinsi Ufalme unavyofanya kazi. Kumbuka, hadithi hizo kuu za Biblia zipo kwa sababu fulani—Yesu anajaribu kukuonyesha jambo fulani.

Tena, Ufalme wa Mungu ni ufalme na unafanya kazi kwa sheria na kanuni ambazo hazibadiliki kamwe. Kama nilivyosema, unaweza kujifunza kanuni hizo, na kuzitumia kama vile mkulima anavyoelewa sheria za wakati wa kupanda na kuvuna katika ulimwengu wa asili na hutumia sheria hizo ili kufanikiwa. Kwa sababu Ufalme unatumia sheria kufanya kazi ambazo zimetolewa kwa kila raia kuelewa na kutumia, *mtu yeyote* anaweza kujifunza kuzihusu. Wakati mwingine, kujua au kutojua jinsi sheria hizi zinavyofanya kazi kunaweza kuwa jambo linaloleta uzima au mauti.

Mark na Hannah walikuja kanisani kwetu wakiwa na hitaji la kupata mtoto. Hadi wakati huo, Hannah aliambiwa na madaktari kwamba kutokana na masuala mbalimbali ya mwili wake, ingekuwa vigumu kwake kupata mimba au kubeba mtoto. Alipoendelea kusikia kuhusu wema wa Mungu na kujifunza sheria za Ufalme katika Kanisa la Faith Life, aligundua kwamba alikuwa mjamzito. Alifurahi kupita kiasi. Lakini muda si muda, alianza kupata maumivu makali ya tumbo. Mara mbili, yalikuwa makali sana kiasi cha kumfanya Hannah kuzimia.

Baada tukio moja kama hili, alitaka mambo yakaguliwe kwa hivyo alienda kwa daktari wake. Daktari wake hakuwa kazini, lakini yule aliyekuwepo alitaka kumfanyia uchunguzi ili kuona shida ilikuwa wapi.

Alichokiona daktari ni ganda kubwa la damu, kisha akamwambia mimba ilikuwa imetoka, na hakusikia mapigo ya moyo wa mtoto.

Daktari alipendekeza aje siku iliyofuata ili mtoto wake aliyekufa atolewe tumboni mwake, lakini Hannah alikataa. Mume wake, Mark, alimtia moyo Hannah kupitia kwa Neno la Mungu na ahadi za Mungu na kumshawishi asitupilie mbali imani yake kuhusu mtoto huyo.

Wikendi hiyo, aliombewa kanisani na alikuwa na hakika kwamba angekuwa na mtoto mwenye afya njema licha ya yale ambayo daktari alikuwa amemwambia.

Jumatatu hiyo, aliingia kuonana na daktari wake binafsi, maana hakuwepo ile siku alipoenda kumwona. Daktari wake alipendekeza afanyiwe uchunguzi mwingine. Hannah alisema daktari alikuwa na sura ya kupigwa na mshtuko usoni mwake alipokuwa akitazama matokeo katika skrini ya kompyuta na mara moja kutazama skanisho zilizofanywa siku chache awali. Kisha akamwambia Hannah maneno yafuatayo: "Nimekuwa nikifanya kazi hii kwa miaka 30, na sijawahi kuona jambo hili likitukia hapo awali. Ninaona ganda kubwa la damu kwenye matokeo ya wiki iliyopita na kutokuwepo kwa mapigo ya moyo. Ninapokutazama leo, ganda lote la damu limetoweka, na kuna mtoto mkamilifu, aliye hai, mwenye mapigo kamili ya moyo."

Baada ya miezi michache, Hannah alizaa mtoto msichana mwenye afya njema, ambaye alimwita Evelyn. Siku moja akiwa na hamu ya kutaka kujua maana ya jina hilo, alitafuta maana yake na kushangaa kwamba lilimaanisha *uhai!* Ninapoandika haya leo, mtoto wa pili wa Hannah anatarajiwa siku yoyote sasa.

Hadithi hii ya kushangaza kwa hakika ilikuwa kazi ya Mungu, lakini kama mwanasayansi wa mambo ya kiroho, unapaswa kufikiria maswali machache kama haya sasa hivi. Kwa nini hili lilitokea? Je, Hannah ni mmoja wa watu wanaopendelewa na Mungu? Je, Mungu alichagua kwa nasibu tu kumponya mtoto wake? Haya ni maswali ambayo yanapaswa kujibiwa.

Tena, kwa Mkristo wa kawaida huo ulikuwa muujiza. Lakini ninawahimiza watu kufikiria upya neno muujiza maana linamaanisha kitu kisicho cha kawaida. Katika Ufalme, hii ilikuwa tu kazi ya sheria ya Ufalme.

Iwapo ningedondosha jiwe na likaanguka chini, ungefikiri mimi ni wazimu ikiwa ningesema kwa sauti, "Ajabu! umeona hilo? Jiwe limeanguka chini; huo ni muujiza!" Hungekubali ni muujiza kwa sababu unajua hiyo ni kazi ya sheria ya mvuto, na inafanya kazi kwa njia sawa kwa *kila mtu wakati wowote. Lazima* jiwe lianguke chini.

Kwa hivyo kama mwanasayansi wa mambo ya kiroho, lazima utafute vidokezo juu ya kile kilichotokea katika hadithi, vidokezo vya kiroho vitakavyofunua sheria za Ufalme zilizopo.

Moja ya hadithi nzuri katika Biblia itakayotusaidia kupata majibu inapatikana katika Luka sura ya nane.

> *Na alipokuwa akienda makutano walimsonga. Na mwanamke mmoja, ambaye ametokwa na damu muda wa miaka kumi na miwili, [aliyekuwa amegharimiwa mali zake zote kwa kuwapa waganga] asipate kuponywa na mtu yeyote, alikwenda nyuma yake, akaugusa upindo wa vazi lake; na mara hiyo kutoka damu kwake kulikoma.*
>
> *Yesu akasema, "Ni nani aliyenigusa?"*
>
> *Basi, watu wote walipokana, Petro alimwambia, "Bwana mkubwa, makutano haya wanakuzunguka na kukusonga."*
>
> *Yesu akasema, "Mtu alinigusa, maana naona ya kuwa nguvu zimenitoka."*
>
> *Yule mwanamke, alipoona ya kwamba hawezi kusitirika akaja akitetemeka, akaanguka mbele Yake, akamweleza mbele ya watu wote sababu yake ya kumgusa, na jinsi alivyoponywa mara. Akamwambia "<u>Binti, imani yako imekuponya</u>; enenda zako na amani."*
>
> — Luka 8:42b-48

Katika hadithi hii, tunapata mwanamke ambaye alikuwa mgonjwa sana kwa miaka mingi wala hakuweza kupona. Alipokuja nyuma ya Yesu, na kugusa vazi Lake alipona mara moja. Sasa, kuna vidokezo vya kina sana vya utendaji wa Ufalme katika hadithi hii ambavyo tunaweza kujifunza hapa na ambavyo vitadhihirisha baadhi ya majibu tunayotafuta.

Kwanza kabisa, umati wote uliokuwa umemzunguka Yesu ulikuwa ukimgusa. Kama hadithi inavyosema, alikuwa karibu kupondwa na umati uliokuwa ukimsonga. Yesu alipouliza, "Ni nani aliyenigusa?" Petro alishangazwa na swali hilo kwa sababu, tena, *kila mtu* alikuwa akimgusa. Lakini Yesu alisema mtu huyu alikuwa amemgusa kwa njia tofauti—alihisi nguvu za Roho Mtakatifu zikimtoka.

Baada ya kusoma hadithi hii, unapaswa kuwa na hamu kubwa rohoni mwako kukoma na kufikiria kile ambacho kilikuwa kimetokea. Akili yako inapaswa kuingia mara moja katika hali ya uchunguzi na kujawa na maelfu ya maswali. Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, tunahitaji kujua kwa nini mwanamke *huyu* aliponywa na hakuna mtu mwingine aliyeponywa.

Ninaweza kukisia kwamba kulikuwa na wagonjwa wengine wengi pale ambao walikuwa wakimgusa kimwili lakini hawakuponywa. Kwa hiyo tunahitaji kuuliza, "Kwa nini upako ulitiririka kwa mwanamke huyu tu na si kwa kila mtu mwingine aliyemgusa wakati huo?"

Jibu la jadi la kidini ni kwamba aliponywa kwa sababu Yesu alimponya. Lakini je, Yesu alikuwa akimhudumia kimakusudi alipoponywa? Je! Aliweka mikono Yake juu yake? Je, aliamuru ugonjwa uondoke kwenye mwili wake? Jibu ni la. Kwa kweli, Yesu hakujua kwamba mwanamke huyo alikuwa pale. Ilimbidi aulize ni nani aliyemgusa.

Kwa hiyo, je, Yesu alichagua kumponya wakati huo? Tena, hakujua alikuwa pale. Kwa hiyo, aliponywaje? Kwa nini aliponywa? Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, tunaweza kuondoa wazo kwamba alikuwa mmoja wa watoto maalum wa Mungu au kwamba alikuwa na uhusiano maalum na Yesu, kwa sababu Matendo 10:34 inasema kwamba Mungu hana upendeleo.

Tunaweza pia kudhani kwamba kwa kuwa Yesu hata hakujua kwamba alikuwa pale, hakuwa na sehemu katika uamuzi wake wa kuponywa siku hiyo. Tunaweza kukubaliana kwamba Yeye alikuwa hifadhi ya upako, lakini hakuwa sehemu ya uamuzi *aliofanya* wa kuponywa wakati huo.

Yesu alituambia hasa jinsi alivyojiingiza katika mamlaka na nguvu za Ufalme. Alisema, "*Binti, imani yako imekuponya. Enenda zako na amani*." Sentensi hii inatuambia kila kitu tunachohitaji kujua na kujibu swali letu la kwa nini na jinsi alivyopokea siku hiyo. Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, hebu tuanze kuchunguza hadithi hii kwa kina ili tuone ikiwa tunaweza kupata dalili za sababu zilizomfanya apokee.

Kwanza kabisa, Yesu alimwita *binti Yake*, kumaanisha kwamba alikuwa sehemu ya taifa la Israeli, mzao wa Ibrahimu. Kama mtoto wa Ibrahimu, alikuwa na baraka na faida za agano alilofanya Mungu na Ibrahimu.

> *Akawaambia, "Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele Zake, na kutega masikio usikie maagizo Yake, na kuzishika amri Zake, Mimi sitatia juu yako maradhi yoyote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye."*
>
> — Kutoka 15:26

Kwa hiyo, Yesu alipomwita binti Yake, hilo lilimaanisha kwamba alikuwa na haki ya kisheria ya mambo yote yaliyokuwa katika agano alilolifanya Mungu na Ibrahimu. Hata hivyo, ukweli huu pekee hauwezi kuwa sababu tu iliyomfanya apokee maana kila mtu pale siku hiyo alikuwa na uhalali

huo huo. Ilibidi kuwe na kitu kingine ambacho kilikuwa kimesababisha nguvu za Ufalme wa Mungu kutiririka. Kisha Yesu ametuambia sababu moja zaidi iliyomfanya apokee. Kwa kweli, Yesu alisema hii ndiyo sababu *haswa* iliyofanya yule mwanamke kupokea kibinafsi.

Alisema *imani yake* ilimponya.

Kwa hivyo, sasa tunajua sababu iliyomfanya aweze kupokea—ilikuwa ni haki yake kupokea kihalali kwa vile alikuwa binti wa Ibrahimu, na pili, imani yake ilikuwa kibonyezi kilichofungulia nguvu hizo kutiririka kibinafsi ndani ya mwili wake wakati huo.

Ukweli kwamba alikuwa binti unaweza kulinganishwa na kampuni ya umeme inayowasha nguvu za umeme zinazoingia kupitia kwa nyaya katika nyumba yako. Nguvu zipo, lakini hiyo haimaanishi kwamba taa zako zitawaka. Lazima pia ufinye kibonyezi kabla ya kuwasha taa.

Kwa hiyo, yeye kama mzao halali wa Ibrahimu, alikuwa na haki ya kisheria ya kuponywa. Walakini, kwa sababu alikuwa na mamlaka juu ya dunia na maisha yake mwenyewe, ilimbidi kuwasha swichi ili kuachilia nguvu hizo.

Lakini swichi iko wapi? Je, tunaiwashaje?

Ili kujua, tunahitaji kufafanua masharti yetu.

## Imani ni nini?

Imani ni neno ambalo Wakristo hutumia kiholela. Na nina hakika kwamba wengi hawajui imani kwa kweli ni nini, kwa nini inahitajika, jinsi ya kujua kama wako katika imani, na jinsi ya kupata imani. Ikiwa imani ndiyo swichi iliyofungulia upako uliomponya yule mwanamke, basi tunahitaji kuchunguza imani kwa ukaribu sana!

Tunapata ufafanuzi wetu wa imani katika Warumi 4.

> *Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa, "Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu; huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*
>
> — Warumi 4:18-21

Hebu tuelewe mpangilio wa hadithi hii. Ibrahimu na Sara hawangeweza kupata watoto. Simaanishi walikuwa na shida kupata mtoto na walipaswa kuendelea kujaribu. Namaanisha walikuwa karibu miaka 100, na kamwe haingewezekana. Miili yao haingeweza kupata watoto; haingewezekana kabisa!

Biblia inasema kwamba Ibrahimu alikuwa *amesadiki kikamilifu* kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kufanya yale aliyosema licha ya mambo ya asili yaliyodhihirisha ukweli tofauti. Huu hapa ni ufafanuzi wetu wa neno imani: "kuwa na hakika kabisa kwamba Mungu ana uwezo wa kufanya yale ambayo ameahidi."

Ninaliweka hivi: "**Moyo wako unapokubaliana na mbingu**." Si kukubaliana tu kiakili na kile anachosema Mungu bali *kusadiki kikamilifu*.

### Ufafanuzi wetu wa maana ya imani

Sema kwa sauti pamoja nami ili kuhakikisha kuwa umeelewa: Imani ni kusadiki kikamilifu kile anachosema Mungu! Ni wakati mioyo na akili zetu zinakubaliana na mbingu, *kushawishiwa kikamilifu*.

### Kwa nini imani inahitajika?

Mbona Mungu huwa hamponyi kila mtu hospitalini anapotaka? Kwa nini huwa hakomeshi vita? Kwa nini huwa hatumi malaika kutuhubiria Injili? Nina hakika umesikia maswali haya yote hapo awali. Jibu ni kwamba hawezi kufanya hivyo.

Si kwamba Mungu hana uwezo wa kufanya hivyo, lakini hana mamlaka ya kufanya hivyo.

Ili kuelewa ninachosema, tunahitaji kuangalia Waebrania.

> *Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema,*
>
> *"Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake."*
>
> *Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu <u>kisichowekwa</u> chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*
>
> — Waebrania 2:6-8

Mungu alimpa mwanadamu mamlaka kamili ya kisheria juu ya ulimwengu wote alipowekwa hapa. Hakuna kitu ambacho hakikuwa chini ya mamlaka yake. Alitawala juu ya eneo hili kwa mamlaka kamili. Uwezo wake wa kutawala kwa mamlaka uliungwa mkono na serikali iliyomweka hapa. Kimsingi, alitawala akiwa na mamlaka aliyokabidhiwa na Ufalme wa Mungu. Alivaa taji ya serikali hiyo, ambayo iliwakilisha utukufu wa Mungu, upako, na cheo cha heshima au mamlaka aliyokuwa nayo.

Sasa, bila shaka, hakuwa amevaa taji halisi ya chuma, lakini alikuwa na taji kwa maana ya kile ambacho taji inawakilisha. Ili kupata picha nzuri ya jambo hili, tafakari kuhusu mfalme wa asili. Ingawa yeye ni mtu wa asili na hana nguvu halisi katika utu wake wa asili, yeye huvaa taji, ambayo inaashiria kwamba hajiwakilishi mwenyewe tu bali ufalme mzima na serikali. Maneno yake yanabeba mamlaka kwa sababu yanaungwa mkono na nguvu na maliasili zote za serikali na ufalme anaowakilisha.

**MBINGU HAINA MAMLAKA DUNIANI ISIPOKUWA MOYO WA MWANAUME AU MWANAMKE UNAPOSADIKI KIKAMILIFU KILE MBINGU INACHOSEMA, AMBAYO INAITWA IMANI.**

Ukifikiria polisi anayeelekeza magari barabarani, yeye husimamisha lori kubwa na mamlaka yanayosema, “Simama kwa jina la sheria.”

Ukifikiria sherifu anayeelekeza trafiki, atasimamisha lori kubwa la trekta kwa maneno machache tu, “Simama, kwa jina la sheria!”

Ndio, lori hilo ni kubwa zaidi kumliko—naye mwenyewe, hawezi kulinganishwa na lori—lakini lori hilo husimama, si kwa sababu ya mtu mwenyewe bali kwa sababu ya beji aliyo nayo, ambayo inawakilisha serikali. Katika hali hii, serikali ni kubwa zaidi kuliko mtu mwenyewe. Dereva wa lori huwa hamhofu *mtu mwenyewe*, lakini anaihofu serikali ambayo mtu huyo anawakilisha, na hilo humfanya dereva wa lori kusimama. Vile vile ni kweli hapa. Adamu alitawala kila kitu kilichoumbwa katika ulimwengu. Nguvu na enzi ya Mungu, iliyowakilishwa na taji ya utukufu na heshima, ilimpa mwanadamu uhakikisho kwamba maneno yake yalitawala kwa niaba ya Ufalme wa Mungu.

*Mbingu ni mbingu za Bwana, bali nchi* ***amewapa wanadamu.***

— Zaburi 115:16

Kanuni hii ya mamlaka ya mwanadamu juu ya dunia ni muhimu kwa ufahamu wako wa sheria ya Ufalme, hasa sababu imani inahitajika ili Mungu apate mamlaka ya kisheria katika hali yoyote.

> *Yesu akawaambia, "Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake mwenyewe, na kwa jamaa zake, na nyumbani mwake." Wala* ***hakuweza kufanya mwujiza wowote huko****, isipokuwa aliweka mikono Yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao.*
>
> — Marko 6:4-6

Nikiuliza watu barabarani ikiwa Yesu angeweza kufanya chochote, labda watasema angeweza. Lakini nikiwauliza kama kuna mahali popote katika Biblia ambapo Yesu alijaribu lakini hakuweza kufanya miujiza, watasema nini?

Ninakuhakikishia wataniambia kwamba hakukuwa na tukio kama hilo katika Biblia. Lakini umesoma kuhusu tukio moja kama hilo, sivyo? Yesu hakuweza kuwaponya. Kama mwanasayansi wa mambo ya kiroho, ninataka kujua kwa nini.

Jibu ni rahisi—hakuweza, na sasa unajua ni kwa nini. Ilikuwa ni kwa sababu hawakuwa na imani, ambayo ina maana kwamba hapakuwa na makubaliano na mbingu, na hivyo mbingu haikuwa na mamlaka ya kisheria katika hali hiyo.

Hakikisha una ufahamu dhahiri wa kile ambacho tumegundua.

**Mbingu hazina mamlaka juu ya dunia isipokuwa moyo wa mwanamume au mwanamke umeshawishika kabisa juu ya kile mbingu inachosema, ambayo ni IMANI.**

Kama katika mfano wetu wa awali, hebu tuseme kwamba mtu fulani uliyemjua ni mgonjwa, na anajulikana sana ulimwenguni kote. Mamilioni ya watu wamwombee lakini mtu huyo anakufa. Je, Neno la Mungu lilishindwa? La. Hiyo haiwezekani. Kwa hivyo, lazima tupate jibu letu mahali pengine.

> *Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba.*
>
> — Mathayo 6:7-8

Watu wengi huamini kwamba watu wengi wanapoomba, ndivyouwezekano wa Mungu kusikia na kusukumwa kusaidia unavyokuwa mkubwa zaidi. Natumai tumeshughulikia mengi ya kutosha hadi sasa kiasi cha kukufanya ujue kwamba huu ni uwongo kabisa. Na tunaposema hapakuwa na imani, kimsingi, tunazungumza juu ya yule anayehitaji kupokea kutoka kwa Mungu kuwa na imani. Kulingana na hadithi yetu ya Marko 6, itabidi ukubali kwamba Yesu alikuwa na imani nyingi, lakini hakuweza kuwaponya.

Kwa hivyo ikiwa mimi na wewe tunazungumza kuhusu rafiki mgonjwa ambaye mamilioni ya watu wanamwombea, nitakuuliza, "Mgonjwa *anasema nini?*"

Tunaweza kuwa na watu bilioni *20* wanaomwombea mtu fulani, lakini ikiwa mtu huyo hana imani na anasema atakufa, basi atakufa.

Tena, hebu tufikirie mfano wetu tulioutazama hivi punde katika Marko 6. Tunajua kwamba Yesu alikuwa na imani ya kuponya, lakini hangeweza kuwafanyia watu chochote bila imani yao.

Watu wengi wamekuja kwangu wakisema kwamba bibi yao au babu yao au jamaa ni mgonjwa na kusema kwamba wamekuwa wakimwombea, lakini hakuna mabadiliko. Mimi kila mara huuliza, "Bibi anasema nini? Babu anasema nini? Ana imani?"

Wajua, huna mamlaka ya kiroho juu ya mtu mwingine. Unaweza kumhudumia, lakini yeye anapaswa kutumia imani yake mwenyewe. Kwa hivyo kitu cha lazima ninachowaambia watu wafanye kama wanataka kuhudumiwa kwa ufanisi ni kubadilisha mtazamo wao kwanza. Ninazungumza juu ya picha aliyo nayo mgonjwa kuhusu hali yake mwenyewe. Huwa ninataka kubadilisha mtazamo huo kutoka kifo hadi uzima.

> *Wanafunzi wa Yohana wakamletea habari za hayo yote. Ndipo Yohana alipowaita wawili katika wanafunzi wake, akawatuma kwa Yesu akiuliza, "Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?"*
>
> *Nao walipofika Kwake, walisema, "Yohana Mbatizaji ametutuma Kwako, akisema, 'Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?'"*
>
> *Na saa ile ile aliwaponya wengi magonjwa yao, na misiba, na pepo wabaya; na vipofu wengi aliwakirimia kuona. Ndipo alipojibu, akawaambia, "Nendeni mkamweleze Yohana hayo mliyoyaona na kuyasikia; vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakasika, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, maskini wanahubiriwa habari njema."*
>
> — Luka 7:18-22

Tazama kwamba Yesu hakurejelea Maandiko. Angesema, "Nyinyi rudini mkamwambie Yohana Andiko hili ama lile." Lakini la, aliwaambia kuhusu mambo yote mazuri yaliyokuwa yakitendeka katika Ufalme wa Mungu.

Fanya vivyo hivyo ili kumsaidia rafiki au mwanafamilia. Mwambie rafiki yako ambaye ni mgonjwa hadithi ya jinsi Yesu alivyomponya mtu mwingine. Ikiwezekana, mwambie hadithi kuhusu mtu ambaye aliponywa kutokana na ugonjwa uleule ulio mwilini mwao. Picha hii itamtia moyo na kuleta matumaini. Matumaini daima huwa na picha, na hii ndiyo picha unayotaka rafiki yako aone, kwamba uponyaji wa ugonjwa huo upo.

Mara rafiki yako atakapoona kwamba anaweza kuponywa, basi atakuuliza jinsi hilo linavyowezekana. Huu ndio wakati ambao umekuwa ukingojea—sasa yuko tayari kupokea maagizo kuhusu Neno la Mungu na kanuni za Ufalme. Kwanza, utataka kumleta katika Ufalme ikiwa hawajazaliwa mara ya pili; na pili, utahitaji kutumia muda pamoja naye kumweleza Maandiko kuhusu uponyaji. Ikiwezekana, mwachie nyenzo fulani ili kusisitiza yale ambayo umemwambia. Tumeona mamia ya watu wakiponywa kila aina ya ugonjwa na kuwekwa huru kwa kufanya hivi. Kitu kingine ninachofanya, kabla ya kuwaombea, ni kuwauliza kwa nini wanafikiri watapona tunapoomba. Ninataka imani yao iunganishwe na Andiko fulani, wala si tendo la kuomba tu.

Sasa tunajua imani ni nini—makubaliano na mbingu, moyo wako ukiwa na hakika kabisa kuhusu kile ambacho Mungu anasema. Pia tunaelewa sasa kwamba imani inahitajika ili kumpa Mungu mamlaka ya kisheria duniani kupitia kwa mtu aliye na mapatano na mbingu.

## Je, tunapataje imani?

*Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*

— Warumi 10:17

Imani hujaje kwa kusikia Neno la Mungu? Mchakato ni upi? Je, kusikia tu Neno ndilo jambo pekee linalohitajika ili imani isitawishwe katika roho ya mwanadamu?

Ili kuelewa jinsi imani inavyokuja na kile ambacho Warumi 10:17 inazungumzia, tunaweza kutazama Marko sura ya 4. Sikuzote mimi husema ukirusha Biblia yako hewani, inapaswa kutua kwenye Marko sura ya 4;

andiko hili ni muhimu hivyo!

Yesu alisema katika Marko 4:13 kwamba usipoelewa kile alichokuwa akifundisha katika sura hiyo, huwezi kuelewa mfano *mwingine wowote* katika Biblia. Hili ni jambo muhimu sana! Kwa nini sura hii ni muhimu sana? Kwa sababu inatuambia jinsi mbingu inavyoingiana na ulimwengu, jinsi inavyopata mamlaka, na mahali hilo hutukia. Hakuna kitu muhimu zaidi katika maisha yako kuliko kujua sura hii yote inazungumzia nini.

Katika sura hii, Yesu anatuambia mifano mitatu kuhusu jinsi imani inavyokuja katika roho ya mwanadamu, ambayo ni, kama unavyojua sasa, hitaji la mbingu kuivamia Dunia kihalali. Hadithi tatu katika sura hii ni mfano wa mpanzi, mfano wa mtu anayetawanya mbegu, na hadithi ya mbegu ya haradali.

Hebu tuanze kwa kutazama hadithi ya pili ambayo Yesu anasimulia katika Marko sura ya 4, hadithi ya mtu anayetawanya mbegu.

> *Akasema, "Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa yenyewe—kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika."*
>
> — Marko 4:26-29

Jambo la kwanza tunalohitaji kufanya ni kufafanua masharti yetu. Je, ni *mbegu* gani ambayo Yesu alizungumzia na ardhi ni nini? Yesu alifafanua maneno hayo mawili katika mfano uliotangulia wa mpanzi katika sura hii hii.

Mbegu ni Neno la Mungu, na ardhi ni moyo wa mwanadamu au roho ya mwanadamu. Kwa hiyo katika mfano huu, Yesu anasema mtu hutawanya Neno la Mungu moyoni mwake. Kisha *peke yake*, udongo, au *moyo* wa mwanadamu, huanza kutokeza imani, au mapatano, na mbingu. Sasa, huu ni mchakato wa asili na kazi ya roho yako ya kibinadamu—utasindika kile ulichoweka humo.

Kabla sijaendelea, ni muhimu kukumbuka maana ya imani ni nini—ni wakati *moyo wa mwanamume au mwanamke umeshawishika kwa uthabiti kuhusu kile mbingu inasema*.

Jambo la kukumbuka hapa ni kwamba kukubaliana na mbingu si kitu sawa na kukubaliana kiakili na Neno la Mungu. Biblia inasema kwamba Ibrahimu *alisadiki kabisa*. Ili kukusaidia kupata picha dhahiri ya maana ya kusadiki kikamilifu, hebu tuseme nimekuambia uruke kutoka juu ya

jengo la Empire State katika Jiji la New York. Ili kukushawishi kujaribu, nikwambie kwamba ukipigapiga mikono yako juu na chini kama ndege kwa nguvu, utaweza kuruka kwa usalama hadi ardhini. Utanicheka waziwazi kwa sababu UNAJUA kitakachokupata. Unajua matokeo bila shaka yoyote. Huko ndiko kusadiki kikamilifu. *Unasadiki*; hakuna uwezekano mwingine—utakufa ukiruka.

Kwa hivyo, hebu tutazame hali nyingine na tuone jinsi utakavyoishughulikia. Tuseme una uvimbe mkubwa sana kwa mwili wako, na daktari amesema una takriban mwezi mmoja wa kuishi: una ugonjwa wa saratani. Daktari kwa kweli amesema kwamba aina yako ya saratani ni nadra sana hivi kwamba hakuna mtu ambaye amewahi kuishi ambaye amegunduliwa kuwa nayo.

Sasa, tuseme unajua kile 1 Petro 2:24 inachosema.

> *"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili Wake juu ya mti," tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; "na kwa kupigwa Kwake mliponywa."*
>
> — 1 Petro 2:24

Maandiko yanatuambia jibu, lakini wewe na mimi tuna tatizo kubwa. Tulikulia katika ufalme wa giza, na upotovu na kifo vilikuwa vimetuzunguka. Tumekulia katika ufalme wa hofu, tukiwa na hakika kabisa ya kile ambacho hofu inasema. Kwa hiyo katika kielezi kilicho hapo juu, tumezoezwa kwamba saratani inaweza kuua. Tuna ushahidi katika kila matangazo ya vyombo vya habari kwamba hii ni kweli. Kwa hivyo tutabadilishaje makubaliano yetu; tutasadikije kikamilifu kile Mungu anachosema? Naam, kwa kweli, hatuwezi peke yetu. Lakini Neno la Mungu li hai na limejaa nguvu, na kwa kulipanda katika roho yako, roho yako na Neno huanza kukubaliana na kile ambacho mbingu inasema.

> *Akasema, "Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana **<u>nchi huzaa yenyewe</u>**—kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika."*
>
> — Marko 4:26-29

Udongo (moyo wako) peke yake, huanza kukubali. Tambua kwamba

huwezi kuomba kupata imani; ni kazi ya moyo wako na Neno. Tunapotazama andiko hili, tunaweza kuona kwamba mapatano ya moyo wetu na mbingu ni mchakato; si jambo linalotokea mara moja. Mfano huu unatuambia kwamba mwanzoni moyo wetu unapopokea Neno, imani huanza kukua, kama vile jani au chipukizi la mbegu iliyopandwa hivi karibuni hukua. Kisha huendelea na kukua kama bua, na kisha huunda kichwa. Kichwa ni mahali ambapo mbegu au matunda yanaanza kuundwa. Mmea unapokuwa katika awamu hii, bado huna chochote cha kula. Mmea haujazaa matunda yake yaliyoiva na kukomaa, lakini unakua.

Ndivyo ilivyo na Neno la Mungu. Hakuna mabadiliko yanayoonekana katika ulimwengu wa asili wakati imani inakua. Bado hakuna makubaliano, lakini hakika mmea *unakua*, imani *itaingia*, na makubaliano *yatafanyika*. Yesu anaendelea kueleza kwamba mbegu katika kichwa inapokomaa au kuiva, wakati wa mavuno umefika, makubaliano yapo, na sasa imani ipo. Unapopanda mbegu kwenye ardhi, kupitia kwa mchakato wa kuchibuka, mmea huanza kukua, ingawa bado hakuna matunda. Mmea unaendelea kukua kwa muda mrefu ikiwa uko katika mazingira sahihi; nao unapokomaa, huzaa matunda yakeUnapopanda mbegu kwenye ardhi, kupitia mchakato wa kuota, mmea huanza kukua, lakini hakuna matunda bado. Mmea unaendelea kukua kwa muda mrefu kama unakaa katika mazingira sahihi. Inapokomaa, huchipua matunda yake.

Tuseme umelima mahindi. Mmea wa mahindi huchipua suke la mahindi, lakini mwanzoni, ni suke dogo tu la mahindi lisilo na mahindi usiyoweza kula. Lakini baada ya muda, nafaka kwenye sikio hukomaa na kuiva. Sasa pata hili! Wakati huo punje ya mahindi kwenye sikio inalingana na punje ya mahindi iliyopandwa ardhini, kuna makubaliano.

**Mbegu iliyo kwenye kichwa cha mmea inapokomaa, huonekana sawasawa—SAWASAWA—na ile iliyopandwa.**

Panda mmea wa mahindi, na mbegu iliyokomaa kwenye sikio itafanana na ile uliyoipanda. Zinafanana. Zinafanana na zina ladha sawa; huwezi kuzitofautisha.

Kwa hivyo hebu nifafanue kile Yesu alichosema. Tunaposikia Neno la Mungu (Warumi 10:17), tunalitawanya ndani ya utu wetu wa roho, yaani mioyo yetu. Tukiliweka Neno hilo mioyoni mwetu, litakua na kukomaa; na litakapokomaa, mioyo yetu itasadikishwa kikamilifu kuhusu kile ambacho mbingu imesema. Mbingu na nchi zinalingana, na mbingu sasa zimepata mamlaka ya kisheria katika ulimwengu kupitia kwa mtu ambaye amesadiki kikamilifu. Mawazo na imani yetu vyote vinalingana kabisa na kile mbingu

inasema kwa ujasiri kamili. Hili si jambo la kiakili. Hiki sasa kimekuwa kile tunachoamini kwa hakika kama vile tunavyoamini kwamba jiwe huanguka linapoangushwa. Mbingu hupanda Neno katika ulimwengu ambapo litasababisha makubaliano na mapenzi ya Mungu. Mbingu zikisema umeponywa, basi hilo Neno likikomaa moyoni mwako, utakachokiona ni kile mbingu zinachosema. Hakuna hofu tena. Ukifumba macho utajiona umepona! Hii ndiyo sababu Waebrania 11:1 inasema,

> *Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni <u>bayana ya mambo yasiyoonekana</u>.*

Unaweza kukosa kuyaona katika hali ya kawaida, lakini umeyaona katika roho yako, na ni halisi, ni kama umeyashikilia mkononi mwako. Makubaliano hayo yanaitwa imani, na imani hiyo husababisha picha hiyo kutokea hapa duniani, katika maisha yako!

Lakini subiri; Marko sura ya nne haimalizii hapo. Baada ya kutufundisha jinsi mioyo yetu inavyokubaliana na mbingu na imani kuingia, inatupa maelekezo ya jinsi ya kuvuna matunda hayo.

> *Hata matunda yakiiva, mara **<u>atapeleka mundu</u>**, kwa kuwa mavuno yamefika.*
>
> — Marko 4:29

Tambua kwamba ingawa moyo unakubaliana na mbingu na kuna imani, bado hakuna kinachotokea. Kwa nini? Vile tumekuwa tukisema wakati wote, una mamlaka ya kisheria hapa katika ulimwengu.

Je, unakumbuka mazungumzo yetu juu ya Luka 8 kuhusu mwanamke aliyetokwa na damu? Kumbuka Yesu alisema, “Binti, imani *yako* imekuponya”? Nilisema basi binti huyo alitambua mbele za mbingu, ya kwamba kwa sababu alikuwa binti wa Ibrahimu, alikuwa na haki za kisheria. Nililinganisha hili na kuwa na nyaya kutoka kwa kiwanda cha nguvu za umeme zilichounganishwa na nyumba yako. Umeme upo lakini unapaswa kuwasha taa kibinafsi. Ndivyo ilivyo pia katika hili. Imani inapoimarika, nguvu zipo, lakini hakuna kitakachotokea hadi ubonyeze swichi.

WEWE unapaswa kuachilia nguvu za Ufalme wa Mungu hapa duniani kwa sababu ni wewe tu, mwanamume au mwanamke uliye duniani, unayeweza kufanya hivyo kisheria. Kanuni hii haswa ndiyo uliyoitumia ulipookoka, kama Warumi 10:10 inavyosema.

> *Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*
>
> — Warumi 10:10

Kwa moyo mtu huamini Neno na kupata haki. Kupata haki kunamaanisha kushughulikiwa kisheria. Kwa hiyo wakati moyo wa mwanamume au mwanamke unakubaliana na mbingu—wakati anaamini kile mbingu zimesema—yeye huhesabiwa haki mbele za mbingu na nchi. Sasa ni halali kwa mbingu *kuingilia* maisha yake na kuathiri dunia kwa niaba ya Ufalme wa Mungu. Lakini cha ajabu, ingawa sasa ni halali na ana imani, bado hakuna kinachotokea. "Lakini, Gary, nilifikiri ulisema ikiwa nina imani, italeta mamlaka ya kisheria ya mbingu hapa." Sahihi, lakini mtu anapaswa kuachilia mamlaka ya mbinguni hapa mara imani inapokuja. Hebu tuangalie Maandiko yetu kwa mara nyingine.

> *Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na* ***kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu****.*
>
> — Warumi 10:10

Ukiwa na imani au kuhesabiwa haki, ni halali kwa mbingu kuivamia Dunia, lakini angalia kwamba andiko linasema kwamba ni kwa kinywa chako utakiri na kuokolewa. Je, unaona sehemu hizo mbili? Sehemu ya Mbingu ni kuleta Neno ndani ya moyo wako ambapo litaleta mapatano hapa ulimwenguni. Kisha makubaliano au imani vikishakuwepo, lazima utende kulingana na makubaliano hayo na uachilie mamlaka ya mbinguni katika hali yako ili kupokea kile ambacho mbingu imesema.

Maandiko yetu katika Marko 4:29, yanasema mavuno yanapokuja, mtu (aliye duniani) huweka mundu ndani. Yeye ndiye anayepaswa kutenda kulingana na Neno la Mungu mara imani inapokuja na kupokea mavuno hayo.

Hebu nirudi nyuma nizungumze kwa muda kuhusu mundu iliyo hapa katika Marko nne. Ninaamini kwamba wengi katika kanisa hawajafundishwa jinsi ya kutumia mundu, maana yake hawajafundishwa jinsi ya kuvuna kile wanachohitaji. Sikujua hilo pia hadi Bwana alipoanza kunifundisha kuhusu utendaji wa Ufalme. Hapa kuna hadithi ya jinsi nilivyopata ufunuo wangu wa kwanza

**UKIWA NA IMANI AU KUHESABIWA HAKI, NI HALALI KWA MBINGU KUIVAMIA DUNIA.**

wa mchakato huu muhimu katika Ufalme. Nilialikwa kuhubiri katika kanisa moja huko Atlanta.

Ilikuwa ibada ya Jumatano jioni; kanisa halikuwa kubwa, na hilo lilikuwa sawa kwangu. Nilipenda sana kuwafundisha watu kuhusu Ufalme. Nilipofika kanisani, niliona ajabu kwamba milango ilikuwa imefungwa na hakukuwa na mtu. Ilikuwa dakika kumi kabla ya ibada kuanza.

Nilisikia lori kubwa sana nyuma yangu, na nilipotazama, niliona lori kuukuu likiingia nyuma ya uchochoro wa kanisa. Sikufikiria chochote juu yake; maana, nilikuwa jijini Atlanta.

Nilipokuwa nikingoja, mwanamume mmoja alikuja kutoka nyuma ya jengo na kujitambulisha kuwa mchungaji. Alisema anasikitika kwa kuchelewa, lakini lori lake kuukuu lilimpa shida kuwaka. Aliniambia ni lazima aliwashe kwa kuliviringisha chini ya kilima maana kifaa fulani cha injini kilikuwa kimeharibika. Aliendelea kusema kwamba wakati mwingine haikuwa ikiwaka kabisa, na ilimlazimu kutembea maili tano hadi kanisani.

Inabidi nikiri kwamba nilishangazwa kidogo na mazungumzo haya. Aliendelea kueleza kwamba kanisa hili kwa kweli lilikuwa huduma ya uenezi na kwamba alilisha maelfu ya watu kila mwezi, kwa kawaida jumla ya milo 10,000 kwa mwezi, kutoka mahali hapo.

Mchungaji alipokuwa akizungumza nilifadhaika sana. Hapa kuna mtu wa Mungu anayelisha watu 10,000 kwa mwezi, na hana hata gari la heshima? Ningeweza kutatua shida hiyo. Nilikuwa na gari mpya sana yenye maili 20,000 nyumbani ambayo ningempa.

Nilimweleza mpango wangu na kwamba ningemtuma mmoja wa wafanyakazi wangu kumletea gari. Yeye, bila shaka, alifurahi sana. Nilitumia jioni hiyo kumfundisha yeye na kanisa lake dogo kuhusu Ufalme wa Mungu na jinsi unavyofanya kazi kuhusiana na pesa. Nilijua ilikuwa muhimu waanze kuonyesha jinsi Ufalme ulivyo kwa wale waliouhitaji sana.

Niliporudi nyumbani, nilipanga gari lipelekwe hadi Atlanta. Wakati mfanyakazi wangu alipokuja kuchukua gari, nilijua kwamba nilikuwa nikifanya shughuli ya kiroho mbinguni. Nilijua kwamba nilipoachilia gari hilo katika Ufalme wa Mungu, ningeweza kumwamini Mungu kupata gari nililohitaji pia.

Mimi sio mtu wa magari, maana yake sivutiwi na magari. Kuna watu wanaovutiwa, lakini si mimi. Kwa hiyo mfanyakazi wangu alipokuja kulichukua niliweka mkono wangu juu ya gari hilo, na nikasema, "Baba, ninaachilia gari hili kwa kazi yako huko Atlanta. Ninapoliachilia, ninalipanda kama mbegu na ninaamini kwamba nimepokea. ..." Sikuweza

kufikiria gari ambalo nilitaka. Kwa hivyo nikasema, "Nitarudi kwako juu ya hilo!"

Kweli, kwa miezi michache iliyofuata, sikufikiria gari sana, lakini asubuhi moja, nilimuuliza mke wangu Drenda aina ya gari ambalo angependa. Baada ya kufikiria kidogo, alisema kuwa gari lenye paa la kukunja au linaloweza kutenganishwa lingekuwa nzuri. Naam, nilimuuliza ni aina gani alitaka, na hakuna hata mmoja wetu ambaye angeweza kufikiria aina yoyote ya magari yaliyopo. Kwa vile nilitaka kumnunulia Drenda gari, nilitaka kuhakikisha kwamba alipata gari alilolipenda. Nilimwambia aangalie mtandaoni au atazame kote na anijulishe ikiwa alipata ile aliyoipenda. Hatukumwambia mtu yeyote kuhusu shauku yetu ya kupata gari jipya, lakini wakati huohuo, tulikaa macho tulipokuwa tukizunguka huku na huko, tukitafuta gari ambalo lingeweza kutuvutia.

Siku moja, tulikuwa tukiingia kwenye mkahawa fulani katika eneo hilo kwa ajili ya kupata chakula cha mchana, na ghafula, Drenda akapaza sauti, "Ndiyo ile!

"Ndiyo ile nini?" Nikauliza.

"Gari ninalopenda." Alikuwa akielekeza kidole upande wa sehemu ya maegesho, kwa hivyo nilizungusha gari letu katika eneo hilo na kusimama nyuma ya gari aina ya BMW 645Ci, gari nzuri bila shaka. Na ninaweza kuongeza gari la gharama kubwa pia. Nilimpongeza kwa chaguo lake na kumwambia lilikuwa gari zuri.

Sasa, unahitaji kujua kwamba mimi na Drenda huwa hatutumii pesa nyingi kununua magari. Kama nilivyosema, sijawahi kuwa mtu wa magari. Maana ninafanya kazi katika eneo la fedha, nilijua pia jinsi zinavyopungua thamani haraka na kwamba ilikuwa bora sikuzote kununua gari ambalo lilikuwa na umri wa mwaka mmoja hadi miwili. Kwa hiyo huo ndio uliokuwa mpango wangu; ningetafuta gari nzuri iliyotumika.

Baada ya juma moja, kijana mmoja kutoka kanisani alinipigia simu na kusema maneno haya, "Nimepata gari la Drenda!" Nilishangaa kwa sababu hatukuwa tumemwambia mtu yeyote kuhusu BMW tuliyoiona siku ile katika chakula cha mchana.

Nilimuuliza ni gari aina gani, akasema ni gari aina ya BMW 645Ci, ile haswa tuliyoitaka. Alisema alipokuwa akizunguka huku na kule, aliliona, na Bwana akamwambia ni gari la Drenda.

"Sawa, sasa una usikivu wangu," nilimwambia. Gari lilikuwa limetumika kwa mwaka mmoja na lilikuwa katika hali nzuri sana. Nilililipia pesa taslimu, na Drenda akapata gari lake. Ajabu, hilo lilitendekaje? Hebu

tulinganishe hadithi hii na yale tuliyojifunza kuhusu kuwa na imani na kutumia mundu.

Nilipotoa gari langu, nilikuwa na imani. Lakini Drenda aliposema kwa sauti, "Ndiyo ile!" alikuwa akitumia mundu, kisha baada ya siku chache, gari likatokea.

Ingawa nilimsikia akisema kwa sauti, "Ndiyo ile!" Sikuhusisha tamko lake na Marko sura ya nne na kutumia mundu. Lakini tukio hili linalofuata lilifanya jambo hili liwe wazi kabisa.

Nimetaja mara kadhaa kwamba ninamiliki ekari 60 na takriban ekari 10 ni ardhi yenye majimaji. Ninapenda kuwinda katika msimu wa joto, na hata ingawa nilikuwa nimewinda bata katika shule ya upili, kwa kweli sikuwa nimefanya uwindaji wowote wa bata kule Ohio. Lakini mwaka huo, bwawa lilikuwa limejaa maji, na makundi makubwa ya bata yaliendelea kurukaruka ndani yake. Mamia kwa siku yalikuwa yakija kulala usiku. Kwa hiyo nilichukua bunduki yangu usiku mmoja na kwenda nje na kuwa na wakati mzuri wa kuua bata wachache kwa ajili ya chakula cha jioni. Katika msimu wa vuli mwaka huo, mimi na vijana wangu tulifurahia uwindaji mzuri wa bata.

Jambo moja nililoona, hata hivyo, ni kwamba wakati mwingi, bata walikuwa umbali ambao risasi zangu hazingewafikia vizuri. Wakati wa kuwinda bata, kisheria unaruhusiwa kutumia risasi za chuma kinyume na risasi za jadi. Risasi za kawaida ni nzito na huhifadhi nishati yake mbali zaidi kuliko risasi ya chuma, na hivyo basi kukawa na tatizo la kupiga risasi wakati wa kuwinda bata. Lakini wakati huo nilipokuwa nikizungumza na wawindaji-bata wenzangu wachache, waliniambia kuhusu bunduki mpya ambazo zimeundwa kwa ajili ya kuwinda bata tu. Walikuwa na uwezo wa kufyatua risasi nzito zaidi na walikuwa wamevaa mavazi ya kuwaficha pia. Nilipendezwa sana na uwezekano wa kununua moja ya bunduki hizo, lakini ilikuwa Desemba, na msimu wa kuwinda bata ulikuwa unakaribia kuisha, kwa hivyo sikufikiria zaidi juu jambo hilo.

Mapema Januari, kwa bahati nilikwenda kwa duka la bidhaa za michezo liitwalo Cabela kutafuta kitu fulani, na nikakumbuka bunduki zile za bata. Nilitaka kuona moja. Kwa hiyo nilipokuwa nikitoka nilipitia sehemu ya bunduki hizo, na nikaona sehemu kamili ya bunduki mpya za kuwinda ndege wa majini. Nakumbuka, bila kufikiria juu yake, nilinyoosha kidole changu kwa ile iliyoonekana bora na kusema kwa sauti kubwa, "Bwana, nitaichukua hiyo." Sikuwa nimefikiria juu yake nilipotamka hilo; maneno yalitoka mdomoni mwangu tu. Msimu wa bata haukufunguka tena hadi

msimu wa vuli, kwa hivyo sikupanga kununua bunduki hadi msimu ulipokaribia kidogo.

Baada ya majuma mawili, nilialikwa kuwa mnenaji katika mkutano fulani wa biashara. Nilipomaliza, Mkurugenzi Mtendaji alinishukuru na kusema walikuwa wameninunulia zawadi. Na cha kushangaza ni kwamba, alileta bunduki ileile—*muundo haswa*—niliokuwa nimeona wiki mbili awali katika lile duka. Kwa kweli, nilishangazwa kabisa na zawadi hiyo ya ukarimu, lakini nilijua hii haikuwa bahati tu. Nilikumbuka nilichosema nilipokuwa kwenye lile duka na kugundua nilichokuwa nimefanya. Nilikuwa nimetumia mundu!

Kuelewa kile ambacho umesoma katika sura hii ni, kama nilivyosema hapo awali, *muhimu* kwako katika kuweza kupokea chochote na kila kitu kutoka kwa Mungu. Kila kitu unachopokea kutoka kwa Mungu kitapitia mchakato huu, kwa hivyo hakikisha unaelewa kile ambacho umesoma hivi punde. Soma tena ikiwa unahitaji! Ndivyo ilivyo muhimu!

SURA YA 8

# UNAHITAJI MKOBA WA FEDHA: SEHEMU YA PILI

Ilibidi tuchukue mchepuko huo mrefu kwa sababu najua ni muhimu kwako kufahamu Ufalme unahusu nini. Tena, Wakristo wengi hawana hawaelewi utendaji wa kisheria wa Ufalme duniani, wala kuelewa msimamo wa kisheria walio nao kibinafsi katika Ufalme. Sasa unafahamu ni kwa nini ilinibidi kuchukua mchepuko huu katika mada hii ya imani na mamlaka. Kwa sababu bila ufahamu huu wa kimsingi, usingejua Maandiko yetu hapa katika Luka yanazungumza nini yanaposema utafuteni kwanza Ufalme na hayo yote mtaongezewa.

Sasa kwa kuwa unajua maana yake, hebu turudi kwenye maandishi yetu.

> *Ninyi msitafute mtakavyokula wala mtakavyokunywa; wala msifanye wasiwasi, kwa maana, hayo yote ndiyo watafutayo mataifa ya duniani, lakini Baba yenu anajua ya kuwa mna haja na hayo. <u>Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa.</u>*
>
> *Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na mioyo yenu.*
>
> — Luka 12:29-34

Tena, Baba tayari anajua unachohitaji, na kila kitu tayari kimetolewa na Baba na tayari ni chako, lakini unapaswa kujua na kuelewa mchakato wa kisheria wa kupokea kutoka mbinguni ili kufurahia yote aliyo nayo.

Mstari wa 32 unaweka wazi urithi wa ajabu ambao umepokea kama mwana au binti wa Mfalme. Anasema, "***Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme.*** "

> *Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.*
>
> — Warumi 8:16-17

Paulo anasema sisi ni warithi pamoja na Kristo. Ukiwa mwana au binti, una urithi—Ufalme.

Koma na utafakari jambo hilo kidogo. Tayari una haki ya kisheria katika yote yaliyo ndani ya Ufalme. Sio lazima kuomba-omba. Ni yako tayari.

Lo, jinsi ninavyotumai ushikilie kauli hiyo. Ndiyo maana 2 Wakorintho 1:20 inasema hivi:

> *Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni "Ndiyo;" tena kwa hiyo katika Yeye ni "Amin;" Mungu apate kutukuzwa kwa sisi.*
>
> — 2 Wakorintho 1:20

Ndiyo maana katika kitabu changu cha mwisho, *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa na Riziki*, nilisema kwamba Sala ya Bwana ina muundo wa ombi la kisheria. Haiulizi inaposema, "*Utupe leo riziki yetu*." Hili si swali; ni ombi la kisheria.

Ni kama vile watoto wangu wanapotaka kiamsha kinywa haiwabidi kuniuliza (bali wanafanya kama wamiliki kwa maneno yao, "Haya, Baba, nipe mayai."), ndivyo ilivyo na Ufalme—tayari una haki ya kisheria kupewa chochote na yote kupitia kwa Yesu Kristo.

Kando na kuwa na ufikiaji wa kisheria wa kile kilicho ndani ya Ufalme, wewe pia ni raia wa Ufalme, jambo ambalo linamaanisha una faida nyingi zaidi, kama vile uraia wako wa Marekani una manufaa ambayo haungeweza kufaidika nayo ikiwa wewe si raia.

*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani Mwake Mungu.*

— Waefeso 2:19

Sasa, hebu tuzungumzie mfuko huo! Yesu alisema unahitaji mfuko wa fedha, unakumbuka?

*Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na mioyo yenu.*

— Luka 12:33-34

Jifanyieni mifuko, akiba isiyopungua katika mbingu ambayo hakuna mtu awezaye kukupokonya. Hebu kwanza tuweke wazi jambo moja: Yesu hasemi kwamba lazima uuze kila ulicho nacho na kubaki bila chochote mpaka uende mbinguni. Kumbuka, Paulo ndiye yule yule aliyeandika 2 Wakorintho 9 ambapo alisema kwamba tutajirishwe katika vitu vyote ili tuwe na ukarimu wote. Kwa hivyo, Paulo hakusema kwamba kuwa na pesa au kuwa na vitu ni dhambi na ni makosa. Yesu alimaanisha ikiwa pesa na vitu *vimekudhibiti*, basi itakuwa bora kuviuza na kuweka moyo wako upya katika hazina usiyoweza kupoteza na inayodumu milele.

Tulipokuwa tukikua pesa ilikuwa kama sanamu. Pesa husaidia kuleta riziki tunayohitaji maishani; hata hivyo, wengi wamegundua kwamba pesa ni mungu mwenye huzuni. Ndiyo maana Paulo alimwambia Timotheo awaonye watu walio na mali watoe na wawe wakarimu ili waendelee kuwa na afya nzuri kiroho. Ni rahisi sana kuwa na moyo unaoona pesa kama sanamu. Kuwa mkarimu ndio dawa ya uchoyo. Pata uzoefu wa kufanya hivyo kila wakati.

*Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.*

— 1 Timotheo 6:17-19

Tazama Paulo alimwambia Timotheo *awaagize*, wala si kuwapa *pendekezo* wale walio matajiri kwamba wawe wakarimu na kuwa tayari kushiriki. Kumbuka, pesa zinahitajika, lakini pesa sio uzima.

**Kwa hivyo hazina yako iko wapi?**

Kutoa hakuufanyi moyo wako kuwa mwororo kwa Mungu na watu tu, bali pia kunalegeza mtego wa pesa ulio moyoni mwako. Moyo hutamani na kuabudu chochote unachoweka mbele yake, kwa hivyo hatupaswi kuziacha nyoyo zetu kutangatanga ovyo. Ni lazima tufunze na kudumisha mioyo yetu kwa Mungu kama chanzo chetu. Kutoa hukabili uchoyo unaovuta mioyo yetu kwa urahisi.

Kwa hivyo kwa nini tunapaswa kutoa hata kidogo? Kwa nini Mungu hawezi kutusaidia kifedha bila utoaji wetu? Hilo ni swali zuri, na tunapata jibu katika Luka sura ya 4 .

Kwanza, kama nilivyosema hapo awali, Mungu hana pesa. Pili, alimpa Adamu mamlaka yote na kamili juu ya dunia, kama inavyosemwa katika Waebrania 2:7-8.

> *Akampandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, "Nitakupa wewe <u>enzi hii yote, na fahari yake</u>, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa Yako."*
>
> *Yesu akajibu akamwambia, "Imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke Yake.*
>
> — Luka 4:5-8

Tukio hili katika Maandiko lilitukia wakati Shetani alipomjaribu Yesu nyikani. Shetani alimwambia Yesu kwamba alipewa enzi zote na fahari zote za mataifa ya ulimwengu. Na, ndio, hii ni kweli. Adamu alikuwa na cheo hicho, lakini alikikabidhi kwa Shetani alipousaliti Ufalme wa Mungu.

Fahari ya taifa ni utajiri wake, na sasa uwezo wa kutawala utajiri wa mataifa ulitawaliwa na Shetani. Usichanganyikiwe—kifungu hakisemi Shetani alipata *mamlaka* juu ya fahari ya dunia yenyewe. Mungu anamiliki ardhi na vyote vilivyomo. Lakini andiko linasema kwamba Shetani ana *madai ya kisheria* juu ya utajiri wa mataifa.

Pesa daima hupigwa chapa na taifa ambalo lina mamlaka kamili juu ya sarafu yake yenyewe. Kwa sababu ya kile Adamu alichofanya, Mungu

hawezi kudai kihalali sarafu ya taifa au kuighushi. Hata hivyo, Mungu anapopata mtu ulimwenguni anayemwamini na aliye tayari kupanda pesa katika Ufalme Wake chini ya mamlaka Yake, basi Yeye hupata kiingilio kisheria na huweza kushughulikia hali hiyo.

Hata hivyo, tena, Mungu hana pesa, kwa hiyo ninamaanisha nini ninaposema anaweza kujihusisha na fedha zetu? Ingawa Mungu hawezi kufanya pesa zijitokeze kwa njia za kimiujiza (hiyo itakuwa kinyume cha sheria kwa sababu ya madai ya kisheria ya Shetani), anaweza kukusaidia kunyakua au kuunda utajiri.

**MUNGU HUFUNGUA MLANGO WA KUPOKEA—SHERIA MUHIMU SANA KATIKA UFALME. TUNAVUNA TULICHOKIPANDA.**

Kama nilivyosema katika hadithi nilizosimulia hapo awali, ukarimu unaipa mbingu mamlaka ya kisheria ya kumpakulia mtoaji maagizo na mwelekeo kuhusu fedha. Unakumbuka hadithi ya samaki katika Luka sura ya 5? Utayari wa Petro kumkopesha Yesu mashua ya biashara ili aweze kuhubiri kutoka humo ulimfungulia mlango Roho Mtakatifu kisheria wa kufunua samaki waliokuwa kwenye kina cha maji.

Kumtolea Mungu hufungua mlango wa kupokea—sheria muhimu sana katika Ufalme. Tunavuna tulichokipanda.

Kwa hiyo ili kufupisha hadithi ndefu, tunajifanyia mifuko katika Ufalme kwa kutoa na kufanya kazi ya Mungu. Utoaji wetu unatupa ufikiaji wa utajiri wa mbinguni, ndiyo maana Paulo aliita "kutoa" mifuko yetu. Ukweli huu unabadilisha kila kitu maishani mwetu. Hatuzuiliwi tena na ufahamu wetu wenyewe. Mungu, Mwenyewe sasa anatusaidia kufanikiwa.

> *Mtatajirishwa kwa kila namna ili mpate kuwa wakarimu kwa kila jambo, jambo ambalo huleta shukrani kwa Mungu kupitia kwetu.*
>
> — 2 Wakorintho 9:11 (Tafsiri ya 'EHV')

Tazama kwamba Biblia inasema *utatajirishwa*, si kwamba *ujitahidi kuwa* tajiri kwa nguvu na hekima yako mwenyewe. La, sasa una mshirika mpya—Roho Mtakatifu—na Yeye anajua mengi zaidi kukuliko.

Ninakumbuka wakati tulipoishi maisha yenye ukosefu kwa miaka ile tisa iliyojaa mafadhaiko. Pesa, au niseme hofu ya kutokuwa na pesa za kutosha, ilikuwa imeutawala moyo mwangu. Ingawa nilikuwa Mkristo, sikuwa nimekuza tumaini langu kwa Mungu vya kutosha ili moyo wangu ubadilishe uaminifu wake kutoka kwa mfumo wa laana ya dunia. Nilikuwa

nimeweka tumaini langu katika hazina mbaya! Wakati huo, *nilijiamini*, na hakika huo ulikuwa uamuzi mbaya.

Ilibidi Mungu anifundishe jinsi ya kujifanyia mfuko ili nipate neema na uwezo Wake. Na ingawa nafikiri kila mtu anayenijua anajua jinsi Mungu alivyofanya hivyo, nataka tena kusimulia hadithi hiyo hapa ikiwa huijui. Unajua, Mungu ni wa kimkakati sana; anajua jinsi ya kufikia kila mmoja wetu.

Napenda kuwinda kulungu lakini sikuwa napata kitu kwa miaka mingi. Nilikuwa ninatoka nje, ninakaa kwa baridi siku hadi siku bila bahati. Sio tu kwamba nilikuwa ninapenda kuwinda; bali nilikuwa na watoto wa kulisha na hakika nilihitaji mawindo. Ingawa nilifanikiwa kidogo hapo awali, miaka kadhaa ilikuwa imepita tangu niwe na msimu mzuri wa kuleta nyama ya kulungu nyumbani.

Siku moja, nilipokuwa nikifikiria nikifikiria kuhusu msimu wa uwindaji wa kulungu uliokuwa ukija, nilisikia sauti ya Bwana. Alisema, "Kwa nini usiniruhusu nikuonyeshe jinsi ya kupata kulungu wako mwaka huu?"

Hilo lilinishangaza. "*Anionyeshe jinsi ya kupata kulungu wangu mwaka huu?" Hiyo ina maana gani?* Nilipoomba kuhusu maneno hayo, nilihisi kutoa fedha kama mbegu au kipaji kwa kusudi hasa la kumwinda kulungu huyo. Nilihisi Bwana akiniambia kwamba nilipotoa mbegu yangu, nilipaswa kuamini kwamba tayari nilikuwa nimempokea kulungu kabla ya kumpata, kulingana na Marko 11:24.

> *Kwa hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*
>
> — Marko 11:24

Ingawa kama Mkristo sikuzote nilitoa na kusaidia kanisa letu, kutoa kama huku kwenye mtazamo uliozingatia na kuamini kwamba nitapokea nitakaposali ulikuwa mpya.

Nilichukua hundi nikaandika katika sehemu ya kumbukumbu, "Kwa ajili ya kulungu wangu wa 1987." Niliiwekelea mikono na kuituma kwa huduma niliyokuwa na imani nayo na nikatangaza kwamba nilipokea kulungu wangu wakati niliituma.

Maana nilikuwa ninaishi katika mipaka ya jiji la Tulsa, Oklahoma wakati huo, kweli sikuwa na mahali pa kuwinda, lakini rafiki yangu kutoka kanisani alinialika twende nyumbani kwa nyanyake mashambani

kwa ajili ya Siku ya Kutoa Shukrani. Alisema kulikuwa na kulungu wachache karibu na shamba hilo. Kwa hivyo familia yangu ilielekea asubuhi mapema ili kufurahia siku hiyo kuu ya chakula na ushirika na sasa kumkamata kulungu wangu.

Rafiki yangu hakujua aniambie niende wapi hasa, lakini kulikuwa na malisho ya wanyama yaliyokuwa yamepakana na msitu, akapendekeza niende huko na nikae karibu na mti mkubwa uliokuwa pale.

Sasa, nataka upate picha hii. Niliketi sehemu ambayo nyasi ilikuwa imekatwa na mti mkubwa ulikuwa katikati. Ninapotazama nyuma, nilikuwa nimeketi kando ya mti pale nje uwanjani. Kulipopambazuka, niliwaza, *Sitafua dafu kuketi mahali palipo wazi. Ninahitaji kutafuta mahali pazuri pa kukaa*.

Nikiwa nafikiria kuinuka na kuelekea porini, sikujua ni nini kilikuwa kinatokea nyuma yangu upande mwingine wa ule mti. Bila mimi kujua, kulungu dume alikuwa akikimbia kwenye uwanja nyuma yangu. Mti ulizuia kulungu dume kuniona wala mimi kumwona. Fahamu aliukimbilia mti ule, akanusa harufu yangu, na kusimama ghafla ili kujua nilikuwa wapi.

Kwa sababu dume alisimama na kutazama karibu na mti, macho yetu yalikutana. Dume alikuwa umbali wa yadi tano tu! Hakupoteza wakati katika kutoroka haraka sana. Alikoroma vikali huku akinyanyuka kwa kasi kuelekea msituni.

Sasa, kujaribu kumlenga kikamilifu kulungu huyo mwenye mkia mweupe mwenye mbio za kasi na kufyatua risasi haikuwa rahisi. Kusema kweli, sikuwa nimewahi kumpiga risasi kulungu aliyekuwa anakimbia. Nakumbuka kwamba ilikuwa vigumu kumfikia kulungu huyo kwa sababu alikuwa akiruka juu angani, kama vile kulungu wenye mikia nyeupe wanavyofanya wanapokimbia kwa kasi. Lakini nilipofyatua risasi, alianguka wala hakusonga. Nilishtuka! Rafiki yangu aliposikia sauti ya bunduki, alitoka nje na kunipongeza kwa kumuua kulungu kwa kuwa alimwona akiwa amelala hapo chini. Sikuwa nimemwambia rafiki yangu kile ambacho Bwana alikuwa ameniambia kuhusu jinsi ya kumpokea kulungu wangu, lakini sasa nilimtazama na kusema, “Sidhani nilimuua kulungu huyu kwa sababu ya uwezo wangu mkubwa wa kuwinda.”

Nikachomoa kutoka kwa koti langu la kuwinda kipande cha karatasi, ambacho nilikuwa nimeandika siku nilipotuma hundi ile. Nilikuwa nimeandika, “Naamini nimempokea kulungu wangu wa 1987, kwa jina la Yesu.” Kilikuwa na tarehe na saa niliyoomba sala hiyo pia. Niliinua kikaratasi hicho ili rafiki yangu akione kisha nikaanza kumwambia kuhusu

kile Bwana alichoniambia nifanye.

Tukio hili lilivutia umakini wangu. Najua bila shaka kwamba Mungu ndiye aliyesababisha tukio hilo. Bila shaka, unapoona kitu kama hicho, akili yako inajaribu kupendekeza kwamba ilikuwa ni bahati tu. Lakini kwa miaka 34 iliyopita, nimewinda kulungu wangu kwa kutumia njia hiihii niliyotumia katika mwaka wa 1987, bila kukosa, kwa kawaida kwa muda wa chini ya saa moja tu msituni.

Mungu alitumia njia hiihii kuwafikia Petro, Yakobo, na Yohana siku ile kwenye Ziwa la Genesareti. Biblia inasema walishangazwa na kile walichokiona.

> *Maana alishikwa na ushangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioupata; na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washirika wa Simoni.*
>
> *Yesu akamwambia Simoni, "Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu." Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao, wakaacha vyote wakamfuata.*
>
> — Luka 5:9-11

Walistaajabu sana hata wakaacha kila kitu na kumfuata Yesu. Waliona njia bora zaidi ya kufanya mambo, njia bora zaidi.

Mungu aliponionyesha Ufalme na jinsi ya kujifanyia mfuko (kiingilio cha kupata hazina yangu kutoka mbinguni) niliohitaji, moyo wangu ulipata uhakika zaidi kuhusu rasilimali zangu zilizo mbinguni kuliko kile nilichokuwa nacho mkononi mwangu.

Mungu alinifundisha kwamba ningeweza kutoa matoleo kwa ajili ya chochote nilichohitaji, naye angenipa mpango wa kupata au kunyakua pesa.

Sina nafasi hapa ya kushiriki matokeo yote ya ajabu ya Ufalme ambayo nimeona, lakini naweza kusema kwamba mimi na Drenda tumeona mambo ya ajabu sana yakifanyika kifedha. Kutoka kuwa maskini hadi kuwa huru kifedha na kuweza kusaidia kazi ya huduma kwa kutoa mamilioni ya pesa kwa miaka mingi ni jambo la kushangaza.

Mojawapo ya mambo ya kwanza ambayo Mungu alinifundisha nilipoanza kujifunza kuhusu Ufalme ni kutoa matoleo kama mbegu kwa imani kwa ajili ya mavuno hususa. Ingawa sina wakati katika kitabu hiki kuangazia kila kitu, katika vitabu vyangu vingine, utapata hadithi za jinsi Ufalme ulivyo mahususi na jinsi mbegu yako inavyohitaji kuwa mahususi pia. Kitabu changu *Mapinduzi Yako Ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa na Riziki*

kinashughulikia hatua za kuachilia imani yako na jinsi hasa ya kupanda mbegu zako kuliko kitabu hiki. Ninakuhimiza upate nakala hiyo na kujifunza zaidi kuhusu mada hii.

Kitabu hiki kinashughulikia kanuni kuu za Ufalme ambazo Mungu alinifundisha kuhusu kuwa mkarimu na kutoa. Natumai vinakutia moyo na kukuchochea kutaka kujifunza zaidi na kuwa yote ambayo Mungu anayo kwa ajili yako.

SURA YA 9

# SHERIA YA KIPIMO!

Miezi kadhaa iliyopita, mimi na Drenda tulipanda mbegu ya dola 15,000 katika huduma fulani. Nilipokuwa karibu kuachilia imani yangu, Roho Mtakatifu alinikumbusha 2 Wakorintho 9:10-11, na sikuweza kuliondoa Andiko hilo kichwani mwangu kwa siku chache baada ya hilo.

> *Na Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, Naye atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*
>
> — 2 Wakorintho 9:10-11

Nilikuwa nikitafakari sehemu ambayo inasema Mungu humpa mpanzi mbegu na mkate kuwa chakula, na maneno "mkate uwe chakula" yalikamata usikivu wangu. Niligundua kwamba watu wengi hukabiliwa na hofu wanapotaka kutoa kwa sababu ya kutoelewa maneno haya. Watu wengi hufikiri wanapotoa kwamba wanaacha kitu fulani, kwamba *inawagharimu*. Lakini Mungu alikuwa akinikumbusha kwamba sio tu kwamba Yeye hutoa mbegu ya kupanda, lakini pia hutoa mkate kwa ajili ya kula, au kile ambacho mtu anahitaji kibinafsi. Bila shaka, tayari nilijua hilo, lakini nilihisi kwamba alitaka kuhakikisha niwaambie watu kwamba—Yeye hutupatia sisi sote, na hatuhitaji kuogopa kutoa.

Usiku huo, wiki kadhaa baada ya kupanda mbegu ya dola 15,000, nilikuwa karibu kuzima taa na kuelekea kitandani wakati, ghafla, nilikuwa na wazo la kuangalia hisa chache ninazomiliki ili kuona jinsi zilivyokuwa

zinaendelea katika soko la hisa. Nilipofungua akaunti yangu, niliona kwamba zilikuwa zimeongezeka kidogo.

Nilikuwa karibu kuweka simu yangu chini wakati macho yangu yalivutiwa na hisa fulani ambayo sikuimiliki. Nilikuwa nimeiona mara moja hapo awali, na kuwa na wazo la kuinunua. Nilipochunguza utendakazi wake wa siku za nyuma, niliona haikuwa na ongezeko lolote kwa miezi 12, kwa hivyo niliamua kutoinunua.

Lakini kwa sababu moja au nyingine, usiku huo, hisa hii ilinivutia. Ajabu ni kwamba nilihisi nilipaswa kununua kiasi fulani cha hisa hiyo, jambo ambalo halikuwa kawaida kwangu. Kwa hivyo, nilinunua hisa ya thamani ya $1,500 na kuweka simu yangu chini.

Drenda na mimi tulizungumza kwa muda mfupi, kisha nikamwambia kwamba nilikuwa nimenunua hisa hiyo, na nikafungua simu kumuonyesha. Nilipoifungua nilishtuka. Ilikuwa imepanda zaidi ya asilimia 100 kwa saa moja tu! Tulikaa macho na kuongea huku tukitazama thamani yake ikiendelea kupanda taratibu.

Kwa muda wa masaa tatu yaliyofuata, hisa ilipanda hadi thamani ya zaidi ya $17,000, kisha ikatulia. Nilimwambia Drenda, “Hizo ni dola zetu 15,000!”

Niliuza hisa hiyo haraka na kupata faida hiyo. Asubuhi iliyofuata thamani ya hisa hiyo ilipungua na haijaongezeka tena kwa kiwango hicho kwa miezi kadhaa tangu wakati huo. Lilikuwa jambo la ajabu sana kuona. Ninajua kwamba ni Roho Mtakatifu aliyeniangazia hisa hiyo, na nilimwambia Drenda ni Mungu aliyekuwa anarudisha mbegu yetu. Mungu humpa mpanzi mbegu, naye hutoa mkate kwa ajili ya chakula! Unajua, sijali jinsi anavyofanya, lakini Yeye hutimiza neno Lake kila wakati!

Lakini lilikuwa jambo la kushangaza kweli. Baada ya kuuza hisa hiyo na kurejesha pesa kwenye akaunti yangu, niliwaza, *Jamani, kama ningejua ingepanda hivyo, ningenunua zaidi ya $1,500*. Daima mtu unapotazama nyuma ndipo unapoona kwa udhahiri kabisa. Ndio, ningenunua hisa ya $10,000, au akili yako inaweza kuyumbayumba na kuwaza, *Je, kama ningenunua hisa ya $100,000? Fikiria kiasi cha pesa ambacho ningepata kutokana na uwekezaji huo.* Lakini sikununua hisa ya $100,000, $10,000 au hata $5,000; bali ya $1,500. Faida yangu ilizuiliwa. Nilinunua hisa ya $1,500, na ingawa nina hakika ningependa faida zaidi, hilo halingefanyika kwa sababu nilinunua hisa ya $1,500 pekee.

Biblia katika Luka 6:38 inatuambia kilichotokea, kwa nini sikupata pesa zaidi usiku huo.

*Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.*
— Luka 6:38

Tazama, niliweka kipimo, nacho kilipimwa kwangu kulingana na kipimo changu mwenyewe—uwezo niliokuwa nao usiku ule ulikuwa sawa na kiasi cha fedha nilizotumia. Niliweka kipimo, na kwa kipimo hicho hicho, nilivuna faida. Yesu alisema kanuni hiyo hiyo inatumika katika utoaji wako pia.

Nataka kukuonyesha hadithi katika Biblia ambapo jambo hili lilitokea. Tunaweza kujifunza mengi zaidi kutoka kwayo kuhusu sheria ya kipimo.

*Basi, mwanamke mmoja miongoni mwa wake za wana wa manabii alimlilia Elisha, akasema, "Mtumishi wako mume wangu amekufa; nawe unajua ya kuwa mtumishi wako alikuwa mcha Bwana; na aliyemwia amekuja ili ajitwalie wana wangu wawili kuwa watumwa."*

*Elisha akamwambia, "Nikufanyie nini? Niambie; una kitu gani nyumbani?" Akasema, "Mimi mjakazi wako sina kitu nyumbani, ila chupa ya mafuta."*

*Akasema, "Nenda, ukatake vyombo huko nje kwa jirani zako wote, vyombo vitupu; wala usitake vichache. Kisha uingie ndani, ukajifungie mlango wewe na wanao, ukavimiminie mafuta vyombo vile vyote; navyo vilivyojaa ukavitenge."*

*Basi akamwacha, akajifungia mlango yeye na wanawe; hao wakamletea vile vyombo, na yeye akamimina. Ikawa, vilipokwisha kujaa vile vyombo, akamwambia mwanawe, "Niletee tena chombo."*

*Akamwambia, "Hakuna tena chombo." Mafuta yakakoma.*

*Ndipo akaja akamwambia yule mtu wa Mungu. Naye akasema, "Enenda ukayauze mafuta haya, uilipe deni yako; nayo yaliyosalia uyatumie wewe na watoto wako."*

— 2 Wafalme 4:1-7

Hii ni hadithi nzuri yenye ufunuo mwingi kuhusu Ufalme. Mwanamke huyu alienda kwa nabii ili kupata msaada. Alikuwa na deni na alikuwa karibu kunyang'anywa wanawe. Lakini cha kushangaza sana ni kwamba, nabii hakumtolea pesa kutoka kwa hazina yake. Badala yake, alimwuliza swali la ajabu sana unapozingatia jinsi hali ilivyokuwa: "Una kitu gani

nyumbani?"

Nafikiri swali hilo lilimshangaza mwanamke huyu, maana unaweza kidogo kusikia mshangao wake katika jibu lake. "Sina kitu nyumbani!" alisema. Lakini alitaja kile alichokuwa nacho. Alikuwa na kiasi kidogo cha mafuta. Hicho tu ndicho nabii alichohitaji kusikia. Hilo ndilo lililokuwa jibu.

Angalia maagizo yake kwa uangalifu.

> *Akasema, "Nenda, ukatake vyombo huko nje kwa jirani zako wote, vyombo vitupu; wala usitake vichache.*

Usitake vichache. Ni vigapi hivyo? Nafikiri utakubali kwamba idadi ya mitungi ambayo alipaswa kukusanya iko wazi kujadiliwa maana ni yeye tu aliyeweza kujua hiyo ilimaanisha nini kwake. Alikuwa karibu kugundua kwamba hakika hakuwa amekusanya vyombo vya kutosha!

> *Basi akamwacha, akajifungia mlango yeye na wanawe; hao wakamletea vile vyombo, na yeye akamimina. Ikawa, vilipokwisha kujaa vile vyombo, akamwambia mwanawe, "Niletee tena chombo."*
>
> *Akamwambia, "Hakuna tena chombo." Mafuta yakakoma.*

Tazama wakati mafuta yalipoacha kutiririka—si baada ya idadi fulani ya vyombo bali vyombo vilipomalizika. Vyombo vyote vilipojaa, alimwambia mwanawe amletee chombo kingine, naye akamjibu kwamba hakukuwa na chombo kilichosalia. Nina hakika angetaka mafuta yaendelee kutiririka, lakini alikuwa amekusanya idadi fulani tu ya vyombo. Ongezeko lake halikuzuiliwa na Mungu bali na mawazo yake mwenyewe.

Nina hakika alitamani angekuwa na mitungi mingi zaidi. Na kama kweli angeelewa ni kitu gani kilikuwa karibu kutokea, nina hakika angebisha kila mlango mjini kutafuta mitungi. Labda angetuma ombi lake la kukusanya vyombo kwa miji mingine.

Hata hivyo hadithi hii ilikuwa na matokeo mazuri: baada ya kuuza mafuta madeni yake yalilipwa, na familia ikatumia mafuta yaliyobaki.

Lakini kulikuwa na uwezekano wa kuwa na matokeo gani? Angelipa madeni ya *kila mtu* ambaye alijua, angejenga uwanja mpya wa jiji, na kusaidia watu wengi.

Kwa hiyo kwa nini alikusanya idadi hiyo ya vyombo? Naamini jibu ni yeye alikuwa na mawazo ya unusuru. Alikuwa amekazia mawazo kwa deni

alilodaiwa na kiasi cha fedha zilizohitajika ili kuendelea kuwalea wanawe. Badala ya kuwa na mawazo yaliyoshinda shinikizo hilo, alizingatia kuliondoa tu. Ninaamini kama angekusanya mitungi elfu moja, yote ingejazwa. Yeye ndiye aliyeweka kipimo!

Mungu anatupa sisi sote fursa sawa na ya mwanamke huyu. Sisi sote lazima tuchague kiasi cha kipimo chetu.

Hebu nifafanue tunapojikumbusha Andiko letu muhimu la sura hii.

> *Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.*
> — Luka 6:38

Sote tunapenda kunukuu sehemu ya kwanza ya Andiko hili—kwamba tukitoa, tutavuna kwa wingi unaomwagika. Lakini mara nyingi, hatusomi sehemu ya mwisho inayosema tutavuna kulingana na *kipimo kile kile tulichotumia katika kutoa*.

Kwa nini kanuni hii ni muhimu sana kwako na kwangu? Naam, hebu nitoe mfano.

Tuseme unataka kuanza ukulima na nikwambie ninataka kununua tani 136 ya ngano. Mimi na wewe tunakubaliana kuhusu bei ya kila tani, na hivyo unajiandaa kupanda ngano kwa shamba lako la ekari 10.

Nafikiri unajua kitakachotokea. Utapungukiwa sana katika tani zinazohitajika kutimiza mkataba wetu. Kwa nini? Kwa sababu hujui ni ekari ngapi zinazohitajika kupandwa ili kuvuna tani 136 ya ngano.

## NI WAKRISTO WANGAPI WANAOANDAA MALORI KUPELEKA MAVUNO YAO SOKONI LAKINI WANA MIMEA MIWILI TU YA NYANYA SHAMBANI?

Katika mfano wa mkulima kipimo ni idadi ya ekari alizopanda. Kwa upande wa yule mjane, kilikuwa idadi ya vyombo alivyokusanya. Katika mfano wa Yesu, ni kiasi tunachopanda.

Ikiwa mavuno tunayotarajia kupokea hayawezekani kulingana na kipimo tulichopanda, basi huwa tunakatishwa tamaa, na labda watu wenye ufahamu mdogo wanaweza hata kumlaumu Mungu kwa kile kinachoonekana kama kushindwa kwa Neno Lake.

Kwa hivyo hapa kuna swali muhimu: Ikiwa mkulima anahitaji kuvuna

tani 136 za ngano na hajui ni ekari ngapi anazohitaji kupanda, basi anapaswa kufanya nini?

**Muulize mkulima anayejua!**

Sasa tutazame kanuni hii katika hali halisi maishani ambayo mimi huona kila wakati.

Mume na mke wanataka kumaliza kulipa deni la rehani ya $300,000, na wanafahamu wanahitaji kuafikiana, na kutoa matoleo kama mbegu, na kuachilia imani yao. Lakini wanapaswa kutoa mbegu ya kiasi gani? Huwa naulizwa swali hili kila wakati. Je, watahitaji kupanda kiasi gani ili kuvuna $300,000? Hawajui la kufanya. Watahitaji kuuliza Yule anayejua, na huyo ni Roho Mtakatifu.

Sote mara nyingi humsikia akinong'ona jibu la swali hilo. Kwa sababu ya kutokuwa na mafundisho mazuri, huwa tunapuuza sauti hiyo ndogo kama kitu tusichoweza kufanya. Kwa mfano, ikiwa unatoa matoleo XYZ, kisha unahisi kwamba unapaswa kutoa mbegu ya $1,000. Mara moja, akili yako inaingilia kati na kusema, "La, siwezi kufanya hivyo," au vibaya hata zaidi, "Shetani, enenda nyuma yangu."

Fahamu kwa uhakika kwamba <u>Shetani kamwe hawezi kukuambia utoe mbegu zaidi katika Ufalme</u>. Anafahamu kikamilifu sheria hii ya Ufalme. Kwa hiyo, kwa sababu hujajenga ujasiri katika kanuni ya kuweka kipimo, akili yako inapobishana, unakubali na kutoa $100 yako ya kawaida. Na, bila shaka, kama mfano wangu wa ngano, utapungukiwa sana katika mavuno unayohitaji.

Sasa, kabla sijaenda mbali zaidi, ninahitaji kufafanua jambo moja:

Kipimo hakiamuliwi na kiasi cha pesa unazotoa kama mbegu!

Tazama Luka 21:1-4:

> *Akainua macho Yake akawaona matajiri wakitia sadaka zao katika sanduku la hazina. Akamwona mjane mmoja maskini akitia mle senti mbili. Akasema, "Hakika nawaambia, huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wote; maana, hao wote walitia sadakani katika mali iliyowazidi, bali huyu katika umaskini wake ametia vyote alivyokuwa navyo."*

Tazama kwamba Yesu alisema mjane maskini alitoa zaidi kuliko matajiri wote waliotoa siku hiyo. Matajiri walitoa pesa nyingi zaidi, lakini Biblia inasema walitoa kutoka kwa mali zao, au tunaweza kusema kutoka

kwa pesa zao za ziada. Yule mjane maskini alitoa kutoka kwa maisha yake hasa, na hilo lilihitaji imani kubwa.

Huhitaji imani unapotoa matoleo kutoka kwa pesa zako za ziada. Bila shaka, kutoa kwa ukarimu kulingana na utele wako ni jambo jema kufanya, lakini katika nyakati hizo, watu walitazama kile ambacho watu walikuwa wakitoa, na matajiri, mara nyingi, walitoa ili kuonekana na watu na kupata cheo cha kidini kati ya wenzao.

Kwa hivyo kupima kulingana na kiasi cha pesa ulizotoa sio sahihi. Ni sehemu kubwa sana lakini sio sehemu pekee.

Tunapaswa kukumbuka kwamba kilicho "kikubwa" kwa mtu mmoja si lazima kiwe kikubwa kwa mwingine.

Hapo awali, kutoa dola elfu moja ilikuwa pesa NYINGI kwangu. Kwa kweli, tulipoanza, hayo yalikuwa matoleo ya miezi kadhaa. Lakini uwezo wetu umekua, na tumeweza kutoa pesa nyingi zaidi kadiri imani na ujasiri wetu unavyoongezeka.

Haya ndiyo ninayowaambia watu: Unapotoa mbegu kwa ajili ya riziki, tenga muda mfupi wa kumuuliza Roho Mtakatifu ni kiasi gani unachohitaji kutoa na mahali pa kutoa.

Kwa kawaida, huhitaji imani kubwa unapotoa mbegu kwa ajili ya mahitaji ya kawaida kama ile unayohitaji unapotarajia mafanikio makubwa, kama vile kulipia nyumba yako. Ninapotoa kwa ajili ya mambo makuu, huwa nataka *kuhisi* kitu. Namaanisha kwamba sitaki kutoa pesa zangu za ziada tu. Nataka kutoa vya kutosha kiasi cha kunifanya nihisi *imani* yangu ikihusika. Kiasi hicho lazima kiwe kikubwa vya kutosha kuweza kuuchochea mwili wangu kuitikia kisha ninasikia akilini mwangu, *Je, una uhakika kuhusu hili?*

Nimeona kwamba Roho Mtakatifu hujibu unapomuuliza kiasi cha kutoa; lakini kuwa na hakika kwamba unataka kumsikia Yeye.

Imebidi mara nyingi nipate msaada katika hili. Kwa sababu mimi ndiye hulipa bili, ni rahisi kwa Drenda kusikia kiasi cha mbegu yetu na asiwe na wasiwasi wowote. Je, unakumbuka hadithi niliyokusimulia kuhusu mara ya kwanza tulipotoa zile $200,000 kwa shule yetu ya Faith Life?

Naam, sikukuambia maelezo yote ya hadithi hiyo. Tulikuwa tumejitolea kwa miaka mitatu, si deni bali lengo ambalo tulijiwekea kutoa katika kipindi hicho. Siku ilipofika ambayo tulipaswa kutangaza nia yetu na kupanda mbegu yetu ya kwanza, niliwaza tutoe $150,000 pekee. Lakini Drenda alibishana nami kwamba alisikia kutoka kwa Roho Mtakatifu tutoe $200,000. Nilipuuza maoni yake na kushikilia msimamo wangu wa

$150,000. Katika ibada alisisitiza tena tutoe $200,000, lakini nilikataa tena.

Kabla ya kupanda matoleo yetu siku hiyo, mkulima mmoja katika kanisa langu alisimama na kuomba fursa ya kuzungumza. Alitia moyo kila mtu pale kumtumaini Mungu kupata mavuno yake. Aliendelea kueleza kwamba, yeye kama mkulima alitegemea sheria za kupanda na kuvuna maishani na aliona ni za kuaminika. Alisema huwa anatumia $200,000 kila mwaka kupanda mbegu yake. Kisha akaendelea kusema kwamba, mwanzoni, inaweza kuonekana kama upumbavu wa kutupa $200,000 ardhini kwa sababu mara unapozipanda, hakuna njia ya kuzipata tena. Lakini alisisitiza kwamba sheria ya kupanda na kuvuna hushinda kila mara kwa kusababisha mavuno makubwa zaidi ya $200,000 alizotumia kupanda mashamba yake.

Drenda alinipiga kiwiko chepesi ubavuni. Nilielewa alimaanisha nini—kutoa $200,000, na hicho ndicho kiasi tulichotoa. Na unakumbuka jinsi Mungu alivyomsukuma yule makamu wa rais wa ile kampuni ya Uingereza kutupa bonasi ya kila mwaka mwaka huo—ilikuwa kiasi kamili cha $200,000. Haikutugharimu hata senti moja kupanda mbegu hiyo. Na, kama nilivyosema katika sura ya awali, tumekuwa tukilipwa bonasi hiyo kwa miaka mingi na tumepokea mapato zaidi ya dola milioni 2.

Tazama, akili ya Drenda haikuwa imejawa na habari nyingi kuhusu gharama ya bili zetu zote, jambo ambalo lilimfanya asiwe na hofu ya kupiga hatua. Ilikuwa rahisi kwake kumsikia Mungu. Na kwa kweli, hilo ndilo nililohitaji kufanya vile vile. Lakini hii ilikuwa mara yetu ya kwanza kutoa pesa kiasi hicho, kwa hivyo ndio, nilikubaliana na hofu niliposisitiza tutoe $150,000. Namshukuru Mungu kwa ajili ya mke wangu, ambaye alinitia moyo kumwamini Bwana kiasi hicho.

Kupanda mbegu *daima* huhitaji imani, *kila wakati*. Kwa hiyo tusiruhusu woga utuzuie kuvuna yote aliyo nayo Mungu kwa ajili yetu.

> *Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu.*
>
> — 2 Wakorintho 9:6

Katika andiko hili, Paulo alikuwa akikusanya matoleo kwa ajili ya kanisa lingine, na aliwakumbusha waumini kanuni ambayo labda alikuwa amewafundisha hapo awali, kwamba watavuna walichopanda kulingana na kipimo walichotumia walipotoa. Paulo alitaja kanuni ya kuweka kipimo.

Petro alipompa Yesu mashua yake ili aitumie siku ile ziwani, tuliona

kwamba mashua ya Yakobo na Yohana ilijazwa mavuno halisi ambayo imani ya Petro ilisababisha kwa sababu walikuwa washirika. Lakini hebu nikuulize swali: Ikiwa Petro angekuwa na mashua 1,000 katika biashara yake siku hiyo, angejaza mashua ngapi?

Ikiwa jibu lako ni mashua 1,000, uko sahihi.

Tena, tunaona kwamba kipimo kimewekwa. Kipimo cha *chombo* chako ndicho Mungu anachojaza. Kwa hivyo, nakuhimiza kuweka kipimo chenye maono makubwa. Hutaki kuangalia nyuma na kusema, "Lo, thamani ya hisa hiyo ilipanda asilimia elfu katika masaa matatu. Laiti ningeweka zaidi."

Kwa hivyo, ni kitu gani kilichonisukuma kununua hisa ya $1,500 tu usiku ule baada ya kuchochewa na Roho Mtakatifu? Kweli, kwangu, ni kwamba sikumwomba Mungu aniambie kipimo cha kutumia. Nilifanya kulingana na mawazo yangu mwenyewe, wala sikusikia sauti Yake.

Sasa, tafadhali usinunue rundo la hisa kwa sababu ya hadithi hii. Kama nilivyosema awali, huwa siweki pesa nyingi katika soko la hisa. Lakini Mungu alitoa hoja yake usiku ule—Yeye hutoa mbegu kwa mpanzi na mkate kwa chakula, na ulikuwa ukumbusho mzuri kwamba tunapaswa *kuweka* kipimo.

Natumai utakumbuka hadithi hii wakati mwingine Mungu atakapokushawishi kufadhili kazi fulani.

Sote tunapaswa kumruhusu Mungu atuzoeze katika hili.

Nakumbuka wakati thamani ya mali kule Florida iliposhuka mnamo mwaka wa 2009. Tulikuwa na marafiki huko walioishi ufuoni, na mara kwa mara tulikuwa tukiwatembelea. Wakati huo, nyumba nyingi kote Florida zilikuwa zikiuzwa. Tulipokuwa tukitembea ufukweni pamoja na rafiki yetu siku moja, alisema, "Nataka kukuonyesha kitu fulani."

Tulitembea hadi kwenye nyumba ambayo ilikuwa na alama ya kuuzwa. Bei ilikuwa $695,000 kwa nyumba mbili zilizokuwa kwenye mali hiyo. (Ndio, ulisoma vyema, nyumba mbili ufukweni kwa dola 695,000. Ziliuzwa na samani pia. Nadhani sote tunakubali kwamba hiyo ni bei rahisi sana.) Moja ingekodishwa na kuzalisha mapato makubwa, maana zilikuwa ufukweni mwa bahari. Lakini sikutaka kutumia kiasi hicho cha fedha wakati huo, kwa hivyo nilikataa kuzinunua. (Najua, najua, sikuwa mwerevu ipasavyo.) Rafiki yangu tayari alikuwa na nyumba nyingi wakati huo na hakutaka kazi ya kusimamia nyumba mbili zaidi. Alitutembeza hadi kwa nyumba hizo. Sio kila siku mfanyabiashara mwenye mamilionea mengi hutoa ushauri wake akisema, "Hivi ndivyo ningefanya." Kwa kweli, Drenda alisema tununue, lakini sikukubali hata kidogo.

Naam, unaweza kukisia matokeo ya hilo. Nyumba hizo mbili zilinunuliwa na kuuzwa tena baada ya miaka michache kwa $3 milioni.

**KWA HIVYO, USIRUHUSU HOFU INENE NAWE UNAPOPANDA MBEGU NA KUWEKA KIPIMO CHAKO. KUWA JASIRI.**

Unajua jambo la kusikitisha zaidi na la kukatisha tamaa lilikuwa ni nini? Sikuomba kuhusu jambo hilo wakati huo tena. Niliweka kando hekima ya Roho Mtakatifu. Nilipuuza hekima ya rafiki yangu, mke wangu, ambaye ana busara sana. Nilikataa kwa sababu nilijua hilo lingemaliza pesa zetu zote tulizokuwa nazo wakati huo, huku uchumi ukizidi kuzorota, sikujihisi kufanya hivyo. Lakini kama nilivyosema, sikumuuliza Mungu kuhusu jambo hilo, ambalo lilikuwa kosa kubwa sana.

Cha kusikitisha ni kwamba, nimekosa mavuno mengi (sio yote ila mengi), na imebidi Mungu ashughulike jambo hili maishani mwangu.

Siku moja miaka kadhaa iliyopita, ilitokea kwamba Drenda alikutana na Kenneth Copeland alipokuwa likizoni katika hoteli fulani, na akamwalika kula kifungua kinywa pamoja naye na mke wake, Gloria.

Walipokuwa mezani, Kenneth alisema alikuwa na neno kutoka kwa Mungu kunihusu na Drenda. Drenda alilirekodi kwenye simu yake maana sikuwa naye katika safari hiyo. Alisema kama ifuatavyo:

"Nimejaribu kuwaletea nyumba na mashamba, lakini hamkuniruhusu."

Lo! Hilo lilikuwa kemeo. Lakini nilipokumbuka mambo mengi ambayo nilikuwa nimekataa, niliona kosa langu. Kwa hiyo, niliamua kwamba kuanzia siku hiyo na kuendelea, sitakosa mavuno yangu tena. Mara tu nilipofanya uamuzi huo, ilishangaza jinsi Mungu alivyoniletea mavuno ya mbegu yangu haraka.

Kwa hivyo, usiruhusu hofu inene nawe unapopanda mbegu na kuweka kipimo chako. Kuwa jasiri. Huwezi kujua jinsi Mungu atakavyotimiza mambo haya, kama vile yule mjane katika 2 Wafalme 4 hakufikiri kwamba mafuta yangeendelea kutiririka. Ikiwa angejua hivyo, hadithi yake ingekuwa tofauti kabisa. Pengine tungekuwa bado tunasoma kuhusu mjane maskini aliyefanyika bilionea katika biashara ya mafuta.

Hatimaye, daima kumbuka utakuwa ukipanda mbegu inayoleta mavuno makubwa na makubwa zaidi. Unaishi leo kutokana na mavuno ya jana, kwa hiyo unahitaji kukumbuka hilo unapotoa.

Pia, kumbuka kwamba giza huwa kuu zaidi mara tu baada ya kupanda

mbegu. Pipa la mbegu liko tupu na mimea bado haijaanza kuota. Lakini wewe shikilia Neno la Mungu, simama imara, na uombe katika Roho kwa ajili ya mwelekeo na mambo ya ndani kuhusu mavuno ambayo Mungu anakuletea.

Ninataka kumalizia sura hii na hadithi ambayo nimesimulia mara nyingi lakini inafaa niirudie. Inahusu mmoja wa wauzaji wangu, miaka mingi iliyopita, nilipokuwa nikijifunza kanuni ya kuweka kipimo. Alikuwa akijenga nyumba mpya na, kama ilivyo kawaida mtu anapojenga nyumba mpya, pesa kwa bajeti ya hazikutosha. Kawaida kitu hubadilishwa au kuongezwa ambacho hubadilisha gharama ya mwisho.

Naam, katika tukio hili, rafiki yangu alikuwa tayari amemaliza pesa zote alizopewa na benki, na hakuwa na pesa zingine. Ikiwa nakumbuka vyema, hakuwa na pesa zote za kulipia kabati za jikoni. Nafikiri alikuwa na upungufu wa takriban $25,000.

Jioni moja, mmoja wa wawakilishi wa mauzo katika kampuni yangu alienda kwa ibada pamoja na mwakilishi mwingine ambaye alikuwa akijenga nyumba mpya. Karibu na mwisho wa ujumbe, mhubiri alikuwa akipokea matoleo kwa ajili ya kazi fulani, sikumbuki kikamilifu maelezo yake, lakini mwakilishi wa kwanza ambaye alienda kanisani pamoja na yule mwakilishi wa pili ambaye alikuwa akijenga nyumba mpya alinijia na kuniambia kwamba jioni hiyo yule mwakilishi mwingine alionekana kufadhaishwa na jambo fulani.

Alieleza kwamba huyo mwakilishi wa pili alitembea hadi mbele ya kanisa na kutoa matoleo yake kisha akarudi na kuketi. Lakini ilionekana kana kwamba alikuwa na fadhaa fulani. Kisha akaniambia kwamba aliinuka na kurudi mbele ya kanisa na kutoa pesa zaidi. Alipokuwa akirudi kwenye kiti chake, alionekana kuwa na wasiwasi hata zaidi. Aliketi pale kwa dakika chache, kisha akitoa sauti ya kuugumia, alienda mbele tena na kutoa pesa zaidi. Wakati huu aliporudi, alionekana kuwa na amani na fadhaa ilikuwa imekwisha.

Baadaye mwezi huo, mwakilishi aliyekuwa akijenga nyumba mpya alitoa ushuhuda kwamba alikuwa akipanda jioni ile kanisani ili kupata pesa alizohitaji kulipia kabati za jikoni. Ikiwa nakumbuka vyema, mjenzi aliamua kupunguza gharama ya makabati kwa 50%, na aliweza kufanya mauzo ya kutosha ili kulipa bili ya mwisho.

Kwa hiyo, ni kitu gani kilichofanyika jioni hiyo? Mwakilishi aliyekuwa akijenga nyumba mpya aliniambia kwamba hakuwa na amani hadi mara ya tatu alipoenda kutoa tena na kumaliza pesa zote alizokuwa nazo. Wajua,

alikuwa akiomba kuhusu kupata zile $25,000 za kulipia kabati za jikoni, na Roho Mtakatifu akamwelekeza kuweka kipimo kilichohitajika kuleta mavuno aliyokuwa akitafuta.

Kwa hiyo, wakati ujao unapopanda mbegu, kumbuka sheria hii muhimu sana ya Ufalme, sheria ya kipimo.

## SURA YA 10

# MFALME MKARIMU

Nina hakika sote tumefanya hivi. Mtu akija kwetu na kutupongeza kwa kitu fulani tulicho nacho tunapenda kusema, "Oh, hii ni mali ya mtumba nilinunua shilingi mia tano tu."

Kwa nini huwa tunasema hivyo? Kwa nini tunaona aibu ya kuwa na kitu kizuri? Inashangaza na pia kuhuzunisha kwamba tulipojenga nyumba yetu mpya huko mashambani zaidi ya miaka 20 iliyopita, tuliomba kwamba iwe kubwa ndani lakini ionekane ndogo nje. Tulikuwa wachungaji wapya, na tulihisi kwamba watu hawangefurahia ikiwa tungejenga nyumba kubwa. Wakati huo, hatukuwa tukipokea mapato yoyote kutoka kwa kanisa—ilikuwa pesa kutoka kwa biashara yetu wenyewe ambayo tulikuwa tukitumia kujenga—lakini kwa sababu moja au nyingine, tulihisi watu wangefikiri kwamba tunatoa pesa kanisani. Kwa hivyo tulijenga nyumba yenye futi za mraba 7,700, lakini unapoitazama nyumba hiyo, kimsingi inaonekana kama nyumba ya kawaida ya ghorofa mbili.

Baadaye, tuligundua huo ulikuwa ujinga mtupu. Kwa nini tuliona aibu kuwa na baraka za Bwana?

Huwa natumia mlinganisho huu katika mikutano yangu.

Tuseme nijikokote kwenda kwa jukwaa nikiwa nimevaa nguo chakavu na chafu na kutangaza kwamba leo tunasherehekea; mimi na Drenda maana tumemaliza kulipia nyumba yetu. Kisha nishiriki jinsi tulivyofanya kazi kwa bidii (wakati mwingine kwa masaa 80 kila wiki) ili kuikamilisha, lakini tumefaulu.

Kila mtu atapiga makofi na kupiga kelele. Kwa nini? Kwa sababu watasema kweli mtu ameshinda mfumo uliopo. Kuna suluhu.

Lakini nikienda jukwaani na kusema, "Leo, mtu tusiyemjua alikuja na

kutukabidhi dola milioni moja, na tumemaliza kulipia nyumba yetu."

Kila mtu atasema hiyo si haki. Kwa nini? Kwa sababu tumelelewa katika mfumo wa laana ya dunia ya kazi chungu na jasho. Hivyo ndivyo tulivyofunzwa kupata riziki. Bila shaka, ni mfumo wa utumwa, kwani wengi huwa hawafurahii kamwe uhuru halisi wa kifedha. Na kwa sababu hii, wengi hawagundui kusudi lao halisi, yaani ASILI yao ya kiroho. Kwa sababu ya kuishi chini ya mfumo wa unusuru, maamuzi mengi ya kifedha tunayofanya huhusu *pesa*, wala sio *kusudi*. Watu huota ndoto ya kuwa huru ili kufuata ndoto na matamanio yao, lakini kwa wengi, hilo halifanyiki kamwe.

Miaka michache iliyopita, Mungu alianza kunizungumzia kuhusu jinsi sehemu maradufu ilivyo yetu. Sehemu maradufu hutuweka huru kutoka kwa mfumo wa laana ya dunia wa unusuru na kuegemea taabu chungu na jasho ili kuendelea kuishi.

Kwa kifupi, sehemu maradufu inamaanisha *zaidi ya kutosha*. Kuwa na zaidi ya kutosha hutupa fursa ya kuishi bila madeni na kuhusika na kazi yenye kusudi badala ya kuuza maisha yetu kwa sababu ya pesa.

Ingawa nilikuwa nimezungumzia suala la sehemu maradufu katika mikutano yangu kwa miaka mingi, nilihisi kwamba Bwana alitaka kunionyesha jambo jipya ambalo sikuwa nimeelewa. Nilijua kulikuwa na zaidi kuliko yale nilikuwa nimeona, kwa hivyo nilimwomba Roho Mtakatifu anionyeshe ni nini.

Nilianza kujifunza Maandiko kuhusu sehemu maradufu na kumngoja Bwana anionyeshe kile ambacho sikuwa nimeelewa. Naam, alivutia umakini wangu kuhusu kile alichokuwa akijaribu kunifunulia kwa njia ya kushangaza zaidi ambayo sikuwa nimewahi kufikiria.

Siku moja mmoja wa washirika wetu katika huduma, ambaye sikuwa nimewahi kukutana naye alinipigia simu. Baada ya kusoma vitabu vyangu, alipata ufahamu kwamba ninapenda kuwinda, kwa hiyo alipiga simu na kusema, "Nataka kukununulia bunduki. Ni aina gani usiyo nayo?"

Wakati huo, nilikuwa na bunduki ya kawaida ambayo nilitumia kuwinda kila kitu kwanzia kuwinda kulungu hadi bata, ndege na sungura. Pia nilikuwa na nyingine yenye shimo mbili ambayo babangu alininunulia nilipokuwa na umri wa miaka 16. Lakini daima nilikuwa nikivutiwa na bunduki nzuri sana nilizoziona mara nyingi katika magazeti ya kuwinda. Zilikuwa na nakshi nzuri na sehemu ya mbao iliyokuwa imekamilishwa kikamilifu. Kwa hivyo, nilimwambia kwamba sikuwa na bunduki kama ile niliyoiona kwa magazeti na nilikuwa nimeitamani kwa muda. Nilishtuka

aliposema kwamba atanitumia bunduki aina hiyo. Hakika hilo halikuwa jambo la kawaida, kwa hivyo nilisisimka.

Kwa kweli, baada ya juma moja, sanduku lililetwa kwa ofisi yangu ya kanisa, na nilipofungua, hakukuwa na bunduki moja tu bali bunduki *mbili* za kupendeza zaidi ambazo nimewahi kuona.

Nilimpigia simu mshirika wetu kwa haraka na kumshukuru kwa zawadi hiyo nzuri.

Wiki iliyofuata, alinitumia bunduki mbili tena! Sasa nilikuwa na bunduki nne bora zaidi kuliko zozote nimewahi kumiliki. Nilimpigia simu tena, na akasema kwamba mara nyingi, watu hawampigii simu kumshukuru kwa zawadi zake; na kwa sababu nilifanya hivyo, alitaka kunitumia zingine mbili. Bila shaka, nilijua Mungu alikuwa akisababisha jambo hilo. Namaanisha bunduki mbili zilikuwa zikitumwa wakati mmoja, na nilikuwa nikimwomba Mungu kuhusu sehemu maradufu.

Naam, ili kufupisha hadithi ndefu, bunduki zilianza kutumwa kwangu, daima katika jozi. Muda si muda, labda nilikuwa na bunduki kumi na nne mpya, zote zenye ubora wa juu zaidi. Hizi hazikuwa bunduki za bei rahisi. Bunduki hizi zilikuwa na thamani ya maelfu ya dola.

Kisha, nilipewa magari mawili makubwa aina ya Cadillac Escalade yenye rangi ya lulu nyeupe. Wakati huo, tulikuwa na gari letu la miaka kumi la aina ya Honda Pilot, ambalo tulipenda (Honda daima huwa gari nzuri), lakini hiyo si Escalade.

Drenda alikuwa ametamani mkoba wa Louis Vuitton kwa miaka kadhaa, na nilimpa kama zawadi maalum ya Krismasi miaka michache iliyopita. Lakini katika siku yake ya kuzaliwa mwaka huu, alipokea—ulikisia vyema—mikoba miwili ya Louis Vuitton, kila mkoba kutoka kwa mtu tofauti.

Pia ndege yetu ya pili ilikuja katika msimu huu, na vile vile nyumba mbili zilizo ufuoni mwa bahari, na juu ya yote, wakati wa Krismasi, tulipewa makoti mawili meusi yenye manyoya laini kabisa, na gharama ya kila moja ni $10,000.

Hebu nikome kidogo na kusisitiza kwamba sijaribu kujisifia hapa, maana hakuna nilichofanya!!!! Bunduki zilikuja tu. Escalades mbili nyeupe zilijitokeza tu. Mikoba ilionekana tu. Makoti yenye manyoya laini yalikuja tu.

Bila shaka tulihusika katika suala la nyumba hizo mbili, lakini tulikuwa tumepanda mbegu kwa ajili ya nyumba iliyo ufuoni miaka michache awali. Sikujua, na Drenda hakuniambia kwamba miaka michache awali alikuwa

amepata nyumba aliyoipenda katika jarida la mali. Alikumbuka akiashiria picha hiyo na kidole na kusema, “Bwana, nataka hiyo.” Wakati huo, tulikuwa na miradi na kazi zingine nyingi sana zilizohitaji fedha hatukuwa na pesa taslimu za kununua nyumba hiyo huko Florida, lakini tulijua kwamba nyumba ingetokea kwa msimu ufaao.

Siku moja nilipokuwa nikifanya mazoezi ya kukimbia, Bwana alinena nami na kusema, “*Tuma Drenda kesho Florida anunue nyumba yake*.” Kulikuwa uharaka fulani kuhusu kesho katika maneno yake, kwa hivyo nikasema, “Lo! Naam, sawa Bwana.”

Kwa hivyo, Drenda alisafiri hadi Florida na kutazama nyumba 25. Miongoni mwa nyumba alizozitazama, moja iliendelea kumvutia.

Nilisafiri huko na tukaiona pamoja na nikakubali kwamba ilikuwa ya kupendeza. (Wakati huu wote, alikuwa amesahau siku ile alipoashiria kidole gazeti la mali na kutangaza kwamba angemiliki nyumba. Sasa karibu miaka mitatu ilikuwa imepita, na hatukuwa tumewahi kuona kibinafsi nyumba aliyoina ile siku kwa gazeti.)

Tulifanya mkataba wa nyumba aliyoitaka; na siku moja, tulipokuwa tumekaa nyumbani kwetu Ohio tukifanya kazi kuhusu baadhi ya ripoti za uchunguzi wa kandarasi zilizohitajika, ghafla Drenda alipaza sauti, “Hiyo ndiyo nyumba yangu!”

Nilishikwa na mshangao, maana tayari tulikuwa tumefanya mkataba na tulikuwa karibu kumaliza mipango yote ya ununuzi. “Bila shaka ni nyumba yako,” nikajibu.

“Huelewi,” akasema. “Hiyo ndiyo *nyumba hususa* niliyoashiria kidole kwenye jarida la mali miaka michache iliyopita!”

Kisha nikakumbuka kwamba jarida la mali alilokuwa ametazama miaka mitatu awali lilikuwa na nyumba katika mji ule ule huko Florida. Je, ilikuwa nyumba ile ile? Drenda alikuwa na hakika kwamba nyumba ilikuwa ile ile, kisha akaanza kutaja sifa za ile nyumba iliyovutia umakini wake miaka ya nyuma. Ililingana na nyumba hii haswa. Kwa hiyo nilifanya utafiti, na hakika nyumba hii tulikuwa tukinunua iliorodheshwa kuuzwa mwaka na wakati ule ule ambao Drenda aliiona na kutangaza kwamba angeimiliki. Lakini niliona kwamba, kwa sababu isiyojulikana, mara tu baada ya kutangaza kwamba angeimiliki, iliondolewa sokoni.

Niliposoma historia ya nyumba hii, niligundua kwamba haikuwa sokoni wakati huu wote hadi siku chache awali iliporudishwa sokoni. Si ajabu Roho Mtakatifu alisema nimtume Drenda Florida keshoye!

Kwa hiyo, tulinunua nyumba hiyo ya ufukweni, na hatimaye Drenda

akawa na nyumba yake, jambo ambalo alikuwa ametamani maishani mwake. Kisha tulirithi makao ya pili ufuoni huko Canada mwaka huohuo. Lo!

Ikiwa hujaona, kila kitu ambacho Mungu alituma kwetu kilikuwa cha hali ya juu kabisa. Tulishtushwa kidogo kuhusu yale yote yaliyotokea. Lakini Bwana alinena nami na kusema, "*Najua HUHITAJI bunduki kumi na nne. Najua huhitaji Escalades mbili nyeupe…*" na akataja orodha nzima.

Kisha akasema, "Sitaki watoto Wangu wawe na mawazo ya uhitaji. Wanamiliki mali yote, na ni furaha Yangu kuwapa watoto Wangu vitu vyema."

Alinikumbusha kwamba Yeye ni Mungu wa zaidi ya kutosha, Mungu wa sehemu maradufu. Kisha akaendelea kusema kwamba watu Wake hawafikirii ukubwa vya kutosha, hawaoti ndoto kubwa vya kutosha, na wanawekea mipaka kile ambacho anaweza kuwafanyia.

**ALINIKUMBUSHA KWAMBA YEYE NI MUNGU WA ZAIDI YA KUTOSHA, MUNGU WA SEHEMU MARADUFU.**

Drenda na mimi tulishangazwa kidogo na yote ambayo Bwana alikuwa akituonyesha. Tuligundua kwamba tulihitaji kuwaambia watu kuhusu sehemu maradufu. Sehemu maradufu haimaanishi kupata vitu viwili viwili vya aina moja—Bwana alikuwa akitumia matukio haya kuvutia umakini wangu. Sehemu maradufu inamaanisha *zaidi ya kutosha*.

Kisha Mungu aliniambia nifundishe kanisa langu ukweli huu, na nilipaswa kuwaambia kuhusu kila kitu alichotuma kwetu na jinsi yote yalivyotokea.

Sasa, mimi na Drenda hatupendi kamwe kuzungumza kuhusu vitu tulivyo navyo, kwa sababu uzima si vitu, na hakika hatutaki kutilia mkazo kutafuta au kuwa na vitu. Lakini sisi hatukutafuta vitu hivi; Mungu alivituma. Kwa hivyo, tulifundisha kuhusu sehemu maradufu kwa muda wa wiki 11 kanisani, na nafikiri hilo lilikuwa na athari kubwa zaidi katika fedha za watu wetu kuliko mfululizo mwingine wowote ambao nimewahi kufundisha.

Lakini unajua nini? Pia niliwafanya watu waondoke kanisani kwa sababu walichukizwa na mambo niliyoyashiriki. Walisema sikuhitaji bunduki hizo zote, au Escalades mbili, au nyumba mbili za ufukweni, au ndege mbili, au makoti mawili mazuri yenye manyoya laini. Walihisi kwamba nilikuwa nikijisifu tu na kufanya *mambo* kuonekana kuwa muhimu bila sababu.

Lakini walikosa kuelewa vyema jambo lote—Mungu alikuwa

akituonyesha kwamba Yeye ni zaidi ya kutosha. Ufalme Wake haujafunikwa na unusuru kama ulimwengu huu. Ufalme Wake ni ufalme wa zaidi ya kutosha, Naye anafurahia kuwatunza sana watoto Wake.

Ilinibidi kuwakumbusha watu kwamba sikusababisha matukio haya yote. Mungu alifanya hivyo ili kutoa hoja—si kwamba kila mtu anapaswa kuwa mmiliki wa gari la bei ghali bali Mungu anataka tuache kukubaliana na jinsi hali zetu zilivyo na pia kumwekea vizuizi. Anataka tuache kuwa na uzoefu wa kusema la, huku tukimzuia kufanya anachotaka kufanya. Anataka tufahamu kwamba Yeye ni Mungu wa zaidi ya kutosha.

Kuelewa jambo hili ni muhimu sana katika mjadala wetu wa kuwa wakarimu. Lazima uwe na kitu cha kuwa mkarimu nacho, haswa kuweza kuwa mkarimu kila wakati. Najua Mungu alipata usikivu wangu, na nilijifunza kutoaibika kamwe juu ya wema wa Mungu.

Majira ya vuli yaliyofuata, mchungaji wa kanisa fulani katika eneo hilo aliuliza ikiwa angeweza kuwinda kwenye shamba langu. Kila mara mimi huwaambia watu kwamba siruhusu uwindaji wowote hadi mimi na watoto wangu tumepata kulungu wetu, kisha ninawaruhusu watu wachache kuingia kabla msimu haujaisha. Vema, msimu huo wa vuli tulikuwa na kulungu wetu kwenye jokofu, kwa hiyo nikamwalika kasisi huyo aje.

Siku alipokuja nilikutana naye nje ili kumpa mwelekeo wa mahali pa kuwinda. Nikaona kwamba alikuwa akitumia bunduki kuukuu ya kuwinda ndege, maana yake ilikuwa na ushanga mdogo wa shaba wa kutumia kulenga. Haikuwa bunduki ya kuwinda kulungu. Unapaswa kuwa karibu sana na kulungu, kwa sababu bunduki za zamani za kuwinda ndege hazikuundwa kuua kulungu. Lakini, bila shaka, unaweza kuzitumia, kama nilivyofanya mara chache katika uwindaji wangu.

Lakini nilipokuwa nimeketi pale nikizungumza naye, nilikumbuka bunduki nzuri sana ambayo Mungu alikuwa amenipa ya kuwinda kulungu. Kwa kweli, ilikuwa bunduki ya kifahari. Nilihisi Roho Mtakatifu akisema, "*Mbona usimpe mchungaji huyu bunduki hiyo uliyopewa? Una bunduki zingine za kuwinda kulungu, lakini hana bunduki nzuri ya kuwinda nayo.*"

Kwa hiyo, nilimpa bunduki hiyo, na alifurahi sana. Zawadi hiyo ilimzungumzia kuhusu wema wa Mungu na kumtia moyo kumtumaini Mungu.

Kumbuka kile nilichokuambia sura chache zilizopita—kwamba baadhi ya pesa na vitu ulivyo navyo si vyako? Mungu alivituma kwako ili kukidhi hitaji la mtu mwingine.

Nilisema hayo yote kusema hivi: Wewe ni raia wa Ufalme mkarimu ulio

na Mfalme mkarimu, lakini hutafurahia kamwe Ufalme yote yaliyo ndani yake ikiwa hutavunja roho hiyo ya umaskini inayokusukuma kushikilia kila kitu unachopata.

Sijui kama umetazama kipindi cha Runinga kinachoitwa Hoarders ambapo watu huingilia kati kubadili hali hiyo. Nyumba huwa imejaa takataka hata huwezi kutembea humo. Mara nyingi, inabidi nyumba ibomolewe au ijengwe upya kwa sababu iko katika hali mbaya. Hivi ndivyo mioyo yetu inavyoonekana wakati tumejaa uchoyo na tunataka kukusanya kila kitu kwa ajili ya siku za mahitaji ya dharura. Pesa na mali hazipaswi kushikiliwa kwa uchoyo.

Ni vigumu sana kuwa mkarimu wakati umedhibitiwa na unusuru. Mungu anataka ujue kwamba kuna utele katika nyumba Yake, hivyo jisikie huru kuwa mkarimu. Ukarimu wako huwaalika watu katika Ufalme wa Mungu na kufungua mioyo yao kupokea wema na ukarimu Wake. Kumbuka, wema wa Mungu ndio unaowavuta watu kwenye toba.

> *Kwa maana ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu. Naye alipokwisha kupatana na wakulima kuwapa kutwa dinari, aliwapeleka katika shamba lake la mizabibu.*
>
> *Akatoka mnamo saa tatu, akaona wengine wamesimama sokoni wasiokuwa na kazi; na hao nao akawaambia, "Enendeni nanyi katika shamba langu la mizabibu, na iliyo haki nitawapa." Wakaenda.*
>
> *Akatoka tena mnamo saa sita na saa kenda, akafanya vile vile. Hata kama saa kumi na moja akatoka, akakuta wengine wamesimama, akawaambia, "Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi?"*
>
> *Wakamwambia, "Kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri."*
>
> *Akawaambia, "Enendeni nanyi katika shamba la mizabibu."*
>
> *Kulipokuchwa, yule bwana wa shamba akamwambia msimamizi wake, "Waite wakulima, uwalipe ujira wao, ukianzia wa mwisho hata wa kwanza."*
>
> *Na walipokuja wale wa saa kumi na moja, walipokea kila mtu dinari. Na wale wa kwanza walipokuja, walidhani kwamba watapokea zaidi; na hao pia wakapokea kila mtu dinari. Basi wakiisha kuipokea, wakamnung'unikia mwenye nyumba, wakisema, "Hao wa mwisho wametenda kazi saa moja tu, nawe umewasawazisha na sisi tuliostahimili taabu na hari za mchana kutwa."*
>
> *Naye akamjibu mmoja wao, akamwambia, "Rafiki, sikudhulumu;*

*hukupatana nami kwa dinari? Chukua iliyo yako, uende zako; napenda kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe. Si halali yangu kutumia vilivyo vyangu kama nipendavyo? Au jicho lako limekuwa ovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema?"*

*Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho.*

— Mathayo 20:1-16

Kwa hiyo Yesu anasema nini katika mfano huu? Kwanza kabisa, tunahitaji kutambua kwamba mwenye shamba anamwakilisha Baba, na mazao anayotaka si maharagwe ya soya au mahindi. Ni roho za watu. Watenda kazi wanatuwakilisha sisi, ambao anatuma kwenye mashamba ya mavuno. Kuna mambo mawili ninaamini Yesu anataka tuone. Kwanza, tazama jinsi mwenye shamba alivyo na nia ya kutafuta usaidizi.

*Kwa maana ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu.*

Yeye huamka mapema ili kutafuta wafanyakazi, na huenda nje tena na tena siku nzima kutafuta mtu yeyote ambaye anaweza kumsaidia katika mashamba yake. Kuna dharura katika matendo yake. Mavuno yameiva na lazima yavunwe, au yatapotea. Ona kwamba anaajiri mfanyakazi saa moja tu kabla wakati wa kufunga.

*Akatoka tena mnamo saa sita na saa kenda, akafanya vile vile. Hata kama saa kumi na moja akatoka, akakuta wengine wamesimama, akawaambia, "Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi?"*

*Wakamwambia, "Kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri."*

*Akawaambia, "Enendeni nanyi katika shamba la mizabibu."*

Sasa siri ya mfano huo ni hii: Kwa nini aliwalipa akianza na yule aliyeajiriwa mwisho? Jibu linaweza kupatikana katika mstari wa 15.

*Na walipokuja wale wa saa kumi na moja, walipokea kila mtu dinari. Na wale wa kwanza walipokuja, walidhani kwamba watapokea zaidi; na hao pia wakapokea kila mtu dinari. Basi wakiisha kuipokea, wakamnung'unikia mwenye nyumba, wakisema, "Hao wa mwisho*

*wametenda kazi saa moja tu, nawe umewasawazisha na sisi tuliostahimili taabu na hari za mchana kutwa."*

*Naye akamjibu mmoja wao, akamwambia, "Rafiki, sikudhulumu; hukupatana nami kwa dinari? Chukua iliyo yako, uende zako; napenda kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe. Si halali yangu kutumia vilivyo vyangu kama nipendavyo? Au jicho lako limekuwa ovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema?"*

## JICHO LAKO LIMEKUWA OVU KWA SABABU YA MIMI KUWA MWEMA?

Tunaposoma hadithi hii, tunaweza kufikiria, *Hiyo sio haki!* Na unaweza kuwa sahihi unapoitazama na mtazamo wetu wa laana ya dunia wa masaa kwa dola. Lakini kama nilivyosema hapo awali, hayo si mawazo ya Mungu. Mwenye shamba alitaka kuwa na uhakika kwamba wale waliokuja baadaye na kulipwa pesa nyingi wangeona ukarimu wake na kutaka kuendelea kumfanyia kazi. Vyema hata zaidi, mwenye shamba alitaka warudi kwa marafiki zao wote na kuwaambia walilipwa kiasi gani cha pesa na jinsi alivyokuwa mkarimu kwao.

**MUNGU YUKO KATIKA BIASHARA YA WATU, NA IKIWA UTAJIHUSISHA NA BIASHARA YAKE, YEYE NI MKARIMU MNO NA ATAKUTHAWABISHA SANA.**

Kwa hiyo hitimisho la mfano huu ni lipi? Mungu yuko katika biashara ya watu, na ikiwa utajihusisha na biashara Yake, Yeye ni mkarimu mno na atakuthawabisha sana.

### Je, unaweza kupokea bure kutoka kwa Mungu?

Yesu alisimulia mfano mmoja wa ajabu sana katika Biblia kuhusu kupokea, najua umeusikia, mfano wa Mwana Mpotevu. Nataka usome, kisha tutazungumza juu yake. Kaa nami hapa. Tunakaribia mwisho wa kitabu, na sitaki uondoke hadi unisikie. Tunapata hadithi hiyo katika Luka 15. Ni maandishi marefu, lakini tafadhali chukua muda kuyapitia.

*Akasema: "Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; yule mdogo akamwambia babaye, 'Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia.' Akawagawia vitu vyake.*

*Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri*

*kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati. Alipokuwa amekwisha tumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, yeye naye akaanza kuhitaji. Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wa nchi ile; naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. Akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu.*

*Alipozingatia moyoni mwake, alisema, 'Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako.' Akaondoka, akaenda kwa babaye.*

*Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana.*

*Yule mwana akamwambia, 'Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena.'*

*Lakini baba aliwaambia watumwa wake, 'Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.' Wakaanza kushangilia.*

*Basi, yule mwanawe mkubwa alikuwako shamba na alipokuwa akija na kuikaribia nyumba, alisikia sauti ya nyimbo na machezo. Akaita mtumishi mmoja, akamwuliza, 'Mambo haya, maana yake nini?' Akamwambia, 'Ndugu yako amekuja, na baba yako amemchinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu mzima.'*

*Akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. Akamjibu baba yake, akasema, 'Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wowote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu; lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinjia yeye ndama aliyenona.'*

*Akamwambia, 'Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.'"*

— Luka 15:11-32

Kwanza, tunahitaji kuelewa kwa nini mwana mdogo aliondoka nyumbani kwa baba. Jibu lilikuwa kwa sababu alikuwa na taswira mbaya kumhusu baba kama kakake mkubwa. Kumbuka, kaka mkubwa alisema alikuwa mtumwa wa babake maisha yake yote na hakupewa hata mwana-mbuzi kushiriki na marafiki zake. Kwa kaka mkubwa, baba alikuwa mgumu. Kisha unaweza kuuliza kwa nini kaka mkubwa hakuondoka na mwana mdogo. Haya ni mawazo yangu tu, lakini kwa desturi ya Kiyahudi, mwana mkubwa alirithi sehemu maradufu babake alipokufa. Mwana mdogo hakuwa na haki ya kupata faida hiyo. Kwa hiyo, mawazo yangu ni kwamba mwana mkubwa alikuwa na kitu ambacho alijua siku moja kingekuwa chake, kwa hivyo aliona ni bora kubaki.

Mwana mdogo alitaka kutafuta mahali pengine bora na kutoka chini ya utawala wa babake, kwa hivyo alichukua sehemu yake ya urithi na kuondoka. Lakini alipoondoka, alijikuta katika ulimwengu ambao hakuutarajia. Mara pesa zake zilipokwisha, aligundua kwamba nchi nzima ambayo alikimbilia ilikuwa katika hali ya ukosefu wa kifedha. Kukawa na njaa kali katika nchi nzima. Akiwa amekata tamaa kuhusu kupata chakula, alifanya jambo ambalo lilikuwa geni kwake. Alijiuza kama mwajiriwa ili kupata chakula. Hii ilikuwa mara yake kwanza maishani mwake ya kuwa na mawazo ya kuwa mwajiriwa. Hapo awali, alitunzwa kwa sababu ya utambulisho wake, wala sio kwa sababu ya kile alichofanya. Sasa alilazimika kufanya kazi, na kazi pekee ambayo angeweza kupata ilikuwa kulisha nguruwe, kazi chafu kabisa iliyodharauliwa na Wayahudi. Biblia inasema kwamba alikuwa na njaa sana hivi kwamba alitamani mabaki ya chakula cha nguruwe, lakini hakuna mtu aliyempa. Sababu? Kila mtu alikuwa katika hali kama yake, hawakuwa na pesa na waliishi maisha ya unusuru. Je, lolote kati ya haya ninayosema linasikika kama jambo unalolifahamu? Hata hivyo, siku moja aliporudiwa na fahamu na kukumbuka kwamba hata watumishi katika nyumba ya babake walikuwa na chakula cha kutosha.

> *Alipozingatia moyoni mwake, alisema, 'Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako.' Akaondoka, akaenda kwa babaye.*

Alipokumbuka kwamba kulikuwa na chakula kingi nyumbani, alianza

safari ya kurudi nyumbani kwa babake si kama mwana bali mtumwa, kama mwajiriwa. Alipanga kukiri kosa na dhambi yake kwa babaye na kisha kumsihi amruhusu kurudi kama mtumishi. Hata hivyo, alipokaribia nyumbani kwao, babake alikuwa nje. Alipomwona, babake alimkimbilia na kumkumbatia na kumbusu.

> *Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana.*

Hebu tupate picha kamili ya kile kilichotokea, maana hadithi hii ni mfano wa Baba yetu Mungu na sisi. Mwana huyu alikuwa ametoka kwenye zizi la nguruwe. Chini ya sheria ya Kiyahudi, alionwa kuwa mchafu. Dakika ambayo baba alimkumbatia, naye pia alifanyika mchafu, lakini alifanya hivyo kwa hiari kwa upendo wa mwanawe. Badala ya kumkemea mwana huyo mchanga na kumwadhibu kwa sababu ya upumbavu wake, baba huyo alimfunika vazi bora zaidi. Kisha akaweka pete ya muhuri kwenye kidole chake, ambayo ilimaanisha mamlaka yake kama mwana yalirudishwa. Kisha, aliweka viatu miguuni mwake, jambo ambalo lilimaanisha kwamba angeweza kupata mali yote. Utapata desturi hii katika Ruthu 4:7.

> *(Basi hii ilikuwa desturi zamani za kale katika Israeli, kwa habari ya kukomboa na kubadiliana, ili kuyahakikisha yote; mtu huvua kiatu chake na kumpa mwenziwe; ndivyo walivyohakikisha neno katika Israeli.)*

Na mwisho, alifanyiwa karamu ambapo ndama aliyenona alichinjwa.

Huyu mwana mdogo alirudi akiwa na matumaini ya kuwa mfanyakazi wa kuajiriwa, lakini baba alimrejesha kama mwana.

> *Yule mwana akamwambia, 'Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena.'*
>
> *Lakini baba aliwaambia watumwa wake, 'Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.' Wakaanza kushangilia.*

Lakini sehemu inayofuata ya hadithi ndiyo ninayotaka uone.

*Basi, yule mwanawe mkubwa alikuwako shamba na alipokuwa akija na kuikaribia nyumba, alisikia sauti ya nyimbo na machezo. Akaita mtumishi mmoja, akamwuliza, 'Mambo haya, maana yake nini?' Akamwambia, 'Ndugu yako amekuja, na baba yako amemchinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu mzima.'*

*Akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. Akamjibu baba yake, akasema, 'Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wowote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu; lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinjia yeye ndama aliyenona.'*

*Akamwambia, 'Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.'"*

Mwana mkubwa alipokuja, alikataa kuingia nyumbani mara tu alipojua kilichotokea. Tazama kile mwana mkubwa alichosema. *"Tazama, mimi **<u>nimekutumikia</u>** miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wowote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu."* Alikuwa akisema kwamba babake alikuwa mgumu, na alijiitaje? Mtumwa! Lakini baba alimuitaje katika mstari wa 31? Mwanangu! Hii ndiyo hoja yangu.

Ulilelewa na mawazo haya haya kumhusu Mungu, kwamba baba ya vijana hawa wawili alikuwa mgumu, maana yake hakukuwa na thawabu katika kumtumikia. Dini imekufundisha kwamba unapaswa kufanya kazi ili Mungu akukubali. Taswira ya mwana mdogo kumhusu babake ilibadilika, hata hivyo, babake alipomkubali bila kumwadhibu na kumpokea kama mwanawe na si mtumwa. Uhusiano wa mwana mkubwa na babake ulitegemea kile alichofanya, hivyo alimtumikia na kujaribu kila wakati kufanya mambo kwa njia sahihi. Unapotazama utambulisho wako kupitia kwa mtazamo wa kile unachofanya, utakosea kila wakati, na utawahukumu vibaya wale walio karibu nawe kama watu wasiofurahishwa nawe. Lakini tuseme ukweli, kaka mkubwa alikuwa mgumu kibinafsi kiasi cha kutoweza kupokea wema wa baba. Alipomshutumu babake kwa kutomtendea haki na kusema kwamba hakuwahi kumpa hata mbuzi wa kula na marafiki zake, babake alisema yafuatayo.

*Akamwambia, "Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako."*

Hakusema, "Mtumwa wangu." Alimwita mwanae! Mwana ni mmiliki mwenza wa mali; yeye ni mwanafamilia. Mtumwa hana urithi. Kaka mkubwa tayari alikuwa na ufikiaji wa kila kitu katika mali hiyo. Lakini mtazamo wake uliopotoka na usio sahihi kumhusu babake haukumruhusu kupumzika na kufurahia kile ambacho tayari kilikuwa chake, kwa sababu alijiona kama mwajiriwa.

Kwa nini nimetumia muda huu wote kukushirikisha jambo hili? Kwa sababu waajiriwa huwa na wakati mgumu sana kupokea kutoka kwa Mungu! Daima wao huhisi wanapaswa kufanya jambo fulani ili waweze kupata kibali Chake; na kwa sababu ya kupungukiwa, wao huona aibu, woga, na kujiona kama watu wasiostahili kupokea kutoka kwa Baba. Usiporekebisha mtazamo huu maishani mwako, hutaweza kupokea kutoka kwa Baba bila kulipa chochote. Na kumbuka, tunahitaji kupokea kwa hiari ikiwa tunataka kuwa wakarimu kama Baba yetu.

Huwezi kufanyia kazi kuwa na haki mbele za Mungu; ni karama ya upendo Wake kwako. Ninapenda yale ambayo Mathayo 3:16-17 inasema.

*Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu Yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ilisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye."*

Huu ulikuwa wakati ambao Yesu alikuwa akianza huduma Yake. Hakuwa amefanya hata jambo moja lililomfanya astahili kusifiwa na Mungu, lakini ona kile alichosema Mungu. Kwamba alimpenda na alipendezwa Naye.

Je, unawakumbuka wale wezi wawili waliokuwa kando ya Yesu alipokuwa msalabani? Mmoja alisema, "Unikumbuke utakapokuja katika ufalme Wako." Yesu akamjibu, Amin, nakuambia, leo utakuwa pamoja nami paradiso. Alifanya nini ili astahili hilo? HAKUNA kitu!

Tulipoliitia jina la Yesu, Biblia inasema tulizaliwa mara ya pili na kuhamishwa kutoka katika ufalme wa giza na kuingia katika Ufalme wa Mungu. Tulifanya nini ili kustahili hilo? HAKUNA kitu.

Kwa hiyo ninapofunga sura hii, tafadhali kumbuka sikustahili chochote kati ya yale ambayo Mungu alituma kwangu mwaka huo. Alikuwa akijaribu

kunisaidia kuelewa kwamba nilipokea Ufalme wote nilipoliitia jina la Yesu. Sihitaji kuyastahili. Kile ninachohitaji tu ni kupokea wema na ukarimu Wake. Mara tu unapokuwa na uwezo wa kupokea ukarimu Wake, unaweza kuwa mkarimu na wema Wake.

SURA YA 11

# AHADI KWA WALIO WAKARIMU

Bill na mkewe, April, kwa miaka 14 wamemiliki biashara ndogo ya mabomba inayoendeshwa na familia. Kama washiriki wa Kanisa la Faith Life, wameona ukuaji wote ambao umetokea kwa miaka mingi na hadithi zote za ushindi. Kwa hivyo waliposikia kwamba tulitaka kupanua Kanisa la Faith Life ili liwe na athari kubwa kwa jamii, waliunga mkono kabisa jambo hilo.

April alishiriki kwamba alikuwa tayari kabisa kutoa $10,000 kwa mradi huo, lakini alishangaa kabisa wakati Bill aliporudi nyumbani kutoka dukani na kumwambia Bwana alikuwa amemwambia watoe $75,000, si $10,000.

April alikubali kutoa dola 75,000 kwa ajili ya upanuzi huo ingawa hawakujua hilo lingewezekanaje. Hawakuwa na pesa wala wazo lolote kuhusu mahali pesa hizo zingepatikana.

Baada ya wiki chache, idara ya jiji ya maji iliwapigia simu na kuwaambia kwamba walikuwa na mradi mkubwa wa ukarabati na kuwauliza ikiwa wangetaka kuunadi. Walikubali kufanya hivyo na kuanza hatua za kisheria za kupata vyeti vilivyohitajika katika kufanya kazi ya jiji. April alisema mkataba ulikuwa na zaidi ya kurasa 100, na pia ilibidi wapate dhamana. Ulikuwa mchakato mgumu kukamilisha hayo yote, lakini waliyakamilisha. Waligundua kuwa wao ndio kampuni pekee iliyowasilisha zabuni kwenye mradi huo, na hawakujua jinsi au kwa nini waliwasilishwa kutuma ombi.

Mara baada ya kuwasilisha mkataba, halmashauri ya jiji hilo liliwapigia

simu na kuwaambia kwamba waliona kwamba kampuni yao ilikuwa ndogo haingeweza kujenga nyumba 200 ndani ya siku 75 pekee. Lakini baada ya mazungumzo, walisadikisha halmashauri ya jiji kwamba wangeweza kukamilisha kazi hiyo.

Bill alisema ulikuwa mradi mgumu na timu ilifanya kazi masaa mengi kupita kiasi na hata Jumamosi. Lakini unajua nini? Walimaliza kwa wakati uliowekwa na waliweza kutoa $75,000 kwa ukarimu kwa mradi wa kanisa na pia kulipa deni lao la matumizi ya nyumbani katika mchakato huo. Walifurahi sana!

Mungu alikuwa na mpango mkubwa zaidi kwa ajili ya Bill na April kuliko ule waliokuwa nao wenyewe. Alijua mioyo yao ilivyompenda, lakini alitaka kuwanyosha, kunyoosha uwezo wao.

Sasa, kwa kuwa tayari wameidhinishwa kwa kazi ya serikali na baada ya kumaliza kandarasi yenye mafanikio katika jiji, mlango uko wazi kwa kandarasi kubwa zaidi katika siku zijazo.

Mungu anapenda kuwanyoosha watu. Anajua uwezo wetu, lakini mara nyingi hatujui uwezo wetu na kwa kawaida tunahitaji kusukumwa kidogo. Huu ni muundo ambao unahitaji kuzoea.

> *Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda, akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini, akaificha fedha ya bwana wake.*
>
> — Mathayo 25:14-18

Tulisoma mfano huu hapo awali, lakini nataka kuashiria jambo ambalo hatujaangalia.

Tazama kwamba mwenye nyumba alipowapa watumishi wake kazi, Andiko linasema walipewa "kila mmoja kulingana na uwezo wake." Aliyepewa talanta tano aliaminiwa na mikoba mitano, kumaanisha kwamba sasa alikuwa na uwezo wa kusimamia mikoba mitano. Ikiwa angekuwa na uwezo mkubwa kuliko huo, mmiliki angempa zaidi. Vivyo hivyo kwa watumishi wale wengine wawili.

Lakini tazama kilichotokea. Yule mtumishi mwenye mikoba mitano ya dhahabu alizidisha ikawa mifuko kumi. Ni nini kilitokea katika mchakato

huo? Naam, kwa maneno rahisi, uwezo wake, uliongezeka kutoka kiwango cha mikoba mitano hadi kumi. Uwezo wake wa kushughulikia uwajibikaji na usimamizi uliongezeka. Alifanyika mtu wa thamani zaidi kwa mmiliki na alijiweka mahali ambapo angeweza kupandishwa cheo zaidi.

Sasa, hekima ya mmiliki ilikuwa hii. Alijua sifa ya mtumishi mwenye mikoba mitano ya dhahabu. Alijua alikuwa na uwezo wa kuinuka hadi kiwango hicho kipya. Ingawa mwenye nyumba alimpa mtumishi mikoba mitano ya dhahabu, ambayo ilikuwa kiwango cha uwezo wake wakati huo, kazi aliyompa mtumishi pamoja na mikoba hiyo mitano ya dhahabu ingevuna zaidi ya yale ambayo mtumishi alianza nayo na hilo lingemsukuma hadi kwenye kiwango kipya cha usimamizi.

Mmiliki alijua kwamba njia pekee ya kumfanya mtumishi wake kuwa wa thamani zaidi ni kumpa fursa ya kunyooshwa ili agundue uwezo wake mwenyewe. Huu ndio utaratibu Mungu anaotumia katika maisha yetu kutufanya kuwa wa thamani zaidi na kutuzoeza kwa ajili ya hatima zetu.

> *Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia.*
>
> — Luka 16:10

Kama nilivyosema katika sura iliyopita, hakuna kazi ndogo. Utakua kupitia kila moja, na kila moja itaongeza uwezo wako kwa ajili ya kazi ijayo.

Nimepitia mchakato huu mara nyingi sana. Kila wakati, ninapojaribiwa kufikiria, *La, siwezi kufanya hilo. Sijui jinsi ya kulitekeleza*, au *sina wakati*. Lakini kila wakati nasema, “Ndio, nimenyoshwa” na ninapata uwezo zaidi.

Watu wanaweza kutazama maisha yangu na kufikiria, *Lo, lazima iwe rahisi sana kutokuwa na madeni, kuwa na vipindi vya televisheni, kuwa na ndege ya kibinafsi. Lo, ni maisha mazuri kama nini*. Naam, nitakubali—ni maisha mazuri kama nini; ni maisha mazuri matukufu! Lakini hujui jinsi maisha yangu yalivyofikia mahali yalipo leo. Hujui jinsi nilivyopaswa kuvumilia ili kupata uwezo wa kiwango hiki, mara nyingi chini ya mashinikizo makali.

Bado ninaendelea kukua, na Mungu anaendelea kunipa kazi kubwa zaidi na zaidi. Ninahisi kwamba mara kwa mara huwa ninapewa miradi mikubwa inayoninyoosha na kunifanya nihitaji pesa zaidi za kuikamilisha. Lakini singebadilisha shinikizo (na wakati mwingine machafuko) na chochote kingine, kwa kuwa ni mfumo wa Mungu wa mafunzo

yanayonisaidia kutimiza yote niliyoitwa kutimiza.

Ikiwa ningeweza kukupa ushauri mmoja, ni kwamba USIKOME! Mruhusu Mungu akunyooshe na kukufanya mtu uliyekusudiwa kuwa.

Mungu daima hutimiza chochote asemacho. Yeye hashindwi kamwe. Hatma yako iko mbele yako, na lazima uendelee.

**Je, utamruhusu Mungu akunyooshe?**

Nilikuwa katika mkutano wa maombi ya Jumatano jioni. Binti yangu alikuwa akiongoza maombi wakati ghafla alisimama, akanitazama, na kuanza kutabiri. Hivi ndivyo alivyosema:

> *Bwana anasema, "Mavuno ni makubwa mno kwako. Ninakunyoosha. Ni kupitia kwa Roho Wangu pekee utaweza kuelewa kile ambacho kiko karibu kutokea. Je, utapiga hatua kwenda mbele, uniruhusu nikuongoze kwenye mambo magumu zaidi ya ufahamu wako, yale yasiyowezekana?"*

Nikawaza, *La! Najua maana ya hii*. Haikuwa mara yangu ya kwanza kupiga hatua kwenda mbele.

Ninathamini ukweli kwamba Mungu alikuwa akiniuliza ikiwa ningemruhusu aniongoze katika mambo magumu, mambo yasiyowezekana. Najua huwa yanakuwa hadithi nzuri mwishowe baada ya kuyapitia maana Mungu hujitokeza kila mara.

Najua uchungu wa kujinyoosha, gharama ya kwenda mahali ambapo hujawahi kufika hapo awali. Lakini, na hii ni LAKINI kubwa, pia najua wema wa Mungu na mfumo Wake wa ukuzaji, kwa hivyo mara moja nilisema, "NDIO!"

Mungu anataka kudhihirisha uwezo alioweka ndani yako. Hiyo ndiyo njia pekee itakayokuwezesha kufikia hatima yako. Inabidi akunyooshe! Je, Mungu hutunyooshaje? *Shinikizo*.

Ukijaza puto na hewa kisha kuifungulia hewa itoke, puto hunyooka na kuwa kubwa zaidi. Hii ni sawa na mimi na wewe. Mara tunaposhinikiza na kutoacha, uwezo wetu hukua. Uwezo mkubwa huleta miradi mikubwa zaidi na zaidi. Inasisimua kuzungumza juu ya kuwa mkarimu hadi Mungu atakapokuambia utoe $100,000. Au utoe gari lako unalopenda sana. Lazima ukue katika kumtumaini Mungu, na uwezo wako mwenyewe unapaswa kukua.

Majuma machache baada ya kukubali mwito wa Mungu katika

ule mkusanyiko, nilipata kujua ulihusu nini. Vipindi vyetu ya runinga, ambavyo vilikuwa kwenye ratiba ya kila wiki, siku moja kwa juma, viliwekwa kufanyika *kila siku*. Hilo linaweza kuonekana kama jambo zuri, lakini kuna masuala machache ya kushughulikiwa unapokuwa na mabadiliko kama hayo. Kwanza ni kwamba gharama yetu ingepanda 500% papo hapo, na hatukuweza kulipa ada ya kila wiki wakati huo. Pili, ingetubidi tutoe na kuhariri vipindi vitano kwa wiki, na hatukuwa na idara ya televisheni. Wakati huo, tulitumia kampuni nyingine kuja na kurekodi vipindi vinne vya televisheni kila mwezi. Walikuwa wakiandaa kila kitu husu vipindi vyetu, walivituma kwa mtandao, na kufanya kazi yote. Basi nilitambua kwamba nilihitaji kuhamisha yote hayo kwenda kanisani kwetu ili kuyasimamia. Na shida kubwa ilikuwa kwamba mimi na Drenda hatukujua jinsi ya kujenga idara ya TV. Lakini tulijitahidi kubaini mambo.

Kwa upande wa pesa, hatukuwa tumemaliza kujenga shule ya kanisa letu The Now Center na hatukuwa na pesa za ziada za kukuza idara ya televisheni. Kwa upande wa uzalishaji, ilitubidi tununue vifaa vya kamera na kuajiri wafanyikazi wa kufanya kazi hiyo. Kulikuwa na siku ambazo lilionekana kama jambo lisilowezekana. Lakini Mungu alikuwa mwaminifu na aliendelea kututia moyo mimi na Drenda, na tukaendelea.

Shida yetu kubwa ilikuja baada ya takriban miezi minne tulipogundua tulikuwa nyuma dola nusu milioni kwenye bili zetu za muda wa televisheni. Hilo lilikuwa gumu hasa kwa sababu jina la kipindi chetu cha televisheni ni *Fixing the Money Thing.*

Nilijiuliza ikiwa tungeweza kuendelea na vipindi vyetu vya televisheni. Nilihisi singeweza kuendelea kwa uadilifu ikiwa singeweza kulipa bili ya muda katika televisheni. Ilinibidi nipambane na mashaka mengi wakati huo. Lakini tena, Mungu ni mwaminifu, na Drenda alikuwa kitia-moyo kwangu mno.

Katika ndoto wiki hiyo, Mungu alinionyesha kwamba bili zote zingelipwa na mkupuo mmoja, jambo ambalo ningesema halingewezekana kwa asili. Lakini wikendi hiyo kanisani, $500,000 zote zilitolewa katika matoleo, na bili za muda wa televisheni, zililipiwa, na zimelipiwa tangu wakati huo hadi leo.

Lo, imekuwa safari ya ajabu!!!!

Tulibadilika kupitia kwa mchakato huu. Sasa tuna vipindi *viwili* vya televisheni kila siku na sisi hutumia mamilioni ya dola kutangaza Injili. Huwa tunatazama nyuma kujikumbusha yale tuliyokabiliana nayo wakati huo, na hayaonekani kuwa makubwa kama yalivyokuwa zamani. Daima

unapaswa kukumbuka kile tulichojifunza katika sura ya kwanza: Neema ya Mungu inafanya kazi pamoja nawe! Kwa sababu ya kutembea na Mungu miaka hii yote, hakika nimeelewa kwa nini barua nyingi za Paulo huanza na maneno haya:

**"Neema na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo na ziwe zenu."**

Tunapaswa kukumbuka hatuko peke yetu. Neema Yake, uweza huo usio wa kawaida, hufanya kazi katika maisha yetu. Ujasiri unahitajika katika kukubali mwito wa Mungu wa kuingia katika yale usiyoyajua, lakini ni jambo bora; naweza kushuhudia hilo.

Mimi na Drenda tumesafiri ulimwenguni kuhubiri Injili. Tumeona kila muujiza ulioandikwa katika Agano Jipya ukitendeka mbele ya macho yetu wenyewe. Tumeona maelfu ya maisha ya watu yakibadilika na tumelishwa vitu bora zaidi vya nchi. Hakuna maisha mengine bora kuliko maisha yenye kusudi!

Ombi langu kwa ajili yako ni kwamba uzidi sana katika kila kazi njema ambayo Mungu amekujalia kuifanya, na kwamba ukumbuke umuhimu wa kuwa mkarimu.

Kwa kumalizia, hii hapa ni mojawapo ya zaburi ninazozipenda sana:

> *Haleluya. Heri mtu yule amchaye Bwana, apendezwaye sana na maagizo Yake. Wazao wake watakuwa hodari duniani; kizazi cha wenye adili kitabarikiwa. Nyumbani mwake mna utajiri na mali, na haki yake yakaa milele. Nuru huwazukia wenye adili gizani; ana fadhili na huruma na haki. Heri atendaye fadhili na kukopesha; atengenezaye mambo yake kwa haki. Kwa maana hataondoshwa kamwe; mwenye haki atakumbukwa milele. Hataogopa habari mbaya; moyo wake u imara ukimtumaini Bwana. Moyo wake umethibitika hataogopa, hata awaone watesi wake wameshindwa. Amekirimu, na kuwapa maskini, haki yake yakaa milele, pembe yake itatukuzwa kwa utukufu. Asiye haki ataona na kusikitika, atasaga meno yake na kuyeyuka, tamaa ya wasio haki itapotea.*
>
> — Zaburi 112:1-10

Ninapenda sehemu inayosema wenye haki watasikitika. Milele Mungu ndiye mwenye neno la mwisho. Daima mafanikio ndiyo kisasi bora zaidi.

Ikiwa unajua hadithi yangu, unajua kwamba kimsingi sikufaulu katika

shule ya upili nilipata wastani wa alama 1.3. Mungu aliponiambia niende chuo baada ya kuniita kuhubiri, sikuwa nikitaka kufanya hivyo.

Nilipofanya mtihani wa Kiingereza katika mwaka wangu wa kwanza chuoni, Profesa wangu alirudisha karatasi langu likiwa na "F" kubwa kwenye ukurasa wa mbele na barua iliyosema, "Kuna uwezekano kweli kwamba ulienda shule ya upili?" Ilinibidi nitafute mwalimu anisaidie kujifunza kile ambacho sikujifunza katika shule ya upili.

**MUNGU YUKO KATIKA BIASHARA YA WATU, NA IKIWA UTAJIHUSISHA NA BIASHARA YAKE, YEYE NI MKARIMU MNO NA ATAKUTHAWABISHA SANA.**

Kitabu changu cha kwanza kilipochapishwa, nilipokea barua pepe kutoka kwa yule profesa wa Kiingereza. Alisema, "Je, kuna uwezekano kwamba huyu ndiye Gary Keesee yule yule niliyekuwa naye darasani?" Alishtuka sana kuona kwamba nilikuwa nimeandika kitabu.

Wewe na Mungu washtue marafiki zako wote!

Siku moja mtu mmoja niliyesoma naye katika shule ya upili alipitia ofisini mwangu katika kampuni yangu ya kifedha na kusema, "Sielewi. Gary aliacha shule ya upili, na sasa yuko kwenye televisheni ulimwenguni pote?"

> *Ninapenda hadithi kama hizo, na Mungu pia anazipenda! Kwa hivyo kumbuka, hadithi yako haijakamilika. Jitahidi kuwa mkarimu unapowakilisha moyo wa Mungu popote uendapo. Jifunze jinsi Ufalme unavyofanya kazi, na utafurahia maisha mazuri ambayo Mungu ameahidi!*
>
> — Gary Keesee

> *Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu; kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. <u>Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!</u>*
>
> — 2 Wakorintho 9:12-15

Ikiwa ungependa kujifunza zaidi kuhusu Forward Financial Group au mikakati yetu ya uwekezaji wa pesa salama, tembelea forwardfinancialgroup.com au tupigie kwa 1-(888)-397-3328.

Iwapo ungependa kujua zaidi kuhusu Mikutano yetu ya Mapinduzi ya Kifedha au ungependa kuandaa mkutano, tafadhali tupigie simu kwa (740) 964-7400 na uulize ofisi kuu.

**Mungu anataka ubarikiwe na ufanikiwe ili uweze kuwa mkarimu katika kila hali!**

Kamwe hutakuwa huru hadi utakapokuwa huru kifedha. Na jinsi mimi na Drenda tumesema kwa miaka 30, daima hutawahi kugundua wewe ni nani na kutimiza kusudi la kiroho la maisha yako hadi utakaposuluhisha suala la fedha.

**UNAWEZA KUWA HURU!**

Nilithibitisha hilo, na maelfu ya wengine wamethibitisha pia. Neema ya Mungu ipo kukusaidia. Kuna mambo umeitwa kufanya ambayo hutaweza kuyakamilisha bila fedha. Ni lazima upate uhuru wa kifedha si kwa ajili yako mwenyewe na familia yako tu bali pia ili watu waweze kuona Ufalme wa Mungu ukitenda kazi maishani mwako.

**Watu wanatafuta majibu. Wanatafuta kitu halisi. Wanahitaji sana kuona Ufalme na sio dini.**

Mungu ni mwema, na ni mkarimu! Tunapokuwa wakarimu, tunashiriki moyo wa Mungu juu ya watu. Kama vile kunywa maji baridi katika siku yenye joto jingi, kuwa mkarimu hutuliza na kuleta tumaini kwa ulimwengu ulio katika jangwa la umaskini.

Katika kitabu hiki cha tano na cha mwisho katika mfululizo wa **Mapinduzi Yako ya Kifedha** na **Gary Keesee**, gundua jinsi unavyoweza kushirikiana na Mungu katika kazi Zake na kupata viwango vipya vya mafanikio.

Pata ufahamu dhahiri wa kanuni ya Ufalme ya nguvu ya ukarimu na jinsi inavyofanya kazi katika kitabu hiki cha ajabu kilichojaa ufunuo mpya, mifano yenye nguvu kutoka kwa Neno la Mungu, na hadithi za kibinafsi zinazotia moyo kuhusu Gary na wengineo waliotumia nguvu ya ukarimu katika maisha yao na kuona mabadiliko makubwa.

**Ukarimu huonyesha watu moyo wako na moyo wa Mungu kuwahusu.**



Gary Keesee ni mwandishi, mmnenaji, mjasiriamali, mtaalamu wa fedha, na mchungaji ambaye ana shauku ya kusaidia watu kuwa washindi maishani, hasa katika maeneo ya imani, familia, na fedha. Gary na mkewe, Drenda, wameanzisha biashara kadhaa zilizo na fanaka, na ndio waanzilishi wa huduma iitwayo Faith Life Now, ambayo ina vipindi viwili vya televisheni—*Fixing the Money Thing* na *Drenda*, kongamano kote ulimwenguni, na rasilimali za vitendo. Wao pia ni wachungaji wa Kanisa la Faith Life karibu na Columbus, Ohio.

P. O. Box 779, New ALBANY, OH 43054, USA